ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.

13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.

25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
32.Mhe. Said Hassan Said	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake

43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo

65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	Jimbo la Jang'ombe
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Thalathini na Moja - Tarehe 26 Juni, 2015

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Taarifa ya Spika ya leo ni ndogo sana lakini muhimu. Waheshimiwa Wajumbe, tumekuwepo katika shughuli zetu za Baraza la Nane kazi ambayo ilianza mnamo tarehe 11/11/2010 na tunaendelea kushirikiana kwa muda waote wa miaka 5 hadi leo hii tunategemea tukamilishe shughuli zetu za muhula wa miaka 5. Ambapo kama mlivyoarifiwa kabla Mhe. Rais tunamtegemea ahutubie Baraza letu hili kunako saa 9:30 wakati wa Alasiri. Kuna mengi katika kipindi hiki cha kibinaadamu yanaweza yakawa yametokezea. Mengine yanaweza yakawa mazuri, mengine yasiwe mazuri, ni udhaifu wa kibinaadamu ndio ambao unaweza ukatupelekea ama kuteleza au wakati mwengine kunyoosha na mambo yakawa mazuri.

Kwa hivyo, kwanza nianze, mimi kama Spika, kama kuna jambo lolote ambalo limetokezea kuwa nimewakwaza Waheshimiwa Wajumbe, naomba sana tusameheane kwa kipindi chote kile tukiwa ndani ya shughuli zetu ndani ya Baraza, lakini hata wakati mwengine katika shughuli nyengine za kwenye Kamati, lakini nyengine za Ofisini kwa sababu wakati wowote wajumbe wanapokuja Ofisini na kuwa na jambo ambalo wameshauri baadhi ya wakati ushauri huo tunauchukua na tunaufanyia kazi, lakini wakati mwengine ushauri huo tunaona kwamba haukukaa vyema.

Sasa inawezekana sana mkaona ee, Spika, hapa leo amendikwaza. Kwa hivyo, kwa yote yale ambayo yametukwaza kwa njia moja au nyengine katika shughuli zetu za humu ndani za kwenye kamati lakini hata shughuli nyengine za kawaida za kiofisi basi mimi binafsi naomba sana muniwie radhi kwa hayo mambo ambayo yatakuwa yameweza kutokezea.

Lakini kwa upande wangu mimi kwa sababu ya kuelewa utaratibu wa shughuli za hapa ulivyo na ndio demokrasia yenyewe, hakuna hata moja ambalo wajumbe mmefanya likawa limenikwaza kwa upande wangu. Unaweza wakati fulani ukaniona nimekunja uso kidogo ni sehemu ya maumbile yangu nilivyo, lakini pia ni kwa sababu hilo jambo tunataka kuhakikisha kwamba tunapata njia iliyo sahihi zaidi na mpaka tunafikia leo, nadhani tumefanya kazi nzuri sana. Na inafaa

tujipongeze sana kwa kazi nzuri ambayo tumekuwa na mashirikiano nanyi na kiti kwa muda wote wa miaka 5. *(Makofi)*

Kwa mnasaba huo nataka nitoe shukurani za dhati kwanza kwa Mhe. Naibu Spika, Mhe. Ali Abdalla Ali, wakati mwengine huyu bwana huwa ninamwambia, anapewa taarifa usiku keshapumzika kwamba kesho uingie Barazani, hajawahi kuniambia kwamba kwa kweli kesho naona kidogo itakuwa tatizo, muda wote anaitikia *hewalla*. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, anastahili kupata pongezi zote. *(Makofi)*

Lakini pili nimshukuru, naanza mmoja mmoja maana ukitaja kwa pamoja ni kuwa kidogo ina ugumu wake. Nimshukuru Mhe. Mwenyekiti wa Baraza hili Mhe. Mgeni Hassan Juma, naye amenisaidia sana, amenisaidia sana si tu katika kuendesha shughuli za hapa, lakini ameweza kuendesha hata ile Jumuiya tunayo *NGO's* yetu hapa ya UWAWAZA, Jumuiya ile kati ya Jumuiya zetu tatu ziliopo hapa Barazani ndio iliyo hai na imehuishwa kwa kiasi kikubwa na yeye pamoja na wenzake Wajumbe wa UWAWAZA. Kwa hivyo, Mwenyekiti, Mhe. Mgeni Hassan Juma, ametuwakilisha vizuri sana ndani ya Baraza hili lakini hata nje ya hapa kwa sababu mialiko mingi sana huwa inatolewa kwa UWAWAZA na huwa anakwenda na anashiriki vizuri sana. Taarifa huwa ananipa kuhusu yale ambayo ameyafanya kwa niaba ya UWAWAZA, lakini hatimaye kwa niaba ya Baraza kwa sababu UWAWAZA wajumbe wake ni sehemu ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa, Mwenyekiti mwenza wa Mhe. Mgeni Hassan Juma, hawa wako *a par* na yeye amesaidia sana, nafasi yake ninapoona ananiletea viji-*notes* vingi vingi sana ni kunikumbusha kwamba kuna jambo fulani linaweza likatokezea, kwa hivyo, ninakujulisha jambo hilo tujitayarishe kama litaweza kutokezea, anafanya sana kazi hiyo. Kwa hivyo, nichukuwe nafasi neye kumshukuru si tu kwa kuendesha hichi chombo, lakini pia amekuwa ananipa taarifa ya mambo ambayo yanaweza yakajitokeza mapema ili niweze kujua nini cha kufanya ili hatimaye jambo hilo liende vizuri. Mhe. Mwenyekiti, Mahmoud Mohammed Mussa, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

Shughuli nzuri hizo zimekuwa hivi kwa sababu ya mashirikiano makubwa ya watendaji wote wakiongozwa na Katibu wa Baraza la Wawakilishi ndugu yetu Yahya Khamis Hamad, sijawahi kusikia yeye na watendaji wake wakikwazana na wakitofautiana kwa mnasaba wa shughuli za Baraza. Kwa hivyo, mashirikiano yao yamesaidia sana kuona wametusaidia katika shughuli za Baraza lakini wamekusaidieni nyinyi Waheshimiwa Wajumbe, pale ambapo mnakuwa na haja ya jambo fulani litengenezwe kwa msaada wa watendaji hao. Nichukuwe nafasi kuwashukuru wote kwa jumla kwa kazi yao nzuri. *(Makofi)*

Lakini humu ndani kuna vijana wanaotembea tembea kutwa nzima asubuhi na jioni ili pale ambapo Mhe. Mjumbe, yeyote ana haja basi awahi kumsaidia na kumsikiliza ili kufanya mawasiliano mazuri humu ndani lakini wakati mwengine tunawatuma hata nje ya hapa katika ukumbi wa Baraza. Kwa ujumla wao ninawashukuru sana kwa kazi hiyo nzuri. *(Makofi)*

Shughuli zetu zimekuwa zinaeleweka sana nje huko kwa msaada mkubwa sana wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kutuma vijana wake hapa wa *ZBC Television* na *ZBC Radio* na wao wanafanya kazi ambayo mara nyingi mmekuwa mnaipigia mfano na kuwatetea kwamba kazi yao ni kubwa na kwa kweli kazi ni kubwa sote tunakubali hivyo na sijawahi kuona kwamba *camera* hizi siku hata moja wakati wa vikao zimeondolewa kwamba hakuna watu wanaoifanyia kazi shughuli hiyo ya kutangaza shughuli zetu kwa wananchi wetu tunaowawakilisha.

Nichukuwe nafasi kuwashukuru sana vijana wetu hawa wa *ZBC Radio* na *ZBC Television* kwa kazi nzuri ya kututangaza vizuri kwa Watanzania kwa ujumla. Shughuli hizi zinakwenda vizuri kwa sababu ya Wenyeviti wa Kamati mbali mbali na wajumbe wao ndani ya Kamati hizo na Makatibu wao ndani ya Kamati hizo kwa ujumla wao nao niwashukuru sana, kwamba wametusaidia kufanikisha shughuli zetu za hapa kwa vizuri na kwa ufanisi mkubwa.

Waheshimiwa Wajumbe, ninakushukuruni wanapokuja wageni wetu mbali mbali mnawapokea kwa hongera nyingi sana. Shukurani nyingi zije kwenu na leo kama mnavyoona mna makaratasi mengi pale ya kuonesha wageni ambao watakuja ambao nitaomba pia muwapongeze kama ilivyo kawaida yenu. *(Makofi)*

Kwa kifupi Waheshimiwa Wajumbe, Baraza letu hili limepata sifa nzuri sana, ukiachia kasoro mbili tatu za hapa na pale, ndio kawaida ya vyombo hivi, lakini limepata sifa nzuri sana kwa wananchi wa Zanzibar lakini kwa wananchi wa Tanzania kwa ujumla. Lakini tushukuru vile vile ufanisi wetu na bila ya kuwa na mivutano hata wenzetu nje duniani huko wanatusifu, kwa mfano juzi juzi tu nilipokuwa nje, Waheshimiwa Wajumbe, kawaida yenu na utamaduni wenu ni mzuri sana, makofi mengi hayo ni kutambua ujio wa Mheshimiwa mama Asha Balozi, mke wa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Idd, naye ni yule pale ninamuomba asimame ili mumpigie makofi kwa wingi zaidi. Tumemualika jioni wakati wa Alaasiri lakini ameona kwa uhondo wa chombo hiki na kwa kawaida yetu aje kuanzia hivi asubuhi, tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe, mimi ninakushukuruni sana, kwa kweli tumejenga sura nzuri sana duniani, walipokuwa wananiuliza katika ziara yetu ya mwisho pale katika Bunge la *European Union*, wakaniuliza je, hivi huko

mnarushiana rushiana viti, mnapigana pigana? Nimewaambia hapana hicho kitu hakipo. Walisema kwenye Mabunge mengine hayo ni mambo ya kawaida, walifurahi sana na wakasifu, yaani wakakusifuni nyinyi kwa mashirikiano makubwa mnayonipa mimi kiasi cha kwamba tukaweza kufanya kazi vizuri. Niliokwenda nao ziara ile wengine ninasikitika kwamba hawapo haya ninayoyasema yote walishuhudia na sifa zote hizo tulipewa na kuzipokea kwa niaba yenu. *(Makofi)*

Basi Waheshimiwa Wajumbe, itoshe shukurani hizo, pale ambapo kuna yeyote ambaye sikutoa shukurani kwake na kweli wapo wale ambao wanawaambia wenzetu pale kwa lugha ya watu wasiosikia na lugha ya watu ambao hawawezi kusema, basi nao tunawashukuru sana kwa sababu watu hao wenye ulemavu nao ni sehemu ya jamii ya Watanzania, ni sehemu ya jamii ya Wazanzibari. Ninawashukuru sana kwa kazi hiyo nzuri nao wamekuwa wanajitahidi kuwapa taarifa kinachoendelea humu ndani ambao wao hawawezi kusikia, lakini pia hawawezi kusema lakini wanaona. Kwa hivyo, ninawashukuru sana na wao kwa kazi nzuri.

Waheshimiwa Wajumbe, kikao cha leo cha asubuhi kilikuwa na taarifa hiyo ya Spika, lakini kuna taarifa nyengine ya mwenzetu Kiongozi wa Shughuli za Serikali ndani ya Baraza hili, nichukuwe nafasi sasa nimkaribishe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, ili na yeye atoe maelezo juu ya shughuli zetu za miaka 5 ambayo inamalizika leo kikazi ili na yeye awe amepata nafasi ya kusema neno kwa sababu maneno yake huyu huwa anasema sema mwisho wa shughuli zetu.

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Kiongozi wa Shughuli za Serikali ndani ya Baraza hili karibu sana. *(Makofi)*

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, sina budi kuanza hotuba yangu hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehema kwa kutujaalia uhai, uzima, afya njema na kutuwezesha kumaliza Mkutano huu wa 20 wa Baraza la Wawakilishi la Nane kwa mafanikio makubwa. Aidha, nachukua nafasi hii kukupongeza na kukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa umahiri na umakini wako mkubwa wa kuliendesha Baraza hili Tukufu kwa kipindi chote cha Uongozi wako. Sisi sote ni mashahidi kwa namna ulivyodhihirisha uwezo na uzoefu wako wa kuliongoza Baraza hili katika kuisimamia na kuishauri serikali juu ya utekelezaji wa mipango mbali mbali ya kuwaletea wananchi wetu maendeleo. Kwa kweli umetuongoza vizuri. (*Makofi*)

Pia, napenda kumshukuru Mhe. Naibu Spika, pamoja na Waheshimiwa Wenyeviti wote wa Baraza kwa kukusaidia ipasavyo katika kuviendesha vikao vya Baraza hili.

Mhe. Spika, naomba kutoa shukrani za pekee pamoja na kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa uongozi wake uliojaa hekima na busara kubwa ambao umeiwezesha nchi yetu kuzikabili changamoto za kiuchumi na kisiasa na kupiga hatua za kimaendeleo. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mhe. Rais kwa imani yake kwangu ya kuniteua kushika nafasi ya Makamu wa Pili wa Rais katika kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya Saba chini ya uongozi wake.

Mhe. Spika, vile vile, napenda kumshukuru sana Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad, kwa kumsaidia na kumshauri Mhe. Rais katika kuiongoza nchi yetu. Aidha, namshukuru Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mashirikiano yake makubwa kwangu binafsi na kwa Ofisi yangu katika kutekeleza mipango na malengo yaliyowekwa na serikali. Hakika katika kipindi hiki cha miaka mitano, Serikali ya Kwanza yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa imefanya kazi nzuri sana ya kuiletea nchi yetu maendeleo.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii pia kuwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kuwasilisha bajeti za wizara zao na kujibu vizuri na kwa umakini mkubwa hoja mbali mbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wawakilishi. Ni matumaini yangu kwamba, Waheshimiwa Wajumbe na wananchi waliokuwa wakifuatilia kwa karibu zaidi mijadala ya mkutano huu wamefaidika na majibu na ufafanuzi uliotolewa.

Vile vile, nawashukuru na kuwapongeza sana Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa michango, mapendekezo na ushauri wao waliotoa wakati wa kuzijadili Hotuba za Bajeti zilizowasilishwa hapa Barazani. Nawashukuru Wajumbe wote kwa kuzipitisha bajeti hizo bila ya pingamizi zozote. Kwa kweli katika mikutano yote ya Baraza lako tukufu, mkutano huu ulikuwa wa kupigiwa mfano kwa kupitisha bajeti zote kwa urahisi.

Upitishaji wa bajeti hizo ulikuwa rahisi zaidi kwa sababu ya kutumia mfumo mpya wa bajeti ulioitwa "*Program Based Budget*" (*PBB*). Buti hazikuwa nyingi mara hii ukifananisha na bajeti zilizopita. Nawashukuru sana Wajumbe kwa ushirikiano wao. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa naomba kuchukuwa fursa hii kuwakumbuka wenzetu waliokwishafika mbele ya haki ambao walikuwa Wajumbe wa Baraza hili. Wajumbe hao ambao wametutoka katika kipindi cha miaka mitano (5) hii ni Marehemu Mussa Khamis Silima, aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Uzini ambae alifariki tarehe 23 Agosti, 2011, Marehemu Salum Amour Mtondoo, aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Bububu ambae alifariki tarehe 15 Machi, 2012, Marehemu

Salmin Awadh Salmin, aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni aliyefariki tarehe 19 Februari, 2015 na Marehemu Ali Khamis Abdalla aliyekuwa Spika Mstaafu alifariki tarehe 8 Agosti, 2014.

Mhe. Spika, viongozi hao walikua mahodari, wenye msimamo thabit, makini na shupavu na walijitolea kwa hali na mali katika kuwatumikia wananchi kwa kipindi chote cha uhai wao. Hatuna budi kuyaenzi na kuyaendeleza yale yote mazuri na mema ambayo wenzetu hao wametuachia kwa manufaa ya nchi yetu. Kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar naendelea kuwapa pole Waheshimiwa Wajumbe, wanafamilia na wananchi wote kwa ujumla kwa misiba hii. Sisi sote ni waja wake Mwenyezi Mungu na bila ya shaka marejeo yetu ni kwake. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu hao mahala pema peponi. *Amin.*

Mhe. Spika, kama tunavyoelewa kwamba Mkutano huu wa 20 ni mkutano wa mwisho kabla ya kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu hapo tarehe 25 Oktoba, 2015. Hivyo, natoa shukurani za dhati kwako wewe Mhe. Spika, viongozi wote na wafanyakazi wa Baraza kwa mashirikiano makubwa katika kuliendesha Baraza katika kipindi chote cha miaka mitano (5). Nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na Wakuu wa Mashirika yote ya Umma kwa bidii na juhudi kubwa katika kutekeleza majukumu yao waliyopangiwa. Jambo ambalo limechangia sana katika hatua za maendeleo tuliyopata katika nchi yetu. Nawashukuru wananchi wote wa Zanzibar kwa utulivu wao na mashirikiano yao na serikali katika harakati za kuiletea maendeleo nchi yetu. Ni imani yangu kwamba, wananchi wote wataendelea kuiamini na kuiunga mkono serikali yao inayoongozwa na Rais kutoka CCM, na watashiriki katika harakati za Uchaguzi Mkuu ujao kwa upendo, amani na utulivu uliokwisha jengeka miongoni mwa jamii yetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mafanikio tuliyoyapata katika Kipindi cha Kwanza cha Awamu ya Saba katika sekta mbali mbali ikiwemo Sekta ya Afya, Elimu, Utalii, Maji, Miundombinu na Mawasiliano na katika Sekta za Uzalishaji (viwanda, kilimo, mifugo na uvuvi) ni ya kupigiwa mfano na tuna kila sababu ya kumpongeza Rais wetu Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein kwa mafanikio haya makubwa. Mafanikio haya makubwa yametokana na utekelezaji sahihi wa Ilani ya CCM ya mwaka 2010 – 2015. Sina shaka kwa mafanikio haya, Rais Dkt. Ali Mohammed Shein atarudi tena kuiongoza serikali hii yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kama tunavyojua kwamba Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ni moja kati ya mihimili mitatu ya nchi yetu ambalo ndilo lenye Mamlaka ya Kutunga Sheria na Kusimamia Utekelezaji wa Shughuli za Umma kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 5 A (1) na (2) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984.

Mhe. Spika, Baraza hili la Nane hadi sasa limeshafanya jumla ya mikutano 20. Katika mikutano hiyo, jumla ya maswali ya msingi 1,630 na maswali ya nyongeza 3,277 yameulizwa kwa serikali na kujibiwa. Aidha, Baraza limefanikiwa kujadili na kupitisha Miswada ya Sheria 63 na hatimaye kutungwa Sheria kutokana na Miswada hiyo. Pia, Baraza hili limeidhinisha Bajeti ya Serikali na Mawizara mara tano (5) hadi sasa. Bajeti ambazo zimesaidia kufanikisha kupatikana kwa maendeleo makubwa nchini mwetu.

Mhe. Spika, vile vile, Baraza hili la Nane liliunda jumla ya Kamati Teule tano (5) ambazo zilikuwa kama zifuatazo:-

a. Kamati Teule ya Kuchunguza Baraza la Manispaa.
b. Kamati Teule ya Kuchunguza Utendaji wa Shirika la Umeme (*ZECO*).
c. Kamati Teule ya Kuchunguza mambo mbali mbali yaliyoibuka kwenye majadiliano ya Bajeti ya mwaka 2011/2012.
d. Kamati Teule ya Kuchunguza Migogoro ya Ardhi.
e. Kamati Teule ya Kuchunguza Upotevu wa Nyaraka.

Ripoti za Kamati Teule zote ziliwasilishwa serikalini na kuchukuliwa hatua zilizostahili.

Mhe. Spika, Baraza pia lilipokea na kujadili hoja binafsi za Wajumbe kama ifuatavyo:-

a. Hoja ya Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura, inayohusu Mkopo wa Elimu ya Juu.
b. Hoja ya Mhe. Hija Hassan Hija, Mwakilishi wa Jimbo la Kiwani, inayohusu Utendaji wa Shirika la Umeme (*ZECO*).
c. Hoja ya Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mwakilishi Viti Maalum, inayohusiana na vitendo vya Udhalilishaji wa Watoto, Zanzibar.
d. Hoja ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni inayohusiana na Uimarishaji wa Huduma za Afya zinazotolewa kwa wananchi wa Zanzibar, na
e. Hoja ya Mhe. Hamad Masoud Hamad, Mwakilishi wa Jimbo la Ole inayohusu Ucheleweshaji wa Upatikanaji wa Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

Hoja zote hizo zilipokelewa na Baraza lako tukufu, kujadiliwa na kutolewa maamuzi stahili.

Mhe. Spika, moja kati ya mambo makubwa na muhimu yaliyofanyika ndani ya Baraza hili la Nane ni Wajumbe wa Baraza lako kushiriki katika Bunge Maalum la Katiba kwa lengo la kuandaa Katiba Inayopendekezwa. Napenda kuchukua fursa

hii kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe, wote kwa ushiriki wao uliowezesha kupatikana kwa Katiba Inayopendekezwa ambayo hivi sasa inasubiri kupigiwa kura ya maoni na wananchi. Katiba hii inayopendekezwa imesaidia kutatua kero nyingi zilizokuwa zinalalamikiwa na upande wa Zanzibar. Miongoni mwa kero hizo ni kutolewa kwa suala la mafuta na gesi asilia kutoka kwenye orodha ya mambo ya Muungano. Katiba hiyo imelitoa suala la mafuta na gesi asilia kutoka kwenye orodha hiyo. Kero hiyo ni miongoni mwa kero nyingi zilizokuwa zinalalamikiwa ambazo tayari zimekwisha patiwa ufumbuzi kupitia Katiba Inayopendekezwa.

MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SABA:

Mhe. Spika, katika kipindi hiki cha Awamu ya Saba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa tumeshuhudia maendeleo makubwa ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kwa upande wa kisiasa, serikali imeweza kuimarisha Umoja wa Kitaifa na mshikamano wa wananchi wetu bila ya kujali itikadi zao za kisiasa. Hali ambayo imepelekea kuimarika kwa uvumilivu wa kisiasa miongoni mwa viongozi na wanachama wa vyama vya siasa na wananchi kwa ujumla.

Mhe. Spika, kwa upande wa maendeleo ya kiuchumi, hali ya uchumi wetu imeimarika kwa kasi na umekua kutoka asilimia 5.2 mwaka 2010 hadi asilimia 7.4 mwaka 2015. Ukuaji huo unatokana na kuimarika kwa sekta ya kilimo, misitu, uvuvi, viwanda na utalii. Kasi ya mfumko wa bei imepungua kutoka asilimia 6.1 mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 5.6 mwaka 2014. Hali hii inatokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa ndani unaotokana na juhudi zilizochukuliwa na serikali katika kuwapatia ruzuku za pembejeo wakulima wetu. Katika kipindi hiki cha miaka mitano (2010 – 2015), Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetoa fidia ya jumla ya Shs. 7,129,591,148 za kuendeleza kilimo, kwa ajili ya ununuzi wa mbolea, madawa, mbegu na kutoa huduma za matrekta kwa wakulima.

Mhe. Spika, kilimo bado kinaendelea kuwa ni muhimili mkuu wa uchumi wetu na ndicho kinachotoa ajira kwa wananchi walio wengi, kwa kutambua hilo serikali imeweza kutekeleza programu na miradi mbali mbali ya kilimo. Juhudi hizi zimepelekea kuimarika utoaji wa elimu kwa wakulima wa mazao ya chakula, biashara, viungo na matunda, matumizi ya pembejeo, matumizi ya zana za kisasa za kilimo ikiwemo matrekta na miundombinu ya umwagiliaji maji mashambani.

Mhe. Spika, serikali imeendelea kuliimarisha na kuliendeleza zao la karafuu kwa kuotesha miche na kugaiwa bure kwa wakulima wetu Unguja na Pemba. Aidha, wakulima wetu wameendelea kupatiwa taaluma ya kilimo bora cha karafuu ikiwemo uimarishaji wa vitalu vya miche ya mikarafuu, uchanganyaji wa mazao

mengine (*mixed cropping*), uvunaji na uanikaji bora wa zao hili. Lengo ni kuhakikisha upatikanaji wa karafuu kwa wingi na zenye viwango vitakavyoipatia nchi yetu bei nzuri katika soko la dunia, ndiyo maana serikali inawahamasisha wakulima kuyaweka mashamba yao ya mikarafuu katika hali ya usafi. Serikali kwa upande wake inajitahidi kuyaweka mashamba ya serikali ya mikarafuu katika hali ya usafi.

Mhe. Spika, serikali kwa kushirikiana na Kampuni ya Bakhressa imeendelea na juhudi za kuimarisha maeneo huru ya kiuchumi ya Fumba. Mpango ulokuwepo ni kuendeleza eneo la Fumba uwe miongoni mwa miji ya kibiashara nchini. Kupitia jitihada hizo, ujenzi wa miundombinu ya barabara, maji na umeme unaendelea, na kwa kuanzia barabara mbili zenye urefu wa kilomita 4.2 ujenzi umekamilika. Aidha, kiwanda cha kuzalisha bidhaa zitokanazo na maziwa kinafanya kazi na kinaendelea kutoa ajira kwa vijana wetu.

Mhe. Spika, Sekta ya Utalii imeendelea kuimarika. Idadi ya watalii walioingia nchini imeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka na kufikia watalii 274,619 mwaka 2015. Ongezeko hili linatokana na kuimarika kwa miundombinu ya utalii pamoja na hali ya amani na utulivu uliopo nchini. Nawaomba viongozi na wananchi wote kuendelea kudumisha amani katika nchi yetu hasa katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu ili utalii wetu uzidi kuimarika na uchumi wetu uzidi kukua. Serikali inawahakikishia watalii wetu hao usalama wao kwa kipindi chote ambacho watakuwa nchini mwetu.

Katika kuimarisha zaidi Sekta hii ya Utalii, Serikali imeamua kuibadilisha mandhari ya Hoteli ya Bwawani, hoteli ambayo ina historia kubwa baada ya kupatikana mwekezaji ambaye yuko tayari kuibadilisha hali hiyo. Mazungumzo baina ya serikali na mwekezaji yamefikia mbali na sasa bado tu serikali kumkabidhi mradi huo kwa mwekezaji na kufunga naye mkataba.

Mhe. Spika, Sekta ya Miundombinu nayo imepata mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa barabara mpya kwa kiwango cha lami zenye urefu wa kilomita 243.85 kwa Unguja na Pemba. Vile vile, barabara zenye urefu wa kilomita 39.3 zimejengwa kwa kiwango cha kifusi. Aidha, barabara zenye urefu wa kilomita 656 zimefanyiwa matengenezo mbali mbali. Ni matumaini yangu kwamba, ujenzi wa barabara hizi utasaidia ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

Hivyo, napenda kutoa wito kwa watumiaji wa barabara hizi na wananchi kwa ujumla kuzitunza kwa faida yetu na vizazi vyetu vijavyo. Wale wenzetu wenye tabia ya kuchoma barabara hizo kwa makusudi waiache tabia hiyo kwani inaigharimu serikali fedha nyingi kuzitengeneza tena barabara hizo. Serikali itawachukulia hatua kali waharibifu hao.

Mhe. Spika, serikali kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya Usafiri Baharini imeendelea kuimarisha usafiri wa baharini kwa kujenga majengo mapya ya kuhudumia abiria katika bandari ya Malindi Unguja. Aidha, serikali imeshanunua meli mpya huko Korea yenye uwezo wa kuchukua abiria 1,200 na tani 200 za mizigo ambayo inatarajiwa kuwasili mwishoni mwa mwezi wa Julai mwaka huu hapa nchini. Aidha, serikali imeendelea kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kuendeleza dhamira ya ujenzi wa bandari mpya, kubwa na ya kisasa katika maeneo ya Mpigaduri ambapo hatua za uchambuzi yakinifu, michoro pamoja na makubaliano ya ujenzi huo na Kampuni ya China *"Habour Engeneering Company"* yamekamilika.

Vile vile, Serikali inaendelea na utaratibu wa kuziendeleza bandari zetu zote za Unguja na Pemba. Uamuzi wa ujenzi wa bandari ya Mpigaduri ulifanywa na Serikali ya Awamu ya Tano kuendelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita na Serikali ya Awamu ya Saba ndiyo iliyoendeleza mradi huo kwa kutafuta wafadhili wa kuijenga bandari hiyo.

Ilani ya CCM ya mwaka 2010 – 2015 kifungu 143 (e) inasema;

> "Kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkuu (*Master Plan*) wa bandari ya Malindi, ikijumuisha huduma za bandari huru na kuendelea kutafuta uwezo wa kujenga bandari mpya ya kibiashara ya Mpigaduri".

Mhe. Rais, anafanya kazi kubwa sana kuhakikisha kuwa mradi unatekelezwa na ndiyo tumefikia hapa tulipo. Mradi huu utaanza kujengwa mara tu baada ya mradi wa *Terminal II* utakapokamilika. Hivyo, serikali itakayokuja itauendeleza tu mradi huu na siyo kuanza upya.

Mhe. Spika, kwa upande wa usafiri wa anga, serikali imejenga maegesho na njia za kupitia ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume. Vile vile, ujenzi wa jengo jipya la abiria la kiwanja hicho unaendelea vizuri na unatarajiwa kukamilika mwezi wa Oktoba mwaka huu. Aidha, serikali inaendelea na uimarishaji wa Uwanja wa Ndege wa Sheikh Abeid Amani Karume - Pemba kwa kuuwekea taa na kuufanyia matengenezo katika njia yake ya kurukia na kutulia ndege. Kukamilika kwa ujenzi huo kutaimarisha utoaji wa huduma za abiria na mizigo katika viwanja vyetu vyote nchini.

Mhe. Spika, mafanikio makubwa yameweza kupatikana katika Sekta ya Elimu katika ngazi zote kuanzia elimu ya awali, msingi, sekondari na elimu ya juu. Miongoni mwa mafanikio hayo ni kupunguza tatizo la upungufu wa walimu, maabara, vitabu vya kiada na ziada pamoja na uhaba wa madarasa na samani.

Aidha, serikali imefanikiwa kwa asilimia 100 kuwaandikisha wanafunzi wote waliotarajiwa kuanza darasa la kwanza mwaka 2015.

Mhe. Spika, serikali pia imeendeleza ujenzi wa skuli za sekondari na kukamilisha ujenzi wa skuli za msingi ambazo zimekuwa zikianzishwa na wananchi wenyewe katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu. Sambamba na mafanikio hayo, serikali imeendelea kuwapatia Mikopo ya Elimu ya Juu wanafunzi ili kuwawezesha kujiunga na vyuo mbali mbali ndani na nje ya nchi. Aidha, serikali imekuwa ikishirikiana na Vyuo Vikuu vilivyopo Zanzibar ili kuongeza fani za masomo kuanzia ngazi ya Shahada ya Kwanza na kuendelea ili kupata wataalamu wa fani mbali mbali.

Mhe. Spika, kupitia Baraza lako tukufu napenda kutoa wito kwa wananchi kuendelea kushirikiana na serikali katika jitihada za ujenzi na usimamizi wa skuli katika maeneo yao. Aidha, natoa wito kwa wale wote waliopatiwa Mikopo ya Elimu ya Juu kulipa mikopo hiyo ili kuwawezesha wanafunzi wengine kupata huduma hiyo.

Mhe. Spika, serikali inaendelea na juhudi zake za kupambana na magonjwa mbali mbali ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza. Zanzibar imekuwa mfano kwa nchi za Afrika Mashariki na dunia kwa kuweza kutokomeza ugonjwa wa Malaria. Aidha, serikali inaendelea kuiimarisha Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kujenga na kuweka vifaa vya kisasa ili kuipandisha daraja na kuwa hospitali ya Rufaa na kwa upande wa Hospitali za Kivunge, Makunduchi na Chake Chake kuwa Hospitali za Wilaya. Hospitali za Abdalla Mzee Mkoani na Hospitali ya Wete zinaimarishwa ili ziweze kupandishwa daraja na kuwa Hospitali za Mkoa.

Katika mwendelezo wa kuimarisha huduma ya afya kwa wananchi wetu, serikali imezipatia hospitali vifaa vya kisasa pamoja na usambazaji wa dawa kwa wananchi. Vile vile, Serikali ya Awamu ya Saba kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo imeweza kujenga Bohari Kuu ya Dawa ya kisasa ambayo ni mfano katika nchi za Afrika Mashariki na Kati.

Mhe. Spika, UKIMWI na Dawa za Kulevya ni miongoni mwa matatizo yanayoathiri makundi mbali mbali ya watu, hasa vijana. Katika suala la UKIMWI, kiwango cha mambukizi kimeendelea kubakia kuwa asilimia 0.6 na idadi ya watu walioambukizwa virusi vinavyosababisha UKIMWI (*VVU*) waliosajiliwa ni 7,820. Kati ya hao watu 5,375 wanapata huduma ya *ARV*. Katika kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI, serikali imechukuwa hatua mbali mbali, zikiwemo kuimarisha huduma za tiba, huduma za kuzuia maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto.

Aidha, serikali imesambaza mashine tatu mpya za *CD4* ambazo zimepelekwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, Mwembeladu, na Kivunge, na mashine aina mbili za "*Haematology*" na "*Chemistry*" zimesambazwa katika Hospitali za Micheweni, Makunduchi, na Mwembeladu. Pia, Serikali imeimarisha vituo vya ushauri nasaha na upimaji wa *VVU*. Vile vile, Serikali kwa kushirikiana na Taasisi zisizo za Serikali (*NGO's*) inaendelea na shughuli za kuelimisha jamii juu ya mapambano dhidi ya UKIMWI na kupunguza unyanyapaa kwa watu wanaoishi na *VVU*. Pia, vituo vinavyotoa huduma ya ushauri nasaha na upimaji wa *VVU* vimeongezeka kutoka vituo 87 mwaka 2012 hadi kufikia vituo 91 mwaka 2015. Kati ya hivyo, Unguja 58 na Pemba 33. Vile vile, serikali inaendelea kuwahamasisha wananchi kuwa na tabia ya kupima afya zao na kujiepusha na maambukizi mapya ya UKIMWI.

Mhe. Spika, kwa upande wa tatizo la dawa za kulevya, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inasimamia utekelezaji wa Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Na. 12 ya mwaka 2011. Mpango Maalum (*Road Map*) wa Utekelezaji wa Sheria hiyo umeandaliwa na unatekelezwa kwa kushirikisha wadau kutoka Taasisi mbali mbali za serikali na zisizo za Serikali ili kuhakikisha kwamba michango mbali mbali inatolewa kudhibiti uingizaji, usafirishaji, usambazaji na matumizi ya dawa za kulevya. Vile vile, serikali imeandaa Sera ya Dawa za Kulevya na kufanya mikutano na vyombo vya kusimamia sheria (*Law Enforcement Agency)* ili kukuza mashirikiano na vyombo hivyo katika kudhibiti Dawa za Kulevya.

Mhe. Spika, ujenzi wa Kituo Maalumu cha Kurekebisha Vijana walioathirika na Dawa za Kulevya katika eneo la Kidimni, Wilaya ya Kati unaendelea. Aidha, Nyumba za Marekebisho ya Tabia (*Sober Houses*) 13 zimeanzishwa ambazo zimetoa huduma kwa vijana 1,020 kwa Unguja na Pemba. Serikali imechukua jitihada kubwa ya kuziendeleza nyumba hizo ili ziweze kutoa huduma zinazostahiki. Serikali kupitia Vituo vya Ushauri Nasaha imeendelea kutoa ushauri nasaha kwa waathirika wa dawa za kulevya. Pia, taaluma juu ya athari za Dawa za Kulevya imetolewa katika shehia mbali mbali za Unguja na Pemba, Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na skuli kupitia mikutano, makongamano, semina pamoja na utoaji wa kalenda na vipeperushi.

Mhe. Spika, serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo inaendelea na jitihada zake za kuwapatia wananchi wake huduma bora ya maji safi na salama. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali ya Awamu ya Saba imetekeleza Miradi 10 na Programu mbili (2) za kuwapatia wananchi wake maji safi na salama pamoja na kuendeleza Mpango wa Kulinda Vyanzo vya Maji Unguja na Pemba. Vile vile, serikali imeifanyia matengenezo makubwa miundombinu ya usambazaji maji katika maeneo mbali mbali mjini na vijijini ili kuhakikisha kuwa huduma ya maji

inapatikana kwa wananchi wakati wote bila ya usumbufu. Serikali imechukua hatua maalumu ya kuziondosha mita 41 za TUKUZA zilizokuwepo katika visima mbali mbali vya miradi ya maji ili kuwaondoshea kero wananchi na kuhakikisha wanapata huduma ya maji safi na salama bila ya usumbufu.

Mhe. Spika, ili kuhakikisha kwamba Zanzibar inakuwa na umeme wa uhakika, serikali imesimamia kikamilifu utekelezaji wa mradi wa kujenga njia ya pili ya umeme inayopita chini ya bahari kutoka Ras Kiromoni Tanzania Bara hadi Fumba Unguja. Pamoja na hatua hiyo, serikali pia imo katika juhudi ya kutafuta miradi ya umeme mbadala kwa kutumia ama jua, upepo au mawimbi ya baharí, hii itategemea na utafiti unaofanywa kujua ni aina gani ya umeme unaotufaa kwa mazingira yetu hapa nchini.

Aidha, kwa msaada wa Serikali ya Norway, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeunganisha umeme toka Majani Mapana, Tanga hadi Wesha huko Pemba ili wananchi wa Pemba wapate umeme wa uhakika. Umeme huu una nguvu ya 20*MW*, hadi sasa ni matumizi ya 6*MW* tu ndiyo yaliyofikiwa. Waya huu unaweza kuishi kwa muda wa miaka 30 hadi 40. Umeme huu umeanza kutumika kuanzia mwaka 2010.

Mhe. Spika, katika kuendeleza matumizi bora ya ardhi nchini (*Land Use Planning*), serikali imekamilisha Mpango Mkuu wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Ardhi wa Zanzibar. Utekelezaji wa Mpango huu utasaidia kupunguza matumizi holela ya ardhi. Sambamba na Mpango huo, serikali imetayarisha Sheria ya kuanzisha Kamisheni ya Ardhi itakayosimamia matumizi yote ya ardhi nchini. Aidha, serikali imeendelea kuziimarisha Mahakama za Ardhi kwa kuzipatia vitendea kazi na kuziongezea idadi ya Mahakimu. Juhudi zote hizi zimelenga katika kupunguza tatizo la migogoro ya ardhi hapa nchini. Ni matumaini yangu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu watasaidia kuhakikisha kuwa migogoro ya ardi inakuwa historia nchini mwetu.

MAMBO YALIYOJADILIWA KATIKA MKUTANO WA 20:

Mhe. Spika, Mkutano huu wa 20 ulikuwa ni mkutano wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ambapo Bajeti ya Serikali, Mpango wa Maendeleo pamoja na bajeti za wizara zote ziliwasilishwa, kujadiliwa na kupitishwa. Aidha, katika Mkutano huu jumla ya maswali ya msingi 72 na maswali ya nyongeza 174 yaliulizwa na Waheshimiwa Wajumbe na kujibiwa na Waheshimiwa Mawaziri. Pia, Mswada wa Sheria Na. 9 ya 2015 ya Kutoza Kodi na Ushuru na Kurekebisha Sheria Nyengine za Fedha na Sheria za Kodi Zinazohusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo, uliwasilishwa, kujadiliwa na kupitishwa na Baraza lako tukufu.

Vile vile, Baraza lilijadili na kupitisha Sheria Na. 10 ya 2015 ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi Mia Nane na Thalathini, Mia Tatu na Sitini Milioni na Laki Tatu kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2016 na kuruhusu Utoaji na Uhaulishaji wa Fedha Hizo pamoja na Mambo Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, pamoja na jukumu muhimu la Mkutano huu la kuwasilisha, kujadili na kupitisha Bajeti ya Serikali, Mpango wa Maendeleo pamoja na bajeti za wizara zote, Baraza pia lilipata fursa ya kujadili hoja mbali mbali zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wajumbe. Miongoni mwa hoja hizo ni pamoja na hoja ya ukarabati wa nyumba za Mji Mkongwe, mapambano dhidi ya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia, migogoro na unyanyasaji wa wafanyakazi katika makampuni na hoja inayohusiana na malipo ya posho na stahiki za walimu.

Mhe. Spika, serikali inaendelea na juhudi ya kuzipatia ufumbuzi hoja mbali mbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu. Suala la ukarabati wa Mji Mkongwe, serikali tayari imeshafanya tathmini na jumla ya nyumba 26 zimegundulikana kuwa mbovu na zinahitaji ukarabati mkubwa. Kutokana na uwezo wa serikali wa kuzikarabati nyumba hizo kuwa mdogo, imeamua kuziuza baadhi ya nyumba hizo.

Aidha, katika kusimamia suala la udhalilishaji na unyanyasaji wa kijinsia, serikali itaendeleza mashirikiano na wananchi katika kupambana udhalilishaji wa aina zote nchini. Hivyo, serikali inawaomba wananchi waendeleze mashirikiano baina yao na serikali yao katika kuwafichua wale wote wanaofanya vitendo vya udhalilishaji.

Mhe. Spika, katika kulishughulikia tatizo la migogoro na unyanyasaji wa wafanyakazi katika makampuni hasa ya kitalii, serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma inaendelea kuwakumbusha wamiliki wa mahoteli kufuata Kanuni na Sheria za Kazi zilizopo nchini na kuacha kuwanyanyasa wafanyakazi wao. Aidha, serikali inawataka waajiriwa wa makampuni hayo kuwasilisha malalamiko yao wizarani ili wizara ichukuwe hatua zinazofaa. Vile vile, kwa upande wa malipo stahiki na maposho kwa walimu waliosimamia mitihani iliyopita, serikali tayari imeshalipa malipo stahiki na maposho kwa baadhi ya walimu na hatua za kuwakamilishia malipo stahiki na maposho kwa walimu waliobakia zinaendelea.

Mhe. Spika, harakati za Uchaguzi Mkuu wa 2015 tayari zimeanza kwa Vyama vya Siasa kutafuta wagombea wa nafasi mbali mbali za uongozi wa nchi yetu. Ni muhimu kwetu sisi viongozi kuzidi kuwanasihi wafuasi wetu na wananchi kwa ujumla kujiepusha na aina zote za vitendo vitavyoweza kupelekea uvunjifu wa amani na usalama wa nchi yetu. Ni imani yangu kwamba, tunaweza kuchaguana

bila ya kutukanana, kugombana, kuchukiana, kuhasimiana au kufanya vurugu za aina yoyote ile. Hii ni nchi yetu sote na hivyo, usalama na amani ni muhimu kwetu sote.

Mhe. Spika, mafanikio yetu tuliyoyapata kwa muda mrefu na maendeleo yetu yanategemea kudumu kwa hali ya amani na utulivu katika nchi yetu. Nawasihi wananchi wote watumie haki yao ya kidemokrasia kuchagua viongozi makini wenye nia ya dhati na uwezo wa kuwatumikia na kuwaletea maendeleo wananchi. Serikali itahakikisha ulinzi na usalama unaimarika na haitokuwa tayari kumvumilia mtu yeyote au kikundi chochote kitakachovunja sheria na kuhatarisha amani na utulivu wa nchi yetu. Tusifikirie hata siku moja kuwa vikundi vinavyojitayarisha au kutayarishwa kufanya vitendo vya kuhatarisha amani ya nchi kuwa vinaikomoa serikali bali vinajikomoa vyenyewe. Tunawaomba wazazi kuwadhibiti vijana na watoto wao ili wasijiingize au kutumbukizwa katika vitendo vya uvunjifu wa amani.

Mhe. Spika, kabla ya kumalizia hotuba yangu, naomba kwa mara nyengine tena nikushukuru wewe binafsi kwa jinsi ulivyoliendesha Baraza kwa umakini na uadilifu mkubwa. Narudia kuwashukuru pia, Mhe. Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu kwa kutekeleza majukumu yao vyema katika kipindi chote cha miaka mitano (5). Vile vile, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, Makatibu Wakuu wa wizara zote na watendaji wote wa serikali kwa utendaji wao mzuri uliotuletea mafanikio makubwa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa aina ya pekee namshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Mohamed Aboud Mohamed, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, Afisa Mdhamini-Pemba, Wakurugenzi na Watendaji wote wa ofisi yangu kwa namna walivyonipa mashirikiano na kunisaidia katika kutekeleza majukumu yangu. Sasa niishukuru pia Ofisi yangu ya Faragha kwa kunivumilia wakati wote.

Aidha, napenda kuwashukuru wake zangu Bi. Pili Juma Iddi na Bi. Asha Suleiman Iddi na familia zangu kwa ujumla kwa namna walivyonipa moyo, kunivumilia na kunisaidia katika kipindi chote nilichotumikia nchi yetu katika nafasi hii ya Makamu wa Pili wa Rais. Zaidi namshukuru sana Bi. Asha kwa namna alivyonisaidia katika shughuli za Jimbo langu la Kitope wakati nikiwa na shughuli nyingine za Kitaifa, lakini pia namshukuru sana kwa ubunifu wake. Pia, napenda kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Kitope kwa kushirikiana nami katika kipindi chote cha miaka mitano kwa nia ya kuliletea Jimbo letu maendeleo. Nawaomba waniunge mkono tena nitakapokwenda tena kuomba ridhaa yao ya kuwatumikia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, navishukuru vyombo vyote vya habari vilivyoshirikiana nasi katika Baraza hili wakiwemo wataalamu wetu wanaotafsiri kwa lugha ya alama waliowawezesha wenzetu wenye matatizo ya kusikia kufuatilia mijadala na shughuli mbali mbali za Baraza hili. Pia, namshukuru Katibu wa Baraza la Wawakilishi na wafanyakazi wote wa Baraza hili kwa maandalizi mazuri ya mikutano yote. Kwa aina ya pekee napenda kumshukuru sana Mhasibu Mkuu wa Baraza kwa kazi nzuri alizofanya katika kipindi chote cha miaka mitano kuwahudumia vizuri Wajumbe wa Baraza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nawatakia kila la kheri Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, watakaopata nafasi ya kurudi Majimboni kuomba ridhaa ya wananchi kuchaguliwa tena kuingia Baraza lijalo. Nawatakia kheri katika mchakato huo na ni matumaini yangu kwamba wengi wetu tutarudi tena katika Baraza hili kuendelea kuwatumikia wananchi. Lakini pia nawatakia kila la kheri wale Wajumbe ambao hawatopata bahati ya kurudi tena Barazani hapa, nawaombea wafanikiwe katika mambo watakayoamua kuyafanya hapo baadae.

Mhe. Spika, mwisho napenda kuchukuwa nafasi hii kuelezea masikitiko yangu kwa lile jambo lililotokea Barazani hapa tarehe 23 Juni 2015 kwa Mawaziri na Wajumbe wengine wa Baraza lako tukufu kutoka Chama cha CUF kuamua kutoka nje ya Baraza wakati Baraza lilipotaka kupitisha Sheria ya Matumizi kutokana na bajeti zilizowasilishiwa Barazani. Kitendo hiki hakikuwatendea haki wananchi kwani kama Sheria ya Matumizi isingepita, maana yake serikali ingeshindwa kuwatumikia wananchi kuwaletea maendeleo kwa vile isingekuwa na fedha.

Mhe. Spika, napenda kuwapongeza sana kwa dhati Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Wajumbe wengine wa Baraza lako tukufu kutoka Chama cha Mapinduzi kwa kuchukuwa hatua madhubuti kuhakikisha kuwa Sheria ya Matumizi inapita. Kitendo hicho kilikuwa cha kizalendo na kimeonesha upenda kwa wananchi wetu, hongereni sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa vile Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Moh'd Shein leo tarehe 26/06/2015 saa 9:30 jioni atakuja kulihutubia Baraza hili na baadae kutoa tamko la kulivunja. Sasa kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja ya kuliakhirisha Baraza lako tukufu hadi hapa saa 9:30 barabara za jioni. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nichukuwe nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Lakini sitaki leo niwe msemeji peke yangu mimi na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Nichukuwe nafasi ya kumkaribisha Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kutoa neno la shukurani kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia na kutuwezesha kwa asubuhi ya leo kukutana tena hapa. Aidha, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kutoa neno la shukurani.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe nataka nichukuwe fursa hii kumshukuru kwa dhati kabisa Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Moh'd Shein kwa uongozi wake, busara zake na uvumilivu wake na namna ambavyo ameunda serikali yake na alivyoweza kuisimamia kutekeleza majukumu yake kwa mafanikio makubwa sina budi kumpongeza sana.

Aidha, nimshukuru sana sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa namna ambavyo amemsaidia Mhe. Rais, lakini pia kwa namna ambavyo amesimamia shughuli zetu za serikali katika Baraza lako hili tukufu. Kwa kweli ametuongoza vizuri na tumetekeleza yale yote ambayo wananchi walitarajia yatekelezwe.

Lakini kwa heshima ya kipekee Mhe. Spika, naomba sana sana niwashukuru wananchi wote wa Zanzibar kwa namna ambavyo wameipokea serikali yao na namna ambavyo wamekuwa makini kufatilia shughuli hizi za Baraza. (*Makofi*)

Mhe. Spika, katika kipindi hichi cha miaka mitano wananchi wa Zanzibar wameonesha wazi kabisa namna ambavyo wameshirikiana na Baraza hili kwa namna walivyotupa maoni yao na namna walivyofatilia ili kuhakikisha tunatekelezwa wajibu wetu vizuri. Wananchi wetu ni wasikivu, wametuvumilia na tunaomba waendelee kuwa wasikivu, watuvumilie na waendelee kutupa kura zao sisi viongozi tunaotokana na Chama Cha Mapinduzi hasa kwa kuona imani kubwa tulionayo katika kutekeleza majukumu yetu na kuitakia mafanikio makubwa nchi yetu.

Maana Mhe. Spika, kama si kitendo cha Wajumbe wa Baraza lako tukufu wa kutoka CCM kupitisha kwa kauli moja matumizi ya serikali, maana yake kungekuwa hakuna matumizi na kwa msingi huo kungekuwa hakuna shughuli za kimaendeleo zingefanywa kwa wananchi. Kwa hiyo, nataka nichukuwe fursa hii kuwapongeza sana sana Wajumbe hawa wazalendo wenye umakini mkubwa, wenye ujabari na umahiri wa kutumikia nchi yao, hongereni sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa kuwa tumefanyakazi kwa miaka mitano kwa pamoja kwa vyovyote vile kutatokea hitilafu za hapa na pale, lakini kwa niaba ya wenzangu wote Mawaziri tunaomba radhi sana kwa wenzetu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa pale ambapo pametokea hitilafu yoyote ile katika kutekeleza wajibu wetu. Naamini sasa yote tuliyoyafanya tulifanya kwa nia njema ya kutekeleza majukumu yetu ya kutumikia nchi yetu ili tupige hatua kubwa sana.

Sasa tunaondoka hapa kwa moyo mmoja kwa nia moja kwenda kwa wananchi kuyaeleza mafanikio makubwa yaliyotekelezwa kupitia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na kuwaomba wananchi wote wa Zanzibar (Unguja na Pemba) kutokana na mafanikio haya ambayo wameongozwa na jamadari wetu mkuu Dr. Ali Moh'd Shein tumchague tena kwa kishindo kikubwa ili aongoze nchi yetu na tuwachague kila pale penye nafasi ya Uwakilishi wa Mwanachama wa CCM ili CCM iendelee kuongoza nchi yetu.(*Makofi*)

Baada ya hapo Mhe. Spika, napenda kukushukuru wewe, nimshukuru Mhe. Naibu Spika, niwashukuru Wenyeviti wetu wa Baraza na Wajumbe wote wa Baraza hili na Mawaziri wenzangu kwa kufanya kazi kwa pamoja kwa vizuri sana na kutekeleza wajibu wetu, Waheshimiwa, nakushukuruni na nakutakieni kila la kheri. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Hizi zilikuwa ni shukurani za Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, hasa zaidi kwa niaba ya Waheshimiwa Mawaziri. Kwa hiyo, tuchukuwe nafasi vile vile kumkaribisha Mjumbe mwengine kati ya *back benchers* na huyu basi nadhani kwa kujali masuala la ajenda ni mwanamke, nimuombe Mhe. Panya Ali Abdalla, nae atoe shukurani. (*Makofi*)

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kuchukuwa fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana wataala* ambaye ametujaalia uhai wake tukaweza kukutana mahala hapa tukiwa tumo katika harakati za kumalizia umri wetu huu wa Baraza hapa.

Mhe. Spika, sina budi pia kuchukuwa fursa hii kwa kuniteuwa kuwa niwe miongoni mwa watu wa kutoa shukurani katika *back benchers.* (*Makofi*)

Mhe. Spika, nianze shukurani zangu za dhati kabisa, kwanza nimshukuru Rais wetu wa Zanzibar Mhe. Dr. Ali Moh'd Shein kwa uvumilivu wake na ujasiri wake mkubwa ambao ametuonesha katika kipindi chote cha miaka mitano ambapo nchi yetu inaendelea kuwa katika hali ya amani na utulivu ni jambo ambalo tunajivunia sana Wazanzibari, maana bila ya amani na utulivu tusingeweza kuliendeleza Baraza hili mpaka leo linapokaribia kumaliza umri wa Baraza hili.

Mhe. Spika, nichukuwe fursa hii pia kumshukuru sana Makamu wetu wa Pili wa Rais ambaye ameweza kuzisimamia shughuli za Baraza ndani ya Baraza letu hili kwa umakini mkubwa na ameweza kusaidiana na mawizi katika kuzitekeleza kazi za serikali na tumefikia hatua moja kubwa mzuri.

Mhe. Spika, nichukuwe fursa hii kukupongeza kwa dhati kabisa wewe mwenyewe Mhe. Spika, kwa umakini wako na ujasiri wako na busara zako zote ambazo

umetuonesha Wajumbe wa Baraza hili tukufu na ndio maana mambo yote ambayo yamejadiliwa ndani ya Baraza hili, Mhe. Spika, kutokana na busara zako na umakini wako hapakuharibika jambo katika miaka kitano yote. Umeweza kuituliza hali ya Baraza pale ulipoona kuna mawimbi makali na tukaweza kukaa katika mstari mmoja tukaweza kufanikiwa kuliendesha Baraza hili. (*Makofi*)

Lakini pia nichukuwe fursa hii kumshukuru sana Naibu Spika, ambaye ni msaidizi wako, kwa kweli wamefata nyayo zako na wameweza kutumia busara ambazo ulikuwa unawasaidia katika majukumu haya na wameweza na wao kuliendesha Baraza hili bila ya wasi wasi wowote, tunashukuru na tunawapongeza sana.

Mhe. Spika, pia, nichukuwe fursa hii kuwashukuru Wenyeviti wetu Mhe. Mgeni Hassan Juma, akiwa ni mwanamke mahiri kabisa pia Mwenyekiti wetu wa UWAWAZA, wanawake tumeweza kupata mafanikio makubwa kupitia Mwenyekuti wetu huyu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, wakati tunaingia katika Baraza hili sisi wanawake na wengine tulikuwa wageni hatujaona hata njia ya kupita. Lakini kwa ujasiri wa Mwenyekiti wetu huyu tumeweza kupata semina mbali mbali akishirikiana na wewe Mhe. Spika, kwa hiyo, tumeweza na sisi kuweza kusimama na kuzungumza mawili, matatu katika Baraza hili.

Mhe. Spika, tunamshukuru sana. (*Makofi*)

Lakini pia nichukuwe fursa hii kumshukuru Mwenyekiti Mahmoud Mohammed Mussa, kwa kazi kubwa nzuri na yeye ambayo ameifanya katika kulisimamia Baraza hili, pia akiwa ni Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, tumefikia mahala pazuri sana katika busara ambazo wametuonesha.

Mhe. Spika, nichukuwe fursa hii kuwashukuru Wenyeviti wote wa kamati ambao waliweza kushirikiana na kamati zao na wakaweza kuziendesha na hatimae hakukuwa na migogoro yoyote tumeweza kumaliza Baraza hili kwa salama.

Lakini pia Mhe. Spika, nichukuwe fursa hii kuwashukuru waandishi wetu wa bahari ambao kwa kweli wameweza kuwasilisha yale ambayo tulikuwa tukiyatoa hapa Wawakilishi kupeleka kwa wananchi wetu ambayo yakisikilikana *alive.*

Pia, nichukuwe fursa hii kuwashukuru wale wenzetu wa alama la lugha ambao na wao wameweza kutumia fursa nzuri kuwajuilisha wale wenzetu wenye hali ya ulemavu.

Mhe. Spika, pia, nachukuwa fursa hii kwa dhati kabisa kwamba tumeishi ndani ya Baraza hili miaka mitano, yaani siku moja tu kwa mwanaadamu kuishi inakuwa ni mtihani, leo tuneweza kuishi ndani ya miaka mitano ndani ya Baraza hili kupitia Wajumbe wako wote unaotuona hapa bila ya mikwaruzano ambayo ilileta hitalafu watu wakaweza kujuana labda fulani na fulani wamegombana.

Lakini kama imetokea hilo basi kupitia fursa hii naomba nichukuwe fursa hii tuombeane radhi au tusameheane sote kwa yale ambayo yametokezea. Tunachukuwa fursa hii kukuomba wewe Spika wetu kwanza kwa sababu inawezekana na wewe tulikukwaza wakati tukiendelea na mijadala yetu hapa. Lakini kwa uvumilivu wako ulituvumilia na tunaomba radhi sana kama lilitokea hilo utusamehe. Lakini pia Naibu Spika wetu na Wenyeviti wetu kama wao ilitokea tuliwakwaza sisi Wajumbe basi tunaomba radhi sana na tusameheane.

Mhe. Spika, nichukuwe fursa hii kwa sisi wenyewe Wajumbe, aah, kuna kiongozi wetu mkubwa nilimuacha Mhe. Spika, Katibu wa Baraza nae ni kiungo kwetu sisi Wajumbe, tuweza kufanya mambo mengi kupitia Makatibu wetu wa kamati na wao nawashukuru kwa dhati na nawapongeza sana wameweza kutusaidia Wajumbe katika kufanya kazi zetu.

Lakini Mhe. Spika, pia, na wao inawezekana tuliwakwanza sisi Waheshimiwa katika utendaji wetu wa kazi zetu na wao tunawaomba radhi sana watusamehe tulikuwa hatuna lengo la kuwakwaza, lakini tulikuwa tuna lengo la kufikia mafanikio katika nchi yetu.

Mhe. Spika, nichukuwe fursa hii binafsi yangu mimi mwenyewe kulimboa radhi Baraza hili kuanzia Mawaziri, wewe mwenyewe Spika, Makamu wetu wa Pili, Manaibu Mawaziri, Wenyeviti wetu wote na watendaji wetu wote wa Baraza ikiwa nimetokea kumkwaza Mjumbe yeyote, basi naomba radhi anisamehe. Lakini nahisi mambo yamekwenda vizuri *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atujaalie kheri kwa yale yote ambayo tumekusudia kuyafanya katika nchi yetu, Mwenyezi Mungu atuongoze katika kheri hiyo na hasa kupitia Mwezi huu Mtukufu. Huu ni mwezi wa baraka ni mwezi wa maoni, *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atukubalie yale yote ambayo tunamuomba yenye kheri na sisi katika mwezi huu mtukufu.

Inshaallah Mwenyezi Mungu atulipe malipo ambayo tumeyatenda katika mwezi wetu huu mtukufu wa Ramadhani. Lakini *Inshaallah* Mwenyezzi Mungu aijaalie Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hasa kupitia Chama Cha Mapinduzi CCM kiweze kushinda kwa ushindi mkubwa, *Inshaallah* Mwenyezi Mungu Rais wetu amrejeshe madarakani na Wajumbe wote wa CCM waliomo ndani ya Baraza hili *Inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu warudi tena waje waendeleze yale mafanikio ambayo tuliyaachia. (*Makofi*)

Mhe. Spika, tulikuwa na lengo zuri kabisa na kila mmoja ameliona kwamba tuna lengo zuri la kufikia ufanisi mkubwa katika nchi yetu *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atujaalie na mafuta na gesi yapatikane katika nchi yetu ili nchi yetu iweze kukua kiuchumi.

Mhe. Spika, nakushukuru sana na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atujaalie kila la kheri. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Panya Ali Abdalla, pale amesema kwamba anaomba radhi kwa niaba yenu kama mmenikwaza, kama imetokezea kunikwaza lakini nataka niwahakikishie kwamba sikukwazika. Kwa hiyo, mambo yote safi.(*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijawahoji kuhusu hoja ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kuna ombi moja na taarifa tatu na ombi hili limekuja kutokana na hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, ndani ya hotuba yake mna suala zima la misiba iliyotokezea ya baadhi ya Wajumbe wetu, lakini pia msiba wa mzee wetu ambaye alinikabidhi jukumu hili mzee Spika, mstaafu marehemu Ali Khamis Abdalla. Lakini pia imetaja hotuba hii masuala ya maafa mbali mbali. Sasa kama kawaida yake Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa, akanishauri ingefaa kwa kuwa tunamaliza shughuli hii basi tusimame kwa dakika moja kuwakumbuka wote hao pamoja na maafa haya. Niwaombe basi tusimame kwa dakila moja kuwakumbuka wote.

(*Hapa Wajumbe wote walisimama kwa dakika moja kuwakumbuka Wajumbe wenzao waliofariki*)

Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni sana. Nimesema kuwa kuna taarifa tatu; Taarifa ya kwanza nimeletewa taarifa na Katibu wetu wa Baraza la Wawakilishi kwamba ndugu yetu ambaye tumefanya kazi nae kwa karibu sana, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anakusudia kutembelea majimbo yote 50. Kazi atayoifanya huko ni kwenda kufanya ukaguzi kuhusu fedha ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Kwa hiyo, mkipata taarifa huko kwamba ukaguzi umefanyika huko majimboni msije mkakimbia, ila mtayarishe kama mna timu ya pamoja mlikuwa mnakaa muitayarishe, kama kuna hoja zozote anazozihitaji basi mzitoe. Najua mtakuwa na kazi kubwa, lakini na hii ni kazi vile vile. Kwa hivyo, hiyo ni taarifa ya kwanza. (*Makofi*).

Ziara hiyo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali itafanyika katika kipindi cha mwezi huu wa June na Julai kabla hatujaingia kwenye ile taarifa kubwa ya mchakato. Kwa hiyo, nakupeni taarifa hiyo mjitayarishe ili kuweza kuweka mahesabu sawa juu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

Tangazo la pili tena pia na kwenye hotuba hii imejitokeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, alimsifu sana Muhasibu kwa kuwahudumia vizuri sana kwa muda wa miaka mitano. Sasa Katibu alinileta taarifa ili sifa hizo ziwe ziko vizuri, ananambia nikupeni taarifa kwamba madeni yote ambayo hajawalipa Waheshimiwa Wajumbe pamoja na wale wa Kamati basi madeni yote haya yatalipwa leo hii. Nadhani hii ni taarifa nzuri kwamba kila mnachodai mtalipwa, mbona hamna makofi mengi, na kwa hiyo, kama kuna Mjumbe anadai, narudia anadai basi atoe taarifa kwa Ofisi ya Katibu ili madeni hayo yalipwe leo. Kwa hiyo, hiyo ni taarifa ya pili muhimu sana. (*Makofi*)

Taarifa ya tatu ambayo pia imejitokeza kwenye *paragraph* ya mwisho ya hotuba ya Rais kuhusiana na mambo fulani fulani, lakini hasa hii ni taarifa ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad.

Waheshimiwa Wajumbe, jana mlifanya kazi ya kuridhia wageni wetu maalum kuwepo hapa juu, lakini ikawa hamkuridhia ujio wa Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad. Mimi kama *conduit pipe* ya kupeleka taarifa baada ya kazi ile mliofanya nilimuandikia barua kwamba bwana wee, Mheshimiwa, Wajumbe hawakuridhia, kwa hiyo, usije. Kwa hiyo, na yeye ameniandikia barua na nitaisoma.

Barua hii imeandikwa na msaidizi wake, kwa hiyo, nitaisoma kama ilivyo, lakini maagizo yametoka kwake yeye.

Barua imepelekwa kwa Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zanzibar mwaliko wa kuhudhuria ghafla ya uvunjwaji wa Baraza la Nane la Wawakilishi la Zanzibar.

"Kwa heshima naomba uhusike na mada ya barua hii kama inavyosomeka hapo juu, pia, naomba urejee barua yako ya tarehe 25 June 2015, yenye kumbukumbu BLWD10/21/147 inahusika.

Katibu wake anasema; nimeagizwa na Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais kwamba nikushukuru kwa barua yako, pia, anakuhakikishia kuwa ataheshimu maamuzi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na kwa hiyo, hatohudhuria katika shughuli hiyo, yaani hiyo shughuli ya leo wakati wa Alaasiri.

Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, anakutakieni shughuli njema na mafanikio.

Ahsanteni sana".

Hiyo ndio barua inavyosema, haya inatosha. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kwa kuwa nilimuandikia barua na yeye amejibu na taarifa hiyo nimeona niilete kwenu kwa sababu tumeamua humu ndani na ni taarifa muhimu sana.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo nakushukuruni tena kwa mashirikiano makubwa na sasa naomba niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kuahirisha kikao hiki hadi saa 9:30 Alaasiri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe, nasisitiza shughuli rasmi ya Mhe. Rais itafanyika saa 9:30, lakini sisi Wajumbe tunatakiwa tufike saa 8:30. Baada ya hayo sasa naahirisha kikao hiki hadi saa 9:30 jioni leo.

(Saa 4:27 asubuhi Baraza liliahirishwa hadi saa 9:30 Alaasiri)

(Saa 9.30 mchana Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein, mgeni wetu maalum Mhe. Jaji Mkuu Mhe. Omar Othman Makungu, Waheshimiwa Wajumbe, pamoja na wageni wengine waalikwa leo kama tulivyoarifiana kabla ni siku kubwa baada ya Baraza la Wawakilishi kufanya kazi kwa miaka mitano, ikifika kumalizika kwa uhai wa miaka mitano ya Baraza, kwa hivyo, ni utaratibu kwamba tuandae ghafla kama hii na tumuombe Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ili aje kutoa hotuba katika chombo hichi na hatimaye atoe tamko. Tamko lenyewe bila shaka kwa sababu uhai wa miaka mitano umekwisha ni kulivunja, tusitegemee kama atasema ninaongeza muda, hapana. (*Makofi*)

Sasa Mhe. Rais, kabla ya kuingia kwenye shughuli hiyo muhimu katika Kikao chetu cha leo hivi jioni tumewaalika wageni mbali mbali ambao ninaomba nichukue nafasi hii ili niwatambulishe baadhi yao na wengine kwa makundi ili hatimaye tuje tukuombe kulihotubia Baraza na utoe tamko muafaka kwa shughuli ya leo.

Mhe. Rais, katika shughuli ya leo tumemualika Mhe. Mke wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Mwanamema Shein, mama karibu sana, pia, tumemualika mke wa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Asha Balozi naye yupo pale ameshasimama, Mama Asha Balozi tumekuwa nae tangu asubuhi. (*Makofi*)

Vile vile, tumemualika Mhe. Balozi Karume. Wageni wengine waalikwa katika shughuli hii ni Mhe. Balozi Mdogo wa India, *could you rise up to salute the members, Hon. Consul General of India, not at present, Hon. Consul General of China, Hon. Consul of United Kingdom*, yule pale karibu sana, *Hon. Consul of Italy* hakufika, *Hon. Consul of Germany*, karibu sana, Mkurugenzi wa Idara ya Mambo Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mwakilishi Mkaazi wa *UNDP* Zanzibar, Mwakilishi Mkaazi wa Shirika *UNFPA* (*The Representative of UNFPA)* yule pale, Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la *UNICEF (The Representative of UNICEF),* Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la *WHO* yule pale, Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la *ILO not at present*.

Wageni wengine waalikwa ni Mhe. Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Makatibu Wakuu wa Wizara mbali mbali na Manaibu wao wasimame kwa makundi, wale pale. (*Makofi*)

Katika shughuli hii Mhe. Rais pia tumewaalika Wakuu wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama, kwa pamoja ninaomba wasimame. Pia, katika shughuli hii tumewaalika Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya, naomba musimame kwa pamoja, wapo pia baadhi ya Wakurugenzi na viongozi wengineo lakini hasa hasa Mhe. Ndugu yetu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali, Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar. (*Makofi*)

Sasa hayo makofi basi bakisheni kidogo kwa sababu kuna na bosi wake Mhe. Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar. Mhe. Rais makofi hayo yanaashiria kwamba mara baada ya shughuli hii mchakato unaoendelea ni watu hao. (*Makofi*)

Lakini pia tunaye Ndugu yetu Mkurugenzi wa Mashitaka (*DPP*), huyu pamoja na kwamba Mhe. Rais umempa madaraka ya kuwa Mkurugenzi wa Mashitaka, lakini tunafanya kazi naye kwa karibu sana. Pia, tunaye Ndugu yetu Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi, naona amechelewa kidogo, viongozi wa vyama vya siasa kwa pamoja waliohudhuria tunaomba wasimame, tumewaalika pia vile vile viongozi wa Dini akiwemo Mufti Mkuu wa Zanzibar, hakufika bado, Mhe. Kadhi Mkuu wa Zanzibar, lakini pamoja na viongozi wa Dini akiwemo Askofu wa Kanisa la *Anglican* Dayosisi ya Zanzibar kama yupo asimame na Askofu wa Kanisa la Katoliki Jimbo la Zanzibar, tunamuomba asimame kama yupo. (*Makofi*)

Mhe. Rais, tunao viongozi wa Vyuo Vikuu *(Vice Chancellor)* kutoka *Zanzibar University* kama yupo namuomba asimame, *Vice Chancellor* wa *Zanzibar State University* kama yupo asimame. Lakini vile vile tunaye *Vice Chancellor* wa *Al Sumait University* Chukwani, eeh! yupo hapa. (*Makofi*)

Tumewaalika pia kwa sababu tumefanya kazi nao kwa muda mrefu na kwa karibu Wakuu wa Vyombo vya Habari, wakiwemo Mkurugenzi Mkuu wa *ZBC*, hawa kwa pamoja ningeomba wasimame wote wale wa vyombo vya habari. (*Makofi*)

Mhe. Rais, hao ni baadhi tu ya wageni, lakini ninaambiwa hapa pia umefuatana na washauri wako, wote nawaomba wasimame kwa pamoja. (*Makofi*)

Mhe. Rais, kama kuna wageni wengine wowote ambao kwa bahati mbaya sikuwataja waelewe kwamba shughuli ya leo hasa ni ya Mhe. Rais, lakini ninakubali kwamba kuwepo kwao tunakutambua kwa dhati na wote Waheshimiwa Wageni waalikwa karibuni sana.

Mhe. Rais, Baraza la Wawakilishi la Zanzibar limeanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 63 cha Katiba ya Zanzibar na Baraza hili lina sehemu mbili ambapo kwa mujibu wa Kifungu hicho; Sehemu ya Kwanza ni Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Sehemu ya Pili ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao ndiyo hawa wamekupigia makofi mengi sana.

Mhe. Rais, chombo hichi ni cha Uwakilishi wa wananchi kimekuwa kikitekeleza majukumu yake kwa ushirikiano mkubwa ya Kikatiba na ya Kiutawala baina ya pande zake hizo mbili. Hiyo ni pamoja na Miswada ya Sheria inayopitishwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na kwamba Miswada hiyo haiwezi kuwa ni Sheria mpaka pale ambapo wewe Mhe. Rais, utakuwa umeitia saini kwa mujibu wa Kifungu cha 78 cha Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Rais, maisha ya chombo hichi cha wananchi kwa mujibu wa Kifungu cha 62 cha Katiba ya Zanzibar ni kipindi cha miaka mitano, tangu Mkutano wa Kwanza toka kuundwa kwake. Mhe. Rais, safari ya maisha ya Baraza ilianza tokea Novemba, 2010 na kipindi hicho cha miaka mitano kinakaribia kumalizika.

Kutokana na maisha hayo ya Baraza kukaribia kumalizika, Katiba yetu inataka Baraza hili livunjwe rasmi kama inavyofafanuliwa chini ya Kifungu cha 61 (2)(a) kuwa Mhe. Rais, anaweza kulivunja Baraza kama limemaliza uhai wa miaka mitano uliotajwa kwa mujibu wa Kifungu cha 62 cha Katiba.

Mhe. Rais, katika ushirikiano ule uliotajwa Kikatiba hapo juu baina ya pande mbili za Baraza ambao ni Rais wa Zanzibar kwa upande mmoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa upande mwengine, Katiba chini ya Kifungu cha 61 limeweka jukumu hili la kulivunja Baraza mikononi Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa hivyo, Mhe. Rais, ndiyo tukakuomba uje utimize mahitaji hayo ya Kikatiba kwa kuwahotubia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la

Wawakilishi na hatimaye ulivunje rasmi Baraza la Nane la Wawakilishi lililoanza kazi yake hapo Novemba, 2010.

Mhe. Rais, tunakushukuru sana kwa kukubali ombi hilo na hivi sasa Wajumbe wapo tayari kusikiliza hotuba yako na tamko lako la kulivunja Baraza hili rasmi la Nane la Wawakilishi wa Zanzibar.

Hivyo basi kutokana na mahitaji hayo ya Katiba, Waheshimiwa Wajumbe, sasa wana hamu sana kusikiliza hotuba yako. Nikuombe Mhe. Rais, sasa uchukue nafasi yako kulihotubia Baraza hili na hatimaye utoe tamko la kulivunja.

Mhe. Rais karibu. (*Makofi*)

HOTUBA YA RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI MHESHIMIWA DK. ALI MOHAMED SHEIN, WAKATI WA KULIVUNJA BARAZA LA NANE LA WAWAKILISHI, TAREHE 26 JUNI, 2015

Mhe. Pandu Ameir Kificho,
Spika wa Baraza la Wawakilishi,

Mhe. Balozi Seif Ali Iddi,
Makamu wa Pili wa Rais,

Mhe. Omar Othman Makungu,
Jaji Mkuu wa Zanzibar,

Waheshimiwa Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi,

Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi,

Waheshimiwa Mabalozi wadogo mlioko Zanzibar,

Wawakilishi wa Mashirika mbali mbali ya Kimataifa,

Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Ndugu Wageni Waalikwa,

Mabibi na Mabwana,
Assalam Aleikum

UTANGULIZI:

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, awali ya yote, naanza hotuba yangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu; Mwingi wa Rehema na Utukufu kwa kutujaalia afya njema na uhai tukaweza kukutana katika hadhara hii muhimu. Namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie kila la kheri katika utekelezaji wa wajibu wetu huu wa Kikatiba.

Kadhalika, nawapa pole wale wote walioathirika na maafa ya kipindi cha mvua kubwa za hivi karibuni zilizopelekea watu watatu kupoteza maisha na wengine kupoteza mali na uharibifu mkubwa wa nyumba na mazingira. Aidha, tunawashukuru wale wote waliounganа na Serikali katika kutoa misaada mbali mbali ya kuwafariji ndugu zetu waliofikwa na maafa hayo. Tunawaomba ndugu zetu hao walioathirika waendelee kuwa na nyoyo za subira na Mwenyezi Mungu awape uwezo wa kukabiliana na mitihani iliyowasibu.

Mhe. Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwako na Baraza lako tukufu kwa kunipa nafasi hii ya kuja kulihutubia Baraza hili la Nane kabla ya kulivunja. Kwa hivyo, kikao hiki cha leo kimeitishwa kwa ajili ya kutekeleza matakwa ya Kikatiba kwa mujibu wa mamlaka niliyopewa katika Kifungu cha 91(2)(a) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Kadhalika, kikao chetu hiki ni utekelezaji wa Kifungu cha 92(1) cha Katiba ya Zanzibar kuhusiana na uhai wa Baraza la Wawakilishi kuwa ni kipindi cha miaka mitano tangu ulipoitishwa Mkutano wa Kwanza na leo tarehe 26 Juni, 2015 ndiyo nalihutubia Baraza la Nane kwa mara ya mwisho kabla ya kulivunja ili kupisha Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Napenda nitumie fursa hii ili nitoe shukrani zangu za dhati kwako Mhe. Spika, kwa uongozi wako bora na kwa kazi kubwa uliyoifanya katika kipindi cha miaka mitano ya Baraza hili, kwa kusimamia na kwa kuziendesha kazi za Baraza kwa mafanikio makubwa. Nasema hongera sana.(*Makofi*)

Shukrani zangu za dhati ziwaendee Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili, kwa kuzitekeleza kazi zao kwa moyo wa kujituma, kwa kushirikiana na kwa uvumilivu mkubwa. Ni imani yangu kwamba wananchi wameridhika na namna mnavyowawakilisha mawazo na maelekezo yao katika Baraza hili. Licha ya kuwa na wajumbe wapya wengi katika Baraza hili, na upya wa mfumo wa kisiasa tulionao na muundo mpya wa Serikali, mmeweza kuifanya kazi yenu kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nachukua fursa hii, mimi mwenyewe na kwa niaba ya serikali, kutoa mkono wa pole na rambi rambi kwako, Wajumbe wa Baraza lako tukufu, ndugu, jamaa na wananchi wa Jimbo la Magomeni na Watanzania wote, kwa kifo cha

kiongozi mwenzetu Marehemu Salmin Awadh Salmin; aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni na Mnadhimu wa Chama Cha Mapinduzi hapa Barazani. Hekima, busara na mchango wake katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar na kuliendeleza Taifa letu, hautasahaulika na utaendelea kuthaminiwa. Namuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi - *Amin*.

Mhe. Spika, katika hotuba yangu ya uzinduzi wa Baraza hili la Nane tarehe 11 Novemba, 2010, nilieleza mwelekeo wa mipango ya serikali nitakayoiunda, baada ya wananchi wa Zanzibar kunichagua kwa kura nyingi, kupitia Chama changu cha Mapinduzi, kuwa Rais wa Zanzibar katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 31 Oktoba, 2010. *(Makofi)*

Kadhalika, katika hotuba yangu ile, nilisema kuwa nitaanza Awamu ya Saba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tukiwa na dhima ya msingi ya kuwatumikia wananchi waliotuchagua kwa kipindi cha miaka mitano. Matumaini ya wananchi kwa serikali yao yalikuwa ni kuyaendeleza mafanikio yote yaliyoletwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa awamu zote zilizotangulia na kutekeleza sera na mipango itakayowezesha kukuza uchumi na kuimarisha ustawi wa jamii.

Ili kuyafikia malengo hayo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba inaongozwa kwa kuzingatia mipango mikuu ya kitaifa ambayo ni Dira ya Maendeleo ya 2020, Malengo ya Milenia, MKUZA na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 hadi 2015. Sambamba na hayo, utekelezaji wa ahadi nilizozitoa katika kampeni ya uchaguzi ya mwaka 2010, ilikuwa ni miongoni mwa vipaumbele muhimu katika utendaji wa serikali niliyoiunda.

Mhe. Spika, leo nitaelezea kwa muhtasari mafanikio ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba, katika nyanja zote za maendeleo, kisiasa, kiuchumi na ustawi wa jamii. Ni dhahiri kuwa mafanikio hayo yanatokana na mchango wenu katika kutekeleza wajibu, kufuatana na Mipango mikuu ya kitaifa niliyoeleza hapo mwanzo na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010–2015. Ilani hiyo ni mkataba baina ya wananchi na Serikali yetu. Ni jambo la kufurahisha kwamba hadi leo hii, Ilani hiyo imeshatekelezwa kwa kiwango kinachokadiriwa kufikia asilimia 90. Natoa pongezi kwa wale wote walioshiriki katika utekelezaji wa Ilani hii.*(Makofi)*

Mhe. Spika, siri kubwa ya mafanikio yetu ni kuwa sisi tuliingia katika Muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, tukiwa tayari tunayo Katiba iliyoandaliwa kwa ajili ya Muundo huo mpya. Lakini zaidi ya hayo, tulidhamiria kwa dhati kuitekeleza azma na shabaha ya muundo huo. Tulijenga heshima na mapenzi baina yetu. Tulijenga misingi ya kuvumiliana. Kwa kufanikisha uendeshaji wa serikali,

nilipanga Wizara na kuteua Mawaziri kwa uwiano wa matakwa ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MIPANGO YA SERIKALI:

HALI YA UCHUMI:

Mhe. Spika, Katika kipindi hiki kuanzia mwaka 2010 – 2014, Pato la Taifa kwa bei za miaka hio limekua kutoka TZS bilioni 1,050.8 hadi kufikia TZS bilioni 2,133.5. Kwa bei za kudumu, Pato la Taifa limekua kutoka TZS bilioni 848.2 hadi kufikia TZS bilioni 1,115.4 sawa na ukuaji wa asilimia 31.5 kwa kipindi hicho. Uchumi wetu umekua kutoka asilimia 4.3 mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 7.0 mwaka 2014 sawa na ongezeko la asilimia 2.7. Pato la Taifa kwa mwananchi mmoja, kwa bei za miaka 2010 – 2014, limekua kutoka TZS 856,000 ($613) mwaka 2010 hadi kufikia TZS 1,552,000 ($939) kwa mwaka 2014.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 hadi 2014/2015, mapato ya ndani yameongezeka kutoka TZS bilioni 181.4 hadi kufikia TZS bilioni 360.4, sawa na ukuaji wa asilimia 98.7 kwa kipindi hicho au sawa na wastani wa asilimia 19.7 kwa kila mwaka.

Mhe. Spika, kwa upande wa mfumko wa bei, tunaendelea kuwa na mfumko wa bei ulio katika tarakimu moja. Katika mwaka 2010, mfumko wa bei ulikuwa wa wastani wa asilimia 6.1 na umeshuka hadi kufikia wastani wa asilimia 5.6 kwa mwaka 2014.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016, ambao mjadala wa bajeti hii umemalizika juzi, Bajeti yetu itaendelea kuzingatia malengo makuu ya Serikali. Malengo hayo ni kujenga jamii:

(i) Iliyoelimika kwa elimu bora na inayotoa wataalamu wenye hadhi ya kimataifa;
(ii) Yenye siha,
(iii) Iliyoimarika kiuchumi; na
(iv) Inayojali Umoja wa Kitaifa na kufuata misingi ya Utawala Bora.

Mambo haya ndio yanayojenga falsafa iliyomo katika Dira ya Maendeleo ya 2020 ambayo inatekelezwa kwa sasa kupitia MKUZA II na Mpango wake Mkuu wa utekelezaji. Utendaji wa sekta zote umejielekeza katika kufikiwa kwa malengo hayo makuu.

Mhe. Spika, katika kuinua uchumi wetu, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha Idara ya Mipango, Sera na Utafiti katika kila wizara kwa lengo la kutilia mkazo umuhimu wa utafiti katika maendeleo yetu. Serikali kwa kushirikiana na Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (*COSTECH*), imeendeleza tafiti katika taasisi mbali mbali ikiwemo Kilimo, Elimu, Uvuvi, Afya na Nyanja nyenginezo. Serikali imeandaa mpango wa mkakati wa utafiti kwa kila wizara, ambayo sasa umeanza kutekelezwa.

MATOKEO KWA USTAWI: (*RESULTS FOR PROSPERITY - R4P*)

Mhe. Spika, katika kutafuta mbinu bora za kutekeleza mipango yetu, Serikali imeanzisha utaratibu wa kuwakutanisha wataalamu wa sekta mbali mbali, kwa mfumo uliopewa jina la Mpango wa Maabara kwa ajili ya kujadili, kupanga na kupitisha maazimio ya utelekezaji wa mipango mbali mbali ya maendeleo. Utaratibu huu hapa petu tumeufuata na tumeupa jina la Matokeo kwa Ustawi (*Results for Prosperity - R4P*) ambao umeonesha kuwa na mafanikio makubwa kwa nchi zilizouanzisha na kuufuata.

Mhe. Spika, hivi karibuni Serikali imeanza kutekeleza programu mbali mbali zinazotayarishwa katika Mpango wa Matokeo kwa Ustawi. Programu zilizoanza kutekelezwa ni pamoja na Programu Mjumuisho ya Kuendeleza Utalii, Programu ya Kuimarisha Mazingira ya Biashara na Mkakati wa Utafutaji Rasilimali Fedha. Kwa sasa mchakato unaendelea wa matayarisho kwa ajili ya sekta afya na elimu ambazo tunatarajia zitaanza katika mwaka huu.

MIRADI YA MASHIRIKIANO BAINA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI:

Mhe. Spika, katika kipindi cha miaka mitano, tumefanya jitihada kubwa za kuimarisha na kuishirikisha Sekta binafsi katika mipango yetu ya maendeleo. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tayari imeanzisha kitengo cha "*PPP*", yaani ubia kati ya huduma za umma na sekta binafsi katika Tume ya Mipango kwa ajili ya kushughulikia miradi itakayoanzishwa kwa mfumo huo. Serikali imejiandaa kuanzisha Idara kamili ya "*PPP*" yaani *Public Private Partnership*, ambayo itahusika na utekelezaji na usimamizi wa shughuli zote za miradi ya mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

UWEKEZAJI VITEGA UCHUMI:

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba, kupitia Mamlaka ya Vitega Uchumi (*ZIPA*) ilifanya kazi nzuri katika kuwavutia wawekezaji wa nje na ndani kuja kuwekeza katika sekta mbali mbali za kiuchumi na kijamii. Kwa

Kipindi cha miaka mitano (2010–2015), tumeweza kusajili miradi 187 yenye thamani ya TZS bilioni 38,560.50, sawa na *USD* 1,881,00 milioni ambayo inakadiriwa kuwapatia ajira watu 9,192. Wawekezaji kutoka Uturuki, China, Italia, Ujerumani na India wameonesha dhamira ya dhati ya kutuunga mkono na nimetumia fursa niliyoipata kuwakaribisha Wawekezaji hawa kuja kuwekeza, wakati nilipotembelea nchi zao, vile vile, wawekezaji wa ndani nao wamehamasika katika uwekezaji kwenye nyanja mbali mbali.

Mhe. Spika, serikali kupitia Mamlaka ya Uwekezaji na Vitega Uchumi Zanzibar (*ZIPA*), kuanzia mwaka wa fedha 2014/2015, imeweka mkazo mkubwa katika kukamilisha dhamira ya kuendeleza maeneo huru ya uchumi. Ni dhahiri kwamba mpango huu tangu ulipobuniwa na hatimae kutolewa Tangazo la Sheria Na. 5 la mwaka 1993 bado hazijachukuliwa juhudi za kutosha za kutekeleza kwa vitendo uendelezaji wa maeneo hayo.

Mhe. Spika, kwa hakika hivi sasa tumejidhatiti kuitekeleza dhana nzima ya maeneo huru ya uchumi kwa vitendo. Mipango yetu ni kuibadilisha taswira ya eneo la Fumba. Tumepanga kuutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Mji wa Kisasa wa Fumba (*Fumba Bay Satellite City Project*). Mji huu mpya wa kisasa na wa kibiashara utakuwa na mtaa mkubwa wa biashara (*High Street*), nyumba za kisasa za kibiashara za kuishi wageni na wenyeji na uwanja wa kuchezea mchezo wa gofu. Vile vile, kutakuwa na hoteli moja kubwa ya nyota tano yenye vyumba 400 na tutajenga eneo la shughuli za biashara ambalo litakuwa na maghala ya kisasa na mfumo wa usafirishaji wa bidhaa wa kisasa. *(Makofi)*

Aidha, katika mji huu kutakuwa na uwanja wa mpira wa kisasa ambao utakuwa na uwezo wa kuchukua kiasi cha watu 45,000. Pamoja na huduma za kijamii za ulinzi, afya na elimu, mradi huo unakusudia kuanzisha bandari ndogo, kwa ajili ya huduma za usafiri wa majini kati ya Zanzibar - Pemba na Zanzibar - Dar es Salaam. Jumla ya hekta 700 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Serikali imeanza mazungumzo na Muwekezaji wa Kampuni mama ya *Bakhresa Group* juu ya kushirikiana katika uwekezaji wa mradi huu kwa mfumo wa ubia (*Joint venture company*).

Mhe. Spika, vile vile, katika eneo hili tutatekeleza Mradi wa Mtaa wa Viwanda. Jumla ya hekta 100 zimetengwa katika maeneo ya Dimani, Kisauni pamoja na Ndambani, kwa ajili ya uendelezaji wa shughuli za viwanda vidogo na vya kati. Mazungumzo yanaendelea kati ya Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar (*ZIPA*) na Kampuni ya *CPC* ya Misri juu ya mfumo na utaratibu na ushirikiano wa uwekezaji wa Miundombinu katika eneo hilo.

Kadhalika, Hekta 60 zimetengwa kwenye kituo cha kimataifa cha mikutano na kukabidhiwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, kwa ajili ya kuandaa maelezo maalum ya mradi wa uwekezaji. Maelezo hayo yakiwa tayari, Mamlaka itashirikiana na Wizara hiyo kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji utakaopangwa.

Mhe. Spika, vile vile, serikali imebuni mpango wa kutekeleza Mradi wa Uendelezaji wa Mji wa Nyamanzi – Fumba. Mradi huu umetengewa kiasi cha hekta 63 ambazo zitatumika kwa ajili ya nyumba za makaazi na biashara mbali mbali ikiwemo maeneo ya makaazi ya kijamii, majengo ya kuishi, huduma za hoteli na kumbi za mikutano, huduma za masoko na mawasiliano, maofisi na maduka pamoja na maegesho ya magari, vituo vya *ferry*, maeneo ya burudani, ya afya na michezo. Maeneo ya asili ya vijiji vya maeneo haya vikiwemo Fumba, Bweleo, Dimani na vijiji vyengine vidogo vidogo, yataheshimiwa na kuendelezwa kwa mashauriano na wanavijiji wenyewe. Hatua ya awali ya kuwaeleza wananchi wa Fumba na maeneo niliyoyataja tayari zimeanza kuchukuliwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika Mkoa wa Kaskazini Unguja, tumeshaanza Mradi wa Maendeleo ya Mji wa Kisasa Kijini – Matemwe. Mradi huu unaendelea kutekelezwa na Kampuni ya "*Penny Royal*" katika maeneo ya Matemwe Muyuni, ambapo utagharimu jumla ya Dola za Kimarekani milioni 220. Mradi huo unajumuisha ujenzi wa Hoteli ya kimataifa yenye hadhi ya nyota tano.

Aidha, mradi huo utahusisha ujenzi wa kiwanja cha kimataifa cha gofu, chenye jumla ya vishimo 18 na ujenzi wa nyumba za makaazi kwa watu wenye kipato cha juu ambazo zitatumia nishati ya nguvu ya upepo. Hivi sasa Kampuni hiyo inaisaidia Serikali katika ujenzi wa barabara yenye urefu wa *km* 20.2 kutoka Matemwe kupitia Kijini kuelekea maeneo ya mradi hadi Kidoti. Ujenzi wa barabara hio unaendelea vizuri, nimekwenda kutembelea na kukagua mimi mwenyewe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika eneo la Mjini Unguja, katika kipindi hiki, Serikali imepanga kutekeleza Mradi wa Kuendeleza Hoteli ya Bwawani na eneo linaloambatana nalo. Serikali italiendeleza eneo hilo kupitia Muwekezaji wa Kampuni ya "*Quality Group*" alieshinda zabuni. Kampuni hii inakusudia kuendeleza eneo la Bwawani kwa kujenga Hoteli ya Kisasa ya nyota tano, majengo ya kisasa ya makaazi, majengo ya biashara, mikahawa, soko la Kizanzibari na maegesho ya magari. Jengo la sasa la hoteli ya Bwawani, halitabinafsishwa, halitavunjwa, litakarabatiwa kwa ajili ya kupokea wageni mashuhuri. Uendelezaji wa eneo la Bwawani utazingatia ipasavyo athari za Kimazingira na urithi wa kale. *(Makofi)*

SEKTA YA BIASHARA NA VIWANDA:

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba, yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa, inaendelea kuimarisha mazingira ya biashara kwa kushirikiana na sekta binafsi. Usafirishaji wa bidhaa unaendelea kuimarika mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2014 tumeweza kuuza nje bidhaa zenye thamani ya TZS milioni 133,591.7 kutoka bidhaa zenye thamani ya TZS milioni 87,799.6 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 52.14. Usafirishaji huo umeongezeka kwa kiasi kikubwa kutokana na jitihada zetu za kuimarisha uzalishaji wa zao la karafuu na mwani, ambayo usafirishaji wake ulifikia TZS milioni 103,079.2 kutoka TZS milioni 75,392.6 mwaka 2013. Hili ni ongezeko la asilimia 77.8 ya usafirishaji wote kwa mwaka 2014. Licha ya kuwepo kwa urari kwa bidhaa kwa usafirishaji nje, takwimu hizi zinatupa matumaini mazuri juu ya mwenendo na ukuaji wa biashara nchini.

Kuhusu biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara, jumla ya bidhaa zenye thamani ya TZS milioni 23,268.7 ziliingizwa Zanzibar kutoka Tanzania Bara mwaka 2010 ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya TZS milioni 64,296.4 mwaka 2014. Vile vile, bidhaa zenye thamani ya TZS milioni 2,203.8 zilisafirishwa kwenda Tanzania Bara mwaka 2010 ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya TZS 366,354.2 mwaka 2014.

Kwa jumla, katika kipindi hiki cha kwanza cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba, urari wa biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara unaendelea kuwa mzuri kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Spika, ni dhahiri kuwa juhudi zilizochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba, za kufufua zao la Karafuu zimezaa matunda mazuri. Mpango wa miaka kumi wa kufufua zao hili, tumekuwa tukiutekeleza kwa mafanikio makubwa.

Katika kipindi cha miaka mitatu ya kwanza ya mpango huo; 2011/12 - 2013/2014, jumla ya tani 11,477 za karafuu zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 130.82 zilisafirishwa na kuuzwa nje ya nchi. Kiwango hicho ni sawa na ongezeko la tani 2,792 ambalo ni sawa na asilimia 32.1 ikilinganishwa na mwaka 2008/09 - 2010/2011. Hadi kufikia tarehe 12 Juni, 2015 jumla ya tani 2, 822 zenye thamani ya TZS bilioni 39.48 zilinunuliwa kutoka kwa wakulima.

Mhe. Spika, Serikali imetimiza ahadi niliyoitoa mwaka 2011 ya kuwalipa wakulima wa zao la Karafuu asilimia 80 ya bei ya karafuu ya Soko la Dunia. Karafuu za Daraja la Kwanza zinanunuliwa kwa bei ya TZS 14,000 kwa kilo badala ya TZS 5,000 kwa kilo, bei iliyokuwepo mwaka 2010. Ongezeko hili ni

sawa na asilimia 180. Kadhalika, vituo vipya vya ununuzi na uuzaji wa karafuu vimejengwa Unguja na Pemba, vituo vya zamani vingi vimekarabatiwa na huduma zote muhimu zinapatikana kwenye vituo hivyo. Pamoja na kahawa, chai, tende, biskuti, maji ya kunywa na pahala pa kukaa pazuri kwa wauzaji wa karafuu kwa wauzaji wa Shirika la *ZSTC*. (*Makofi)*

Tumefanikiwa sana katika kupambana na magendo ya Karafuu na wananchi wanauza karafuu zao katika Vituo vya *ZSTC*. Tunawashukuru sana wananchi wote wa Zanzibar na hasa wa wananchi wa Pemba ambapo karafuu zinatoka nyingi zaidi pamoja na Vikosi vyetu vya Ulinzi na Usalama kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kushirikiana na Serikali katika kupambana na magendo ya Karafuu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, maamuzi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba, ya kulifanyia mageuzi Shirika la *ZSTC* yamekuwa na manufaa makubwa kwetu. Ni habari njema kwetu sisi viongozi na wananchi kutambua kwamba Shirika hili limegeuka kutoka kuendeshwa kwa hasara kuwa Shirika lenye kuendesha shughuli zake kwa faida. Hivi sasa Shirika la *ZSTC* linalipa kodi ya mapato na kulipa faida nyengine Serikalini.

Imebainishwa kuwa kwa hesabu zilizokaguliwa katika mwaka wa 2011/2012, 2012/2013 pamoja na makadirio kwa hesabu za 2013/2014 Shirika limelipa jumla ya TZS 1.8 bilioni kama kodi ya mapato na kulipa gawio la TZS milioni 500 kwa mwaka 2013/2014.

Nachukua nafasi hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Uongozi na Wafanyakazi wa *ZSTC* kwa mafanikio haya makubwa. *(Makofi)*

Mafanikio yaliyopatikana katika kuliimarisha zao la karafuu, kupambana na magendo na kulifanyia mabadiliko Shirika la *ZSTC*, kwa hakika yametokana na Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya 2010/2015 ya kutolibinafsisha zao la karafuu, lakini uandaliwe mpango madhubuti wa maendeleo ya karafuu, ndio haya tuliyoyafanya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kutambua umuhimu wa viwanda katika kukuza uchumi na kuimarisha Soko la Ajira, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba, ilipanga na kutekeleza mipango mbali mbali yenye lengo la kukuza sekta ya viwanda. Ongezeko la bidhaa zinazozalishwa viwandani katika kipindi hiki cha miaka mitano nalo linatupa matumaini na ari ya kuendeleza kwa kasi zaidi.

Thamani ya bidhaa zilizozalishwa viwandani imeongezeka kutoka TZS bilioni 128 mwaka 2013 hadi kufikia TZS 136 bilioni mwaka 2014. Hili ni sawa na ongezeko la asilimia 5.5. Wawekezaji nao wamekuwa wakiwekeza katika viwanda vya

usafishaji nafaka, usindakaji wa maziwa; kiwanda kikubwa kilichopo Fumba cha *AZAM*, uzalishaji sukari kiwanda cha Mahonda, maji ya kunywa na viwanda mbali mbali viliopo, na vinywaji vingine kadhaa wa kadhaa.

Aidha, pamekuwa na ongezeko la ukuaji wa viwanda vidogo vidogo vinavyozalishwa na wajasiriamali wetu wanaozalisha sabuni, vifaa vya ujenzi, samani na bidhaa za viungo Unguja na Pemba.
Wajasiriamali hawa wanazalisha bidhaa za mwani keki, vileja, jam ya mwani na vyakula vyengine mbali mbali. Ukuaji huu vile vile umepelekea kuwepo kwa ongezeko la mchango wa sekta hii kwa pato la Taifa ambapo katika mwaka 2014 ulifikia asilimia 9.9 kutoka asilimia 6.9 mwaka 2013.

Taasisi ya Viwango tuliyoianzisha baada ya kupitisha Sheria ya Viwango Namba 1 ya mwaka 2011 imeanza kazi zake katika kuimarisha bidhaa zinazozalishwa na kuingizwa nchini.

Tunaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kuimarisha sekta ya Viwanda na Biashara ikiwa ni pamoja na kuyafanyia kazi mapendekezo yanayotolewa na Baraza la Biashara la Zanzibar (*ZNBC*) katika mikutano ya kila mwaka tunayoendelea kuifanya.

Natoa shukurani zangu za dhati kwa wajumbe wa *Zanzibar National Business Council (ZNBC)*, na wale wote wanaoshiriki katika mikutano ya mwaka ya Baraza hili, kwa michango na mashirikiano wanayotoa kwa lengo la kukuza sekta zetu muhimu za uchumi hasa Biashara, Viwanda na Utalii.*(Makofi)*

Aidha, natumai kwamba juhudi zetu za kuanzisha Tamasha la Biashara zitakuwa na mchango mkubwa sana katika kutangaza na kukuza biashara, viwanda na shughuli mbali mbali za ujasiriamali zinazoendeshwa nchini.

UTALII:

Mhe. Spika, katika kipindi cha miaka mitano, tumefanikiwa sana kuiendeleza sekta ya utalii. Tumeitekeleza kwa mafanikio makubwa dhana ya "Utalii kwa Wote" niliyoitangaza rasmi tarehe 16 Oktoba, 2011.

Serikali imeifanyia marekebisho Sheria ya Utalii ya mwaka 2009, na kupelekea kutungwa kwa Sheria mpya Namba 7 ya mwaka 2012 ambayo inakidhi haja na kwenda sambamba na dhana ya utalii kwa wote na kutoa miongozo imara ya kuendesha sekta hii.

Takwimu zinaonesha kuwa Idadi ya watalii 132,836 walitembelea Zanzibar katika mwaka 2010; ambapo katika mwaka 2014 watalii wapatao 311,801 waliwasili Zanzibar. Hili ni ongezeko la asilimia 134 katika kipindi cha miaka minne.

Katika kuhakikisha usalama wa wananchi na wageni wanaotutembelea, Serikali imeandaa Mradi wa usalama katika maeneo ya Mji wa Unguja. Jumla ya fedha kwa mradi wote kwa kipindi cha miaka mitano ni Dola za Marekani Milioni 28.9. Fedha zilizotengwa kwa matumizi ya mwaka wa kwanza ni TZS bilioni 10.

Mradi huu utatupatia vifaa vya *CCTV*, magari ya zimamoto, boti za doria na mashine ya kukagulia vifaa vya hatari vilivyofichwa katika magari. Vifaa hivyo tayari vimeshaagizwa na Kampuni ya *RAVITALCO* ya Romania na *ROM SOLUTIONS* iliyosajiliwa Zanzibar.

Vile vile, kwa kushirikiana na Kampuni ya Mawasiliano ya *ZTE* ya China tayari tumeshafunga kamera maalum za usalama (*CCTV*) katika maeneo ya Mji wa Unguja.

Kadhalika, kwa lengo la kuimarisha ulinzi kwa watalii, Serikali imeanzisha Kampuni ya Ulinzi ya JKU, ambayo itatoa huduma kwa sekta binafsi kwenye mahoteli. Sheria hii imepitishwa hapa Barazani.

Mhe. Spika, katika kipindi hiki cha miaka mitano, tumeshuhudia ongezeko la wawekezaji katika ujenzi wa hoteli za kisasa zenye hadhi ya juu. Aidha, tumeshuhudia ongezeko la vivutio vya utalii ikiwa ni pamoja na ujenzi wa viwanja vya michezo hasa mchezo wa gofu ambao unapendwa na watalii. Uwanja huu umejengwa na umezinduliwa katika hoteli ya *SEA CLIFF*.*(Makofi)*

Kumekuwa na ongezeko la idadi ya wageni wanaotoka Mashariki ya Kati na Mashariki ya mbali baada ya kuongezeka juhudi za kuitangaza Zanzibar katika maeneo hayo mapya. Tumefanikiwa kufungua ofisi yetu ya utalii katika Mji wa Mombai, tumemteua wakala maalum tunamlipa kila mwezi, na tayari alikuja na baadhi ya watendaji wenziwe wa huduma za utalii wiki mbili tatu zilizopita. Matarajio yetu tutapata watalii wengi sana kutoka India. *(Makofi)*

MAKUMBUSHO NA MAMBO YA KALE:

Mhe. Spika, katika kipindi cha miaka mitano, tumefanya jitihada za pamoja katika kufanya matengenezo ya makumbusho na kuyatunza mapango mbali mbali. Serikali iko katika hatua za mwisho za kukamilisha Sera ya Urithi wa Utamaduni itakayotoa muongozo wa matumizi bora ya maeneo ya urithi, ili kuimarisha shughuli za utalii.

Miongoni mwa maeneo ya historia, mambo ya kale na urithi wa utamaduni tuliyoweza kuyaimarisha ni Mangapwani, Kuumbi Jambiani na Kwa Bi. Khole kwa upande wa Unguja na Chwaka - Tumbe kwa upande wa Pemba. Natoa wito kwa wananchi waendeleze utamaduni wa kuyatembelea maeneo yetu haya ili kuimarisha utalii wa ndani.*(Makofi)*

SEKTA YA KILIMO:

Mhe. Spika, kwa kutambua kuwa, kilimo ndio chanzo kikuu cha ajira za wananchi kwa asilimia 70 ya ajira, na kinatoa asilimia 27.3 katika Pato la Taifa, niliahidi Serikali itafanya juhudi ya kuiendeleza sekta hii kwa kauli mbiu ya Mapinduzi ya Kilimo. Serikali imelitekeleza hilo, na imefanya jitihada na juhudi mbali mbali ili kuongeza uzalishaji wa mazao hasa mpunga ili kuwa na uhakika wa chakula na lishe.

Serikali imenunua pembejeo mbali mbali za kilimo, matrekta 14 ambayo yanaweza kuvuna kwa mara ya kwanza kwenye historia ya Zanzibar, na vifaa vyengine kadhaa.

Imeajiri wataalamu wa ugani na imetekeleza programu niliyoianzisha mwaka 2011 ya kuwapa ruzuku wakulima wetu ya asilimia 75 ya gharama za bei ya mbolea, mbegu, dawa ya magugu na huduma za matrekta.*(Makofi)*

Jitihada hizo za Serikali ziliweza kuzaa matunda kwa kuongezeka kiwango cha uzalishaji. Mavuno ya zao la mpunga kwa jumla yameongezeka kutoka tani 21,014 mwaka 2010 hadi tani 33,655 mwaka 2013. Hili ni sawa na ongezeko la asilimia 60. Katika kipindi hiki Zanzibar imepata mafanikio makubwa ya uzalishaji wa mazao muhimu ya chakula hadi kufikia tani 674,334.

Mhe. Spika, katika kipindi hiki cha miaka mitano, Serikali imefanya jitihada za kukiimarisha kilimo cha umwagiliaji maji ili kupunguza tatizo linalotukumba katika kilimo cha kutegemea mvua amabazo hazina uhakika baadhi ya wakati.

Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji wa hekta 2,200 katika mabonde ya Cheju, Kibokwa, Kilombero kwa hapa Unguja, Mlemele na Makwararani kwa kule Pemba umeanza kushughulikiwa kwa hatua mbali mbali. *(Makofi)*

Kadhalika, kwa kutambua umuhimu wa utafiti katika kuleta maendeleo ya kilimo, Serikali imefanya jitihada za kukiimarisha kituo cha utafiti wa kilimo Kizimbani kwa kukipandisha hadhi na daraja na kuwa Taasisi ya Utafiti ya Kizimbani. Sheria hii mpya imepitishwa hapa hapa Barazani. Taasisi hii imeshirikiana vyema na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

(COSTECH) katika shughuli za utafiti. Jumla ya mbegu 43 zimefanyiwa utafiti kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa zao la Mpunga wa Kimataifa *(IRRI).* Kadhalika, Taasisi hii imefanya tafiti juu ya mbegu za mazao ya mizizi na kutoa mbegu zinazostahamili maradhi na kunawiri katika mazingira yetu.

Katika kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora za mazao mbali mbali, Serikali imekuwa ikiendeleza majaribio ya mbegu ya mpunga ya *NERICA* katika vituo vya Mwera na Kizimbani. Hivi sasa wakulima tayari wameshapatiwa mbegu hii kwa ajili ya uzalishaji na kuiendeleza na wakulima wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Tafiti mbali mbali zilizofanywa zimeonesha kuwa hii ni mbegu bora kwa mazingira yetu, kwa kuwa inastahamili ukame na inastawi hata katika ardhi isiyo ya mabondeni, pale unapopanda muhogo panda *NERICA* itaota na itamea.

Mhe. Spika, Serikali imefanya juhudi kubwa katika kuhifadhi misitu na miti yetu ya asili. Zanzibar imejaaliwa kuwa na miti ya aina mbali mbali ya asili ambayo idadi yake imeanza kupotea na hatukuwa na utaratibu bora wa kuitunza.

Katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali ilifanya jitihada za kuendesha sensa ya miti mwaka 2013 ili kujua idadi ya miti yote iliyopo Zanzibar.
Pamoja na jitihada hizo, Serikali imeongeza juhudi za uhifadhi wa misitu yetu ya asili ikiwa ni pamoja na msitu wa Jozani, Ufufuma, Kiwengwa na Ngezi kule Makangale pamoja na kusimamia Mradi wa Hifadhi ya Misitu ya Asili *(HIMA)* katika maeneo mbali mbali, Unguja na Pemba. *(Makofi)*

Kwa lengo la kuongeza idadi ya miti tuliyonayo, katika kipindi hiki jumla ya miti milioni 5 ya misitu ilioteshwa katika vitalu vya Serikali peke yake, na miche milioni 8 katika vitalu vya watu binafsi.

Jitihada maalum zimefanywa katika kuimarisha kilimo cha karafuu, ambalo ni zao letu kuu la uchumi. Serikali imewahamasisha wakulima wa zao la karafuu kuyaendeleza mashamba yao na yale mashamba ya Serikali kuwapatia miche mipya bila ya malipo. *(Makofi)*

Hatua hiyo ni miongoni mwa jitihada zangu za mwanzo kabisa za kuimarisha na kulikuza zao la karafuu, ni miongoni mwa utekelezaji wa mpango wetu wa miaka kumi wa kulifufua zao la karafuu.

Katika kipindi cha 2010-2014 jumla ya miche ya mikarafuu milioni 3.7 iligawiwa kwa wakulima kati ya lengo tulilojiwekea na kukusudia; la kutoa miche milioni 3.8, ni miche laki 1 tu tumeshindwa kutekeleza. Hata hivyo ni matumaini yangu kazi hii tuliyoifanya tumeifanya vizuri. (*Makofi)*

MIFUGO NA UVUVI:

Mhe. Spika, katika Sekta ya Mifugo, serikali iliweka malengo ya kuleta mapinduzi ya ufugaji ili kuongeza tija na ubora wa mazao yanayotokana na shughuli hiyo. Dhamira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwa na ufugaji wa kisasa wa ng'ombe wa maziwa, mbuzi na kuku kwa lengo la kuongeza tija na kipato cha wafugaji wetu. Soko la maziwa sasa limekua kubwa kutokana na muwekezaji mzalendo ndugu yetu Said Salim Bakhressa (kufungua kiwanda cha maziwa) cha Maziwa cha kisasa katika eneo la Fumba. (*Makofi*)

Hichi ni kiwanda cha kisasa cha mwanzo katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, mitambo iliyopo katika kiwanda hichi haipo katika kiwanda chengine chochote cha maziwa kwenye ukanda wetu huu. Nendeni kakitembeleeni mtaiona dunia ilivyo.*(Makofi)*

Serikali vile vile, imeimarisha maabara ya mifugo Maruhubi kwa kuifanyia matengenezo makubwa, kuweka vifaa vya kisasa vya kuhifadhia mbegu bora za ng'ombe, na kuendeleza mradi wa upandishaji ng'ombe kwa sindano ili kupata ng'ombe bora.

Kadhalika, serikali iliendesha mradi wa kudhibiti maradhi ya mifugo yasiyo na mipaka ambapo ng'ombe 20,000 walichanjwa kwa kuwakinga na maradhi ya chambavu na kimeta, na kuku 80,000 walichanjwa ili kuwakinga na mahepe.

Mhe. Spika, nilianzisha Mapinduzi ya Uvuvi kama nilivyotamka katika Hotuba yangu ya tarehe 11 Novemba, 2010, nilipolihutubia Baraza la Nane.

Mwaka 2010 tuliahidi kufanya jitihada za kuziimarisha shughuli za uvuvi kwa kutambua umuhimu wake katika kutoa ajira, kutupatia lishe bora na kuongeza mchango wake katika pato la Taifa. Nina furaha kuwa serikali imepata mafanikio katika utekelezaji wa azma hiyo, ambapo mchango wa sekta hiyo katika pato la Taifa sasa umefikia asilimia 7.2. Jumla ya tani 148,535 za samaki zenye thamani ya TZS bilioni 527.5 zilivuliwa hadi mwaka 2014.*(Makofi)*

Ni jambo la kutia moyo, kuona kuwa jitihada za serikali za kushirikiana na wananchi katika kukabiliana na vitendo vya uvuvi haramu, na kuimarisha hifadhi ya mazingira ya bahari, zimesaidia sana kuongeza kiwango cha samaki wanaovuliwa. Jumla ya wavuvi wapatao 2,520 wamepatiwa mafunzo ya uvuvi bora; yakiwemo ufugaji wa samaki na viumbe wengine wa baharini. *(Makofi)*

Serikali imeandaa mpango wa ujenzi wa kituo cha kutotolea vifaranga vya samaki katika eneo la Beit- el-Ras na imetoa mafunzo kwa wafugaji wa samaki 69 kuhusu

utengenezaji wa chakula, ulishaji, namna ya kulisha vifaranga, uchimbaji wa mabwawa na utunzaji bora wa samaki. Vipo vifaranga vya samaki mbali ya vile vya kuku.*(Makofi)*

Mhe. Spika, wakati huo huo, zao la mwani ni miongoni mwa mazao ya baharini yanayotupatia fedha za kigeni. Jumla ya tani 51,687 za mwani mkavu zenye thamani ya TZS bilioni 187 zimesafirishwa nje ya nchi katika kipindi hiki.

Serikali hivi karibuni imewapatia vihori wakulima wa mwani wa Unguja na Pemba kwa ajili ya kubebea mwani wao. Tunafanya juhudi kuwapa nguvu wakulima wetu wa mwani, ili kuhakikisha zao hili linasarifiwa hapa nchini kwa lengo la kukuza uchumi wetu na kuongeza kipato cha wakulima wetu.*(Makofi)*

Tunalisarifu wenyewe, ndio maana nikasema pale mwanzo tunatengeneza keki za mwani, vileja vya mwani, visheti vya mwani, nangatai za mwani, kashata za mwani, jamu ya mwani; vyote nimeviona kwa jicho langu na vyengine nimevijaribu kuvionja. *(Makofi)*

Aidha, mwani umekuwa chakula maarufuu kwa supu ya mwani. Kufuatia safari yangu ya China na Vietnam niliwashajihisha wawekezaji waje washiriki katika sekta hii. Matumaini yangu kwamba utekelezaji utakuwa mzuri. Timu ya mabingwa wa Vietnam walikuja nchini na tumeanza vizuri mjadala nao. *(Makofi)*

Kwa lengo la kuongeza mapato yanayotokana na uvuvi, serikali imejiwekea lengo la kuanzisha programu ya uvuvi wa bahari kuu. Programu hii inakusudiwa kuwawezesha wavuvi wetu kuvua katika kina kirefu cha maji, ili kuongeza kiwango cha samaki wanaovuliwa na kuongeza fursa za ajira, biashara na kuchangia katika ukuaji wa uchumi. Programu hiyo itaendeshwa kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Japan (*JICA*). Maandalizi ya programu hiyo yamekwishaanza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, serikali imeandaa mpango wa kuendeleza uvuvi wa bahari kuu kwa lengo la kuwawezesha wavuvi na vifaa kuongeza kipato chao.

Serikali imefikia makubaliano na Serikali ya Japan kupitia Shirika la Maendeleo la Japan (*JICA*) kuimarisha diko na soko la samaki la Malindi ili liwe la kisasa na lenye uwezo wa kuhudumia vyombo vya uvuvi vikiwemo vinavyovua bahari kuu. Utekelezaji wa mradi huo utakaogharimu Dola za Marekani 244,500 na utaanza mwakahuu. Utakapomalizika utawanufaisha wananchi wengi.

Kadhalika, serikali imewakaribisha wawekezaji kwa makubaliano ya kuwashirikisha wavuvi wazalendo. Katika mwaka 2015, Serikali ya Mapinduzi ya

Zanzibar, imefikia makubaliano ya awali na Mwekezaji *(Hairu Fisheries Management Company)* kutoka Sri Lanka ya kuleta vyombo 20 vya urefu wa mita 18 ambavyo vina uwezo wa kuvua katika kina kirefu na kukaa baharini kwa muda mrefu. Aidha, Mwekezaji huyo atajenga Kiwanda cha Boti za Uvuvi za mita 6 na mita 9 hapa hapa ambazo watauziwa wavuvi wetu.*(Makofi)*

Hatua zote hizo zitaimarisha juhudi za serikali za kuwawezesha wananchi wetu kuitumia raslimali ya bahari kuu kujiongezea kipato chao.

MAZINGIRA:

Mhe. Spika, serikali inatambua umuhimu wa hifadhi ya mazingira katika utekelezaji wa mipango yetu yote ya maendeleo, na imechukua jitihada za kukabiliana na uharibifu wake unaosababishwa na wanadamu na ule unaotokana na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa na serikali ni kuandaa Sera mpya ya Mazingira ya mwaka 2013; yenye kutoa muongozo kwa shughuli za uhifadhi wa mazingira nchini na kutayarisha Sheria mpya ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka huu 2015.

Serikali imezingatia haja ya kufanya tathmini ya athari za mazingira katika miradi ya uwekezaji ambapo jumla ya tathmini 71 za athari za mazingira zimefanywa na wahusika kupewa vyeti vinavyothibitishwa kwamba wamefanya tathmini hiyo. Kadhalika, miradi 221 imefanyiwa ufuatiliaji wa kimazingira na kutolewa ushauri. Vile vile, serikali imechukua hatua za kukabiliana na athari za tabia nchi.

Mhe. Spika, mnamo mwezi Septemba, mwaka 2014 nilihudhuria mkutano wa Kimataifa wa nchi za visiwa, nchi ambazo zinazoendelea nchini Samoa, nilikwenda kumwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete.

Tanzania ilipata heshima ya kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa kuendesha mkutano ule, nami nikapata heshima maalum ya kuhutubia kikao hicho, ambacho katika hotuba yangu ya ufunguzi niliitoa na Mkutano huu uliendeshwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Mhe. Ban ki Moon. *(Makofi)*

Tukio mojawapo muhimu wakati wa mkutano huo ni uzinduzi wa Mpango wa Magharibi ya Bahari ya Hindi, wa changamoto za Ukanda wa Pwani wa Mabadiliko ya Tabianchi *(Western Indian Ocean Coastal Challenges (WIOCC)*. Visiwa vinavyoshiriki mpango huo ni pamoja na Sychelles, Comoro, Mauritius, Reunion na Zanzibar.

Uzinduzi huo ulihudhuriwa na viongozi mbali mbali wa nchi za visiwa pamoja na Washirika wa Maendeleo wakiwemo *Island Partnership (GLISPA).* Katika mkutano huo mimi na Rais wa Sychelles, tulipata fursa maalum ya kuwahutubia wajumbe. Sisi tunatakiwa viongozi waanzilishi wa mradi huu. *(Makofi)*

VYAMA VYA USHIRIKA NA SACCOS:

Mhe. Spika, wananchi wamefaidika sana na taasisi hizo kwa kujipatia ajira na mikopo ya kujiendeleza. Ili kukuza taaluma ya vyama vya ushirika na SACCOS zilizopo, serikali imeandaa mpango mkuu wa mafunzo wa miaka mitatu *(Training Master Plan),* pamoja na kuandaa miongozo ya aina 13 ya kufundishia kwa mujibu wa mahitaji ya mafunzo yaliyoibuliwa.

KAZI, AJIRA NA UTUMISHI WA UMMA:

Mhe. Spika, katika kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana na wanawake, na ili tuweze kuwajengea uwezo wa kipato wananchi hao, katika kipindi hiki cha miaka mitano, serikali imeanzisha Mfuko wa Uwezeshaji, tuliuzindua tarehe 21 Disemba, 2013 ukiwa na jumla ya fedha TZS bilioni 2.413, baada ya kuunganishwa mifuko ifuatayo:

- Mfuko wa Kujitegemea, ulioanzishwa na Dkt. Salmin Amour.
- Mfuko wa JK na AK; na
- Mfuko wa Vijana.

Kati ya fedha hizo, TZS milioni 973 zilipatikana kwa kuchangishwa kupitia Kamati niliyoiunda, TZS bilioni 1.2 zilitokana na mfuko wa AK/JK na jumla ya TZS milioni 140 ni za Mfuko wa Rais wa Kujitegemea, na TZS milioni 100 zilitokana na Mfuko wa Vijana.

Nataka nichukue nafasi hii maalum nimpongeze kwa dhati sana Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma; Maalim Haroun Ali Suleiman, Mwakilishi wa Jimbo la Makunduchi kwa kuridhia dhamana niliyompa ya kuwa Mwenyekiti wa Kusimamia kuchangishwa fedha hizo. *(Makofi)*

Kupitia kwake nawapongeza Wajumbe wote 12 wa Kamati yake; wengine wamo humu ukumbini wamefanya kazi kubwa sana, wao wenyewe Wajumbe walichangia baadhi yao si chini ya shilingi milioni mia moja na zaidi.*(Makofi)*

Lengo kuu la kuunda Mfuko huu wa Uwezeshaji ni kuwa mfuko ulio imara zaidi katika kuwasaidia vijana, wanawake na vikundi mbali mbali vya wajasiriamali katika shughuli zao za kujiendeleza kiuchumi.

Katika kuhakikisha kuwa vijana wanapata fursa za ajira, tumefanikiwa kuzindua Mpango Mkakati wa Ajira kwa vijana wa mwaka 2014/2018. Mpango huu umeweka vipaumbele katika sekta za ujasiriamali, elimu ya amali pamoja na ufundi stadi.

Tumepata mafanikio makubwa katika kutekeleza Programu ya Ajira kwa vijana katika sekta ya kilimo kupitia mashamba darasa, shughuli za uvuvi, ufugaji na utalii.

Nachukua fursa hii kuwapongeza vijana na wanawake kwa ari na moyo waliouonesha katika kuunga mkono jitihada hizi na kwa kutumia vizuri fursa tulizowaandalia.*(Makofi)*

Mhe. Spika, katika kipindi hiki cha miaka mitano tumefanikisha kupatikana kwa nafasi za ajira 25,019 serikalini na katika Sekta Binafsi. Kati ya nafasi hizo, nafasi za ajira 4,850 zilikuwa za taasisi mbali mbali za Serikali, na nafasi za ajira 20,169 zilitokana na sekta binafsi, zikijumuisha ajira za nje ya nchi na taasisi zinazojitegemea kwa wananchi wa Zanzibar wenye sifa zilizohitajika.

Ajira bado ni changamoto nchini kwetu, na hata katika nchi za nje zilizoendelea, hakuna njia ya mkato, tuwashajihishe vijana kutumia taaluma wanazozipata wajiajiri wenyewe katika sekta binafsi na wajiendeleze. Kwa kiasi kikubwa tumefanikiwa sana kupambana na tatizo hilo, na mipango yetu chini ya mkakati wa ajira unatoa matumaini mazuri ya baadaye.

Mhe. Spika, wakati huo huo, serikali imefanikiwa kupandisha mishahara ya watumishi wa umma kutoka kima cha chini cha mshahara wa Tsh.100,000 hadi TZS 125,000 kwa mwezi, sawa na asilimia ishirini na tano (25%), pamoja na kufanya marekebisho ya mishahara ya wataalamu na wafanyakazi mbali mbali; wakiwemo madaktari, mainjinia, marubani, walimu wa sayansi na wengine kadhaa. Serikali ilifanya marekebisho hayo mwanzo katika mwaka 2011.

Vile vile, mwishoni mwa mwaka 2013 na mwanzoni mwa mwaka 2014, serikali ilipandisha tena kima cha chini cha mshahara kutoka TZS 125,000 hadi TZS 150,000 sawa na asilimia ishirini (20%), pamoja na kurekebisha mishahara ya watumishi wazoefu, waliotumikia katika utumishi wa umma kwa miaka kumi na tano (15) na zaidi ambao wana mishahara kati ya TZS 150,000 hadi TZS 225,000, nao tuliwaongezea mishahara yao na kunyanyua kipato chao. *(Makofi)*

Lakini vile vile serikali iliongeza posho mbali mbali ambazo tayari zimeanza kutolewa. Yapo malimbikizo ya mishahara na hasa malimbikizo ya mishahara ya walimu. Niliahidi nilipokutana nao, niliahidi nilipokutana na Vyama huru vya

Wafanyakazi kwamba katika Bajeti hii inayoanza Julai 1 mwaka huu tutayalipa madeni hayo yote wanayoidai serikali, na bajeti hii tayari mumeshaipitisha juzi pamoja na *Appropriation Bill.* Hongereni sana. *(Makofi)*

MIUNDO YA UTUMISHI

Mhe. Spika, katika kuimarisha utendaji kazi, serikali imerudisha tena utaratibu wa kuwa na Miundo ya Utumishi katika Mawizara na Taasisi mbali mbali za serikali. Wizara zote tayari zimeshatengeneza Miundo yao ya Utumishi na imewasilishwa katika Kamisheni ya Utumishi wa Umma kwa kuthibitishwa, maana wao lazima wathibitishe kwa mujibu wa sheria.

Taasisi nyengine za serikali yakiwemo mashirika na taasisi zinazojitegemea zimo katika hatua za utayarishaji wa Miundo yao ya Utumishi kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma.

Serikali imetoa miongozo mbali mbali kwa ajili ya kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza katika marekebisho ya mishahara na maposho, ili kuhakikisha kwamba hakuna mfanyakazi atakayedhulumiwa haki yake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, vile vile, katika kipindi hiki cha miaka mitano, Serikali imeimarisha maslahi ya wananchi wanaofanya kazi katika sekta Binafsi kwa kuitaka iongeze mishahara na posho za wafanyakazi wao. Wafanyakazi wa sekta hiyo wameongezewa kiwango cha mishahara yao kutoka TZS 70,000 mwaka 2010 hadi 145,000 kwa sasa, sawa na ongezeko la asilimia 107. *(Makofi)*

Mhe. Spika, natumia fursa hili kulipongeza Baraza lako Tukufu kwa kupitisha Sheria Namba 2 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011. Sheria hii imetuwezesha kuweka Miundo imara ya uendeshaji na usimamizi wa Utumishi wa Umma na mambo mengine yanayohusiana na hayo. *(Makofi)*

Kutokana na sheria hii, Serikali imeunda Kamisheni ya Utumishi wa Umma pamoja na Tume ya Utumishi Serikalini, Tume ya Utumishi wa Mahakama, Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi na Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ. Taasisi hizi ni muhimu katika kulinda maslahi na haki za wafanyakazi hapa nchini, na zimetoa mchango mkubwa sana katika kuweka misingi mikuu ya maadili ya Utumishi wa Umma na usimamizi wa rasilimali watu.

Jumla ya Sheria za kazi 12 zimetungwa na zimeanza kutumika, zikiwemo Kanuni za mwaka 2014 za Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 2 ya mwaka 2011. Haya yote ni mafanikio ya utekelezaji wa ahadi nilizozitoa za kulinda na kukuza maslahi ya wafanyakazi Serikalini na katika Sekta Binafsi.*(Makofi)*

Mhe. Spika, katika kuimarisha ustawi wa kinamama na watoto, kuanzia tarehe 21 Aprili, 2015 tulianzisha utaratibu unaowawezesha akina mama wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*), kulipwa mafao ya uzazi pale wanapokwenda kujifungua, ili yawasaidie kuimarisha afya zao na za watoto katika kipindi hicho muhimu. Malipo ya mafao ya uzazi hayaathiri mafao yao, ambayo muhusika atapata wakati atakapostaafu, haya ni mafao ya ziada. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunamaliza miaka mitano ikiwa tumo katika hatua za mwisho za kukamilisha Sera ya Usalama na Afya Kazini, ili kuweka mfumo mzuri wa afya katika maeneo yote ya kazi, kwa lengo la kuwakinga wafanyakazi wetu na ajali na majanga mengine yanayotokea katika sehemu za kazi. Aidha, tunamaliza kipindi hiki ikiwa tupo katika hatua za kuanzisha Bima ya Afya. Tumeshafikia hatua nzuri katika azma yetu hii.

SEKTA YA MIUNDOMBINU:

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba ilitambua kuwa lengo lake la kukuza uchumi wa Zanzibar halitaweza kufikiwa na kufanikiwa bila ya azma hiyo kwenda sambamba na uimarishaji wa miundombinu ya uchumi kama vile ya ujenzi wa barabara, bandari, viwanja vya ndege, kuimarisha maeneo huru ya uwekezaji pamoja na kuwa na nishati ya uhakika ya umeme.

Kwa hivyo, katika kipindi hiki cha miaka mitano, jitihada kubwa zimefanywa katika kuimarisha miundombinu hiyo kwa ajili ya uchumi wetu.

Mhe. Spika, kuhusu miundombinu ya barabara, Serikali imeendeleza na imekamilisha kazi za ujenzi wa barabara zote kuu zinazoingia mijini. Kadhalika, tumeweza kujenga barabara ndogo ndogo za mijini na mashamba, na kuifanya Zanzibar sasa kuwa mfano wa nchi zenye mtandao mzuri wa barabara unaounganisha miji na mashamba, na kuwa ni kichocheo muhimu cha maendeleo ya uchumi na kurahisisha shughuli za usafiri wa wananchi na mizigo yao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba, imekamilisha kazi ya ujenzi wa barabara 11 zenye urefu wa (*km* 102) katika Kisiwa cha Pemba na barabara 4 zenye urefu wa (*km* 34.85) katika Kisiwa cha Unguja. Barabara hizi zimejengwa kwa msaada wa *MCC* ya Marekani, *BADEA* na *Saudi Fund* na SMZ. Hivi karibuni tunatarajia kufanya uzinduzi wa barabara ya Wete hadi Gando (*km* 15) na barabara ya Wete hadi Konde (*km* 15), ujenzi ambao utakuwa ni suluhisho la tatizo la barabara la muda mrefu lililokuwa likiwasumbua wananchi wanaoishi katika maeneo mbali mbali.

Kadhalika, kupitia Mfuko wa Barabara, Serikali ilikamilisha ujenzi wa barabara ya Amani hadi Mtoni (km 4) na barabara ya njia nne hadi inayofikia Umbuji yenye urefu wa (*km* 5).

Kazi ya ujenzi wa barabara ya Jendele, kupitia Cheju hadi Unguja Ukuu / Kae Bona yenye urefu (*km* 11.7) na barabara ya Koani hadi Jumbi yenye urefu wa (*km* 6.3) zinazojengwa kwa msaada wa *BADEA* nazo zinaendelea vizuri.

Kadhalika, ujenzi wa barabara Ole hadi Kengeja yenye urefu wa (*km* 35) inayojengwa kwa msaada wa *OPEC Fund* umeshaanza, na barabara inayoanzia Chake Chake kwendea Wete kwa jina la barabara ya zamani nao utaanza hivi karibuni. *(Makofi)*

Mhe. Spika, uimarishaji wa usafiri wa anga ni miongoni mwa masuala yanayozingatiwa na Serikali ya Awamu ya Saba, kama nilivyoahidi wakati wa uzinduzi wa Baraza hili pale mwaka 2010.

Jitihada kubwa zimefanywa katika kukamilisha kazi ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume ikiwa ni pamoja na njia ya kurukia ndege, maegesho ya ndege, ujenzi wa uzio, sehemu ya kuegesha magari, ujenzi wa jengo la abiria, na kuimarisha huduma mbali mbali zinazohusiana na matumizi ya uwanja huo.

Ujenzi wa njia ya kurukia ndege na sehemu ya kuegesha ndege umekamilika. Ndege yoyote iliyotengenezwa dunia hivi sasa, inayoruka juu inaweza kutua Zanzibar, pamoja na ile *Airbus* 380, ikija Zanzibar itatua bila ya hofu yoyote. *(Makofi)*

Ujenzi wa jengo jipya la Abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume nao umefikia hatua nzuri sana. Nimeambiwa ujenzi wake umevuka asilimia 70, tunatarajia kukabidhiwa uwanja huu Oktoba mwaka huu. Mambo yote yakienda vizuri yanavyokwenda sasa, tutasherehekea uzinduzi wa jengo jipya la abira.

Mwezi wa Oktoba sio *saatil khabar,* ni ahadi niliyoambiwa na uongozi wa Serikali ya China. Ujumbe maalum ulikuja hapa kutoka China ukiongozwa na mjumbe wa *Communist Party,* na mwezi mmoja na nusu uliopita Balozi Mdogo wa China mwenyewe katika ziara nilipotembelea uwanja ule, jengo la *Terminal,* amenithibitishia mbele ya wajumbe wote niliofuatana nao kwamba Oktoba, unamaliza. Na kwamba kazi wataimaliza *BCEG* wenyewe, tuombe dua jitihada hizi ziende vizuri, na wenzetu hawa Mungu awape uwezo wa kumaliza kazi iliyosalia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuhusu Kiwanja cha Ndege cha Pemba. Serikali inaendeleza mipango mbali mbali kwa ajili ya kukiimarisha kiwanja hiki ili nacho kiweze kutumika usiku na mchana, na baadae kiweze kutumiwa na ndege zilizo kubwa zaidi.

Katika juhudi tunazoendelea nazo na tunazozichukua za kukiimarisha Kiwanja cha ndege cha Pemba tarehe 16 Machi, 2015 Serikali iliingia mkataba na Kampuni ya *Safegate* ya Ujerumani, kwa ajili ya uletaji wa vifaa pamoja na kusimamia uwekaji wa taa katika kiwanja kwa gharama ya Dola za Kimarekani 508,219.45. Hivi sasa, Kampuni hiyo imeshalipwa malipo ya awali ya asilimia 20. *(Makofi)*

Vifaa mbali mbali kwa ajili ya uwekaji taa hizo vimeshafika Pemba, na kazi ya uchimbaji misingi kwa ajili ya kulaza nyaya imeanza. Kwa upande wa usimamizi wa kazi za kawaida yaani *"civil work"* mtaalamu wa Kampuni hiyo tayari amewasili katika kiwanja cha ndege cha Pemba kuisimamia kazi ya uchimbaji misingi na mashimo. Kazi ya uwekaji taa nimeambiwa inatarajiwa kumalizika mwishoni mwa mwezi wa Julai. Kwa hivyo tuombe Mungu nayo ahadi hii nayo ikamilishwe. *(Makofi)*

Sambamba na juhudi hizi, Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na washirika wa maendeleo mbali mbali ili kupata fedha kwa ajili ya kuimarisha zaidi Uwanja wa Ndege wa Pemba. Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)* tayari imekubali kufadhili kazi ya Upembuzi Yakinufu na mpango mkuu wa kiwanja hicho; kazi ambayo inatarajiwa kuanza ndani ya kipindi cha miezi sita ijayo.

Kukamilika kwa mradi huu kwa hakika kutasaidia sana katika jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali, za kuitangaza Pemba katika masoko ya utalii duniani na kuimarisha biashara na huduma za usafiri kwa wananchi wa Unguja na Pemba. Panapo uhai na majaaliwa Pemba tutaifungua kwa ajili ya utalii. *(Makofi)*

BANDARI:

Mhe. Spika, Serikali imezingatia umuhimu wa bandari, kwa hivyo kwa kushirikiana na Kampuni ya *Azam Marine,* nyote mnajua na mumeona na mnapatumia, imejenga majengo mapya ya kupumzikia abiria katika Bandari ya Malindi.

Aidha, vifaa mbali mbali vimenunuliwa ili kuongeza ufanisi na kasi ya upakiaji na uteremshaji wa mizigo katika meli zinazofika Bandarini. Serikali vile vile imeifanyia matengenezo makubwa gati ya Mkoani Pemba ili kurahisisha shughuli za usafiri wa vyombo na abiria wanaoitumia bandari hiyo.

Ujenzi wa gati ya Tumbatu unaendelea uzuri, pamoja na ujenzi wa gati ya Mkokotoni. Fedha zake zimetengwa hata katika bajeti hii ya mwaka huu. Katika kukabiliana na tatizo la uhaba wa nafasi katika Bandari ya Malindi, na kuwa na Bandari ya kisasa yenye huduma bora zaidi, tayari Serikali imeanza kuchukua hatua za awali za ujenzi wa Bandari mpya ya Mpiga duri. *(Makofi)*
Sio matayarisho, ujenzi wa Bandari mpya ya Mpiga duri. Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China imekubali kushirikiana nasi katika ujenzi huo kupitia Benki ya *Exim* ambapo hatua za Upembuzi Yakinifu zimeshafanywa na Kampuni ya *CHEC (China Harbour Engineering Company Ltd)* kutoka China, na Kampuni hii ndio itakayoijenga bandari hiyo kwa kushirikiana na Serikali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tumefikia hatua nzuri sana katika ujenzi wa bandari hii, ujenzi ambao ulibuniwa kabla ya mwaka 2000, nataka nirudie, ujenzi wa Bandari ya Mpiga duri ulibuniwa kabla ya mwaka 2000, ni wakati wa uongozi wa Dkt. Salmin Amour. *(Makofi)*

Serikali imepanga kujenga Bandari hii kubwa na ya kisasa ili Zanzibar iweze kwenda sambamba na mabadiliko ya kibiashara na uchumi yanayotokea duniani.

Bandari hii mpya itahudumia meli zenye uzito wa Tani 50,000 *(Deadweight tonnage)* na itakuwa na urefu wa mita 300 na upana wa mita 490. Ujenzi wa bandari hiyo utaanza mara tu baada ya kukabidhiwa jengo la *Terminal 2*, ndivyo walivyonieleza viongozi wa Serikali ya Watu wa China, kwamba hatutaanza kujenga bandari mpaka tukukabidhini jengo la abiria la Uwanja wa Ndege *Terminal 2* kwanza. Ilivyokuwa tutakabidhiwa Oktoba basi natarajia mwaka mpya mambo yataanza Mpiga duri. *(Makofi)*

Kwa lengo la kuimarisha usafiri wa baharini, kama mjuavyo nyote na wananchi wote wanavyojua, tuliamua kwa makusudi kuikata fedha kila Wizara pamoja na Baraza la Wawakilishi, ili tutengeneze meli mpya ya abiria. Ulikuwa uamuzi mzito, uamuzi mgumu lakini iliamua, na leo nataka nikupongezeni sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa kuiunga mkono Serikali kukubali na kuridhia Wizara zote tuzipunguze fedha za *OC* ili tutengeneze meli yetu mpya, hongereni sana. *(Makofi)*

Nyote mnajua meli hii tumeamua ijengwe katika Jamhuri ya Watu wa Korea yaani Korea ya Kusini, na nimeambiwa inatarajiwa kufika nchini mwisho wa mwezi wa Julai. Leo nimekutana na Mwenyekiti wa Shirika la Bandari baada ya Sala ya Ijumaa msikitini akaninon'goneza, na wao wanajiandaa namna ya kuanza meli hii. Meli hii ina uwezo wa kuchukua abiria 1200 na mizigo isiyopungua tani 200. *(Makofi)*

UMEME:

Mhe. Spika, nishati ya umeme ni muhimu katika kuimarisha ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii na maendeleo ya wananchi wetu. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika awamu zake zote mbali mbali zimefanya jitihada kubwa za kuhakikisha kwamba Zanzibar inakuwa na huduma za nishati ya umeme ya uhakika.

Katika kipindi cha uongozi wa Serikali yetu hii ya Awamu wa Saba, tumeweza kukamilisha hatua ambazo zilianzishwa na Awamu ya Sita; za kuwa na umeme wa *MW 100* kwa Unguja na *MW 20* kwa Pemba, viwango ambavyo sasa ni zaidi ya mahitaji yetu. Sisi tulikamilisha kazi, wenzetu wa Awamu ya Sita walianza kazi.

Katika hotuba yangu ya tarehe 11 Novemba, 2010 nilipolizindua Baraza la Nane, niliahidi kuwa Serikali itapeleka umeme katika maeneo yote ambayo bado hayajapata nishati hiyo ikiwa ni pamoja na kwenye visiwa vidogo vidogo; Kisiwa cha Makoongwe, Kisiwa Panza na Kisiwa cha Shamiani, niliahidi kupeleka umeme. Jitihada kila mmoja anaziona akienda kule, nguzo tayari, waya zimeanza tulichobakisha ni kulaza waya ule chini ya bahari kwa Makoongwe na kusambaza. Kazi hiyo tutaimaliza muda mfupi sana ujao, na Shamiani tutauvusha kwenye nguzo tu maana si mbali pale Shamiani. *(Makofi)*

Hivi sasa huduma za umeme zinapatikana katika miji yote na vijijini, na tayari vijiji 129 tushaufikisha umeme badala ya vijiji 123, sisi tumeongeza 6 tayari katika kipindi hiki. (*Makofi*)

UCHIMBAJI WA MAFUTA NA GESI:

Mhe. Spika, nimefurahi sana kuona kuwa Baraza hili la Nane limejadili kwa kina suala la uchimbaji wa mafuta na gesi na mumeweza kutoa michango yenu, maoni yenu na kama kawaida yenu kuishauri Serikali kwa namna mbali mbali kuhusiana na suala hili. Hivi sasa tumefikia pahala pazuri sana, hasa tukizingatia kuwa Katiba Inayopendekezwa imezingatia matakwa ya Zanzibar kuhusu gesi na umeme juu ya suala hili. *(Makofi)*

Katika kipindi cha miaka mitano, Serikali imefanya mazungumzo marefu sana, na kusaini makubaliano ya awali (*Memorandum of Understanding*) na Kampuni zinazoshughulikia uchimbaji wa mafuta. Kampuni hizi ni Kampuni ya *RAK Gas* ya Ras Al Khaima, na tumesaini makubaliano hayo kufuatia ziara yangu mji wa Ras Al Khaima katika Falme za Kiarabu mwaka 2012, na vile vile tumesaini makubaliano na Kampuni ya *Shell*, na Kampuni hii tumefikia uamuzi huo baada ya ziara yangu niliyoifanya Uholanzi katika mwezi Agosti, 2013. *(Makofi)*

Dhamira yetu ni kuona kuwa katika kipindi kifupi kijacho, mafuta na gesi yanaanzwa kuchimbwa Zanzibar, baada ya kumaliza kazi ya kisheria ambayo tunasubiri tu muda ufike na sisi tuje tuanze kazi na hawa ambao wamejitokeza au wengine ambao watakuja baadae. *(Makofi)*

Tushapatambua na tushapajua, pahala tutakapojenga matangi makubwa na ya kisasa ya kuhifadhia gesi inayoitwa *liquefied gas* (gesi ya maji maji) wanaohusika na kuja kuwekeza wanatusubiri sisi tu wao wako tayari. Leo ni siri yangu sisemi sehemu gani, baadae nitasema rasmi wakati ukifika. (*Makofi*)

HUDUMA ZA JAMII:

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba, ilitambua wazi kuwa kuimarisha huduma za jamii ni jukumu lake la msingi, na hatua muhimu ya kuendeleza shabaha ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya 12 Januari, 1964 zimeendelea kuchukuliwa. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali imechukua jitihada mbali mbali katika kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za Elimu, Afya na maji safi na salama katika maeneo yote ya Unguja na Pemba, mijini na mashamba.*(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa upande wa sekta ya elimu, niliahidi kuendeleza mafanikio ya elimu yaliyopatikana katika awamu zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zilizopita.

Kadhalika, Serikali yangu iliweka azma ya kuimarisha ubora wa elimu inayotolewa katika ngazi zote kuanzia skuli ya Maandalizi, Msingi, Sekondari na Elimu ya Juu pamoja na Mafunzo ya Elimu Amali na Elimu Mbadala.

Pamoja na hatua hizo, tumedhamiria kuimarisha masomo ya sayansi hasa kwa watoto wa kike, mafunzo ya elimu maalum kwa watu wenye ulemavu, kuimarisha maslahi ya walimu pamoja na kuimarisha mazingira ya kusomesha yakiwemo kuwajengea uwezo, vifaa vya maabara na vitabu vya kiada na kadhalika. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ni jambo la kufurahisha sana kuona mafanikio makubwa sana ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba, imeweza kuyapata katika utekelezaji wa malengo hayo niliyoyabainisha ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2010 – 2015 pamoja na mipango mingine ya Kitaifa niliyoitaja hapo awali. (*Makofi*)

Wakati tukiwa katika mwaka huu wa tano kwa uongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba, tunafarijika kwa mafanikio ya kuandikisha watoto wote waliofikia umri wa kusoma. *(Makofi)*

Kubwa zaidi na la kupigiwa mfano, tumeondoa michango ya wazazi katika elimu ya msingi, na kuondoa gharama za mitihani yote ya elimu ya Sekondari kuanzia mwaka huu wa fedha 2015/2016, ili kuwawezesha watoto wetu wapate elimu bila ya malipo, kwa shabaha ile ile iliyotolewa na tamko la Mwasisi wetu wa Mapinduzi ya Zanzibar hayati Mzee Abeid Amani Karume, pale alipotangaza elimu bure tarehe 23 Septemba, 1964.

Tumeanza vizuri, hatua iliyobakia baadae kuondosha michango mpaka sekondari vile vile. Kwa hivyo, katika kipindi hiki cha miaka mitano, tunajivunia kuongezeka kwa uandikishaji wa wanafunzi katika ngazi ya elimu ya lazima; Maandalizi, Msingi na Sekondari, kutoka jumla ya wanafunzi 317,278 mwaka 2010 hadi kufikia wanafunzi 390,464 mwaka 2015. Haya ni mafanikio makubwa sana.*(Makofi)*

Mhe. Spika, Serikali imepiga hatua kubwa na ni hatua ya kupigiwa mfano katika utekelezaji wa Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima kwa kutumia fedha zetu na michango ya washirika wa maendeleo, kwa kujenga majengo mapya ya skuli, kununua vifaa vya maabara na samani. *(Makofi)*

Serikali imeweza kushirikiana vyema na wananchi pamoja na sekta binafsi katika kuongeza nafasi na fursa za kupata elimu kwa watoto wote wa Zanzibar, na kupanua wigo wa mafunzo yanayotolewa katika elimu ya juu hususan katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*). Kadhalika, Serikali iliendelea kuchukua hatua ya kuwapatia mikopo vijana wanaojiunga na taasisi za elimu ya juu kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, Idadi ya skuli zimeongezeka sasa. Skuli za maandalizi ziko 270 hivi sasa, kutoka 238 mwaka 2010. Skuli za msingi zimeongezeka kutoka 299 mwaka 2010 hadi skuli 370 sasa mwaka 2015. *(Makofi)*

Serikali pia imejiandaa kujenga skuli mpya za ghorofa, ili kuongeza nafasi kwa wanafunzi waliokosa nafasi. Ili kwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia sasa tunatekeleza ule mradi wa Tz – 21 unaohusiana na masomo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika skuli za msingi 248. Skuli hizi zimepatiwa vifaa mbali mbali ikiwa ni pamoja na Kompyuta, vitabu na vifaa vyengine vya ufundi wa TEHAMA pamoja na kuwapatia mafunzo watendaji wanaosimamia mradi huu.

Mhe. Spika, katika hotuba yangu ya uzinduzi wa Baraza hili, niliahidi kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha Elimu ya Sekondari kwa kuchukua hatua mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuyaimarisha mazingira ya ufundishaji na usomaji kwa kuwapatia walimu mafunzo, kujenga skuli mpya 21 ili kuongeza nafasi, kuzifanyia

matengenezo makubwa skuli sita za sekondari na kuzipatia vitabu na vifaa vya maabara skuli zetu pamoja na samani.*(Makofi)*

Kadhalika, kwa lengo la kuwashajihisha watoto wa kike kusoma masomo ya sayansi, niliahidi kuanzisha skuli maalum za sekondari kwa ajili ya watoto wa kike, na sasa mwaka wa pili Skuli ya Sekondari ya Ben Bella kwa Unguja na Skuli ya Utaani kwa Pemba tayari zimeshaanzishwa kwa lengo hilo. (*Makofi*)

Idadi ya Skuli za Sekondari kuanzia kidatu cha kwanza hadi cha sita imeongezeka, kutoka skuli 194 mwaka 2010 hadi skuli 263 mwaka huu 2015. *(Makofi)*

Serikali imeweza kukamilisha azma yake ya kuzifanyia matengenezo makubwa sana Skuli sita za zamani za Sekondari za Unguja na Pemba na kuzipatia vifaa vya maabara na samani kama ilivyoahidiwa. Skuli hizi mnazijua nyote, Tumekuja ipo Unguja, Forodhani na kwa Pemba Utaani, *Fidel Castro* na Uweleni, tumefanya kazi kubwa sana.

Aidha, tumekamilisha ujenzi wa Skuli mpya za Sekondari 19 kama tulivyoahidi katika Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na tayari skuli hizo zinatumika. Tuliahidi kuzijenga ndani ya miaka mitano, yaani mwaka huu Oktoba ndio tumalize, sisi tumemaliza mwaka wa kwanza kwa utekelezaji wake. (*Makofi*)

Serikali imechukua jitihada maalum katika kuhakikisha watoto wenye mahitaji maalum wanapata haki yao ya elimu katika skuli zetu mbali mbali, kupitia mpango wa elimu mjumuisho, pamoja na kuyaimarisha mafunzo ya elimu ya amali na ufundi katika vituo vya Mwanakwerekwe, Mkokotoni na Vitongoji.

Vituo hivi vimetoa mchango mkubwa sana wa kuwapatia vijana wetu mafunzo mbali mbali ya fani za ufundi zikiwemo fundi uashi, seremala, ushoni, uhunzi, upishi, uchoraji, ufundi bomba (ufundi mchundo), ufundi umeme, magari, mafriji, teknolojia ya habari na fani nyenginezo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mafanikio makubwa sana yamepatikana katika kuimarisha fursa za elimu ya juu hapa nchini ili kwenda sambamba na mahitaji ya wataalamu wetu wenyewe. Wanafunzi waliojiunga katika vyuo vikuu vitatu vya Zanzibar; imeongezeka kutoka vijana 3,624 mwaka 2010 na kufikia 6,367 mwaka 2015. Mafanikio hayo ni pamoja na ongezeko la masomo katika viwango mbali mbali kuanzia Ngazi ya Cheti hadi Shahada ya Uzamivu (*PhD*).

Katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) katika kipindi hiki, idadi ya skuli za masomo (*Schools*) imeongezeka kutoka moja hadi tano.

Kadhalika, chuo hiki tayari kimeanza benchi ya pili ya Shahada ya Uzamivu ya Kiswahili pamoja na kuanzisha kitivo cha masomo ya udaktari (*Faculty of Medicine*) katika mwaka 2013. Jambo kubwa zaidi ni ongezeko la wasichana katika masomo ya juu.*(Makofi)*

Katika Mahafali ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) mwaka 2014, idadi ya wahitimu wa kike ilikuwa ni asilimia 64 kati ya wahitimu 741 wa chuo hicho. Mwaka huu wa 2015 chuo kina wanafunzi 2705 ambapo 1654 ni wanawake na 1051 ni wanaume. Haya ndio maendeleo ya elimu ya Zanzibar, na haya ni miongoni mwa mafanikio ambayo nchi yetu inapaswa kuyaendeleza. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa lengo la kuhakikisha wanafunzi wanapata fursa ya elimu ya juu, wanaendelea na masomo yao, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatoa mikopo kila mwaka kwa wanafunzi wapya na wale wanaoendelea. Hadi kufikia mwezi Disemba, 2014 wanafunzi 4,678 walipewa mikopo yenye thamani ya TZS bilioni 19.4.*(Makofi)*

Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Serikali ilipanga kutoa udhamini kwa wanafunzi wapya wa elimu ya juu 1,200. Hata hivyo, idadi halisi iliongezeka hadi kufikia wanafunzi 1,611 sawa na ongezeko la asilimia 34 ya malengo. (*Makofi*)

AFYA:

Mhe. Spika, kwa lengo la kuhakikisha tunaimarisha huduma za afya nchini, na kwamba ni miongoni mwa vipaumbele vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba na shabaha ya Mapinduzi ya mwaka 1964. Miongoni mwa jukumu la msingi la Serikali lilikuwa ni kuyaendeleza mafanikio ya Sekta ya Afya ya awamu zote zilizotangulia katika kutekeleza mikakati ya mipango ya Kitaifa kupitia Ilani ya Uchaguzi ya CCM, MKUZA II, Dira ya Maendeleo ya 2020, pamoja na Malengo ya Milenia pamoja na kuhakikisha Sera ya Afya inatekelezwa kwa vitendo kwa kushirikiana na wananchi.

Miongoni mwa malengo makuu ya Serikali yalikuwa ni kuimarisha huduma za Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja ili ifikie kuwa Hospitali ya Rufaa.*(Makofi)*

Kadhalika tulikusudia kuiimarisha Hospitali ya Abdalla Mzee na Hospitali ya Wete ili zifikie hadhi ya kuwa Hospitali za Mkoa. Kwa upande wa Hospitali ya "*Cottage*" ya Kivunge na Makunduchi kwa Unguja na Micheweni na Vitongoji kwa Pemba nazo tuliamua zifikie kiwango cha hospitali za Wilaya.

Nina furaha sana kusema kwamba Hospitali ya *Cottage* ya Makunduchi imepiga hatua kubwa sana mbele zaidi, hivi sasa kwa utoaji wa huduma sio majengo, kwa

utoaji huduma hospitali ya *Cottage* ya Makunduchi imefika kiwango cha hospitali ya Wilaya. Watu wengi hata wa Mjini wanakwenda Makunduchi kutafuta huduma. *(Makofi)*

Malengo mengine ilikuwa ni kuanzisha Vitengo vya matatizo ya maradhi ya Figo niliahidi hapa hapa, Maradhi ya Moyo na utibabu wa maradhi ya Saratani, ili huduma hizi nazo ziweze kupatikana hapa nchini pamoja na kuziimarisha huduma za kinga na tiba.

Mhe. Spika, mabadiliko makubwa sana yamefanyika katika kipindi cha miaka mitano katika kuimarisha mazingira na huduma zinazotolewa katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja ili ifikie hadhi ya Hospitali ya Rufaa.

Hatua zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na kuipatia vifaa vya kisasa hospitali hii. Katika Chumba cha Upasuaji kuna mabadiliko makubwa sana, Maabara Kuu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ya uchunguzi wa maradhi, mimi mwenyewe nilipokwenda kutembelea nimeshangaa, nilidhani niko Ulaya, Wodi ya Wagonjwa Mahututi imejengwa mpya, na imezinduliwa juzi katika Sherehe za Mapinduzi ina hadhi ya Kimataifa, Wodi ya Wazazi na Chumba cha Wagonjwa wa dharura nazo zimeimarishwa kadhalika. *(Makofi)*

Jengo jipya tumelifungua lenye huduma mpya za kisasa; nazo ni upasuaji wa kichwa na uti wa mgongo. Jengo hili na vifaa vyake vilivyomo ni la pekee katika ukanda wa Afrika ya Mashariki na Kati. Katika hospitali nyengine za Afrika Mashariki zinatoa huduma kama hizo za *neurostadium* lakini sio kama ambazo zinatoka pale Mnazi Mmoja Hospitali sasa hivi.Wanakuja mabingwa wakubwa pale kutoka Spain wanafanya kazi kubwa na washafanya operesheni zaidi ya 1,000; pamoja na kupasua kichwa na uti wa mgongo ambazo miaka ya nyuma ilikuwa hazifanyiki pale Mnazi Mmoja Hospitali.

Tumeanzisha kituo kipya sana kinaitwa Kituo cha Meno cha Tabasam kwa ajili ya kuwahudumia watu wenye matatizo ya midomo. Wapo watu wanazaliwa kwa bahati mbaya wana-*clay palle* (mdomo upo nje) na meno yanachungulia, wanafanyiwa marekebisho pale pale Mnazi Mmoja Hospitali na wale ambao uso wao una matatizo wanarekebishwa pale pale. Hicho ndio kitengo cha meno cha Tabasam.

Kadhalika serikali imeanzisha Kitengo cha Uchunguzi wa Maradhi ya Mfumo wa Chakula kwa kuchunguza pale pale, kabla tulikuwa hata chombo kile cha *endoscopy* hatuna. Sasa kipo kipya na cha kisasa na Wodi mpya ya Wagonjwa Mahututi tumeanzisha. Hivi sasa, serikali inaendelea na mradi wa ujenzi wa jengo

jipya la watoto nyote mnaliona mkipita barabarani lipo mkabala na kiwanda cha madawa cha zamani.

Jengo lile litakuwa na huduma za watoto pamoja na huduma maalum za maradhi ya figo. Watakaohitaji kusafishwa figo zao (*dialysis*) tayari tuna mashine karibu nane kwa wakati mmoja watahudumiwa wagonjwa wanane hata Bara huduma hizo hazijafika wagonjwa wanane, wengine wanne, wengine sita. Mwenyezi Mungu ajaalie jengo limalizike kujengwa huduma hizi zianze mana vifaa vyote vipo tayari.

Kwa hivyo, ni jambo lililo wazi kwamba huduma katika Hospitali ya Mnazi Mmoja zimeimarika sana na zimepunguza kwa kiasi kikubwa idadi ya wagonjwa ambao walikuwa wakifuata huduma hizi baadhi yao nchi za nje. Tumejiandaa tunafundisha wanafunzi wetu wawili wa kidaktari katika taaluma ya elimu ya udhamili (*Master of Medicine*) kuhudumia wagonjwa wa kensa, mmoja anasoma Muhimbili mwengine anasoma nje, wakirudi hawa mambo tayari. Dawa za kutibiwa kensa tumeziagiza hata mwaka huu wa fedha pesa za kutosha mumezipanga wenyewe na mumeziidhinisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, serikali inaendelea na ujenzi mkubwa wa Hospitali ya Abdalla Mzee kwa kuiwekea miundo mbinu ya kisasa na lazima niwapongeze sana ndugu zetu wa Jamhuri ya Watu wa China. Nilipozungumza na Balozi wa China mwaka 2011 kama utani nikamwambia Balozi Hospitali ya Mkoani mumeijenga nyinyi hebu tuifanyie matengenezo iwe mpya. Akanambia Mhe. Rais nimekusikia nitapeleka taarifa nyumbani, kufumba na kufumbua ikaja timu kubwa sana ya wataalamu kutoka Nanjing, China na wamesema ombi limekubaliwa tutaanza kujenga andika rasmi. Ndipo alipokuja Rais Xi Jinping nikazungumza naye katika miradi mitano niliyompa mmoja Abdalla Mzee Hospital, nendeni mkatembelee Mkoani muangalie mambo yanavyokwenda pale. *(Makofi)*

Katika Hospitali ya Wete, tumefanya jitihada ya kuimarisha huduma, tumejenga shughuli za uchunguzi wa maradhi mbali mbali, ujenzi wa jengo la maabara mpya umekamilika. Wodi mpya ya wazazi, wodi ya wagonjwa wa akili na chumba cha upasuaji zimejengwa. Kwa hivyo, na hayo Hospitali ya Wete inaelekea kwa huduma kuwa Hospitali ya Mkoa, hatujakamilisha baadhi ya mambo tutakamilisha kipindi kijacho Mwenyezi Mungu akitujaalia.

Mhe. Spika, mwamko wa wananchi juu ya elimu ya afya na jitihada za serikali katika kuimarisha huduma hizo kumechangia sana katika kuongezeka kwa asilimia ya mama waja wazito wanaojifungua katika vituo vya afya hadi kufikia asilimia 68.3 mwaka 2014. Hivi sasa huduma za kujifungua zinapatikana bure katika vituo 41 nchini. *(Makofi)*

Vifo vya watoto wanaozaliwa hai chini ya umri wa mwaka mmoja vimepungua kutoka 54/1000 mwaka 2010 hadi 46/1000 mwaka 2012 zaidi ya lengo tulililoliweka la vifo 48/1000. Vile vile kuna mafanikio katika kupunguza vifo kwa watoto chini ya umri wa miaka 5 kutoka 73/1000 mwaka 2010, 66/1000 mwaka 2012. Lengo ni kufikia 50/1000. Kwa upande wa kinamama tumepunguza sana vifo vyao, taarifa hizi zitatoka baadae.

Kadhalika, serikali imeendelea kudhibiti kiwango cha Malaria na *VVU*/UKIMWI kuwa chini ya asilimia moja, kwa hakika malengo chini ya asilimia 5. Kwa mujibu wa tathmini ya kiwango cha maambukizo ya *VVU*, Zanzibar inakisiwa kuwa na asilimia 0.5 ya maambukizi kwa watu wenye umri kati ya miaka 15 hadi 24, asilimia 0.6 kwa wenye umri kati ya miaka 15 hadi 49.

Katika kipindi hiki serikali imejenga ghala la kisasa la kuhifadhia dawa katika eneo la Maruhubi. Serikali za Marekani na Denmark zimesaidia ujenzi huu na sisi wenyewe tumechangia vile vile. Hili ni ghala la tatu duniani kwa uwezo na teknolojia ya kuhifadhi dawa. La kwanza liko Marekani, la pili liko Afrika ya Kusini; hili la Zanzibar ni la tatu. Sio kwa jengo, sio kwa chochote kwa uwezo wa namna ya kuhifadhi dawa, miundombinu yake, teknolojia mule ndani ya *computerize* na mambo mengine ni ya hali ya juu sana, wenyewe waliojenga ndio wametwambia siku ya uzinduzi Balozi wa Marekani aliyemaliza muda wake waliyeondoka. Katika kipindi hiki serikali ilivyojenga ghala hilo lakini vile vile imeimarisha kuwa bora zaidi Ofisi ya Mkemia Mkuu wa serikali. Jitihada zinaendelea za kujenga majengo ya kisasa hapo hapo Maruhubi.

Jitihada kubwa zimefanywa katika kukiimarisha Chuo cha Taaluma ya Sayansi za Afya, Mbweni. Mafanikio yamepatikana ambapo kwa sasa idadi ya madaktari wazalendo imefikia 102. Sizungumzii madaktari wasaidizi wala wasaidizi madaktari, nazungumzia madaktari kamili, 102. Tunategemea idadi hiyo itaongezeka hasa baada ya serikali kuamua kuanzisha mafunzo ya udaktari katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) ambapo sasa wapo wanafunzi si chini ya sita mwaka wa kwanza na wa pili. Kwa wastani kwa idadi hiyo ya madaktari walioko Zanzibar sasa, daktari mmoja alikuwa akihudumia wagonjwa 31,838 (1:31,838) mwaka 2010 na ambapo sasa anahudumia wastani wa wagonjwa 9,093 (1:9,093).

Pamoja na madaktari wazalendo, wapo madaktari wa kigeni 20 kutoka China na 20 kutoka Cuba. Idadi hii ndio inafanya kiwango chetu cha daktari mmoja kuhudumia watu wachache sana kiwe Zanzibar kiwango ambacho hakijafikiwa na nchi za Afrika Mashariki na Kati. *(Makofi)*

Napenda nitoe shukurani zangu kwa washirika wetu wa maendeleo wanaotuunga mkono katika azma yetu ya kuziimarisha huduma za afya nchini. Tunathamini sana misaada yao ya mafunzo na utaalamu, vifaa, wafanyakazi na nyenzo mbali mbali ambazo kwa pamoja zimeweza kutuletea mafanikio tuliyoyapata. Zanzibar ina mtandao mzuri wa huduma za afya zinazotolewa katika hospitali na vituo vya afya vya serikali, pamoja na Vikosi vya Ulinzi, Taasisi za Kijamii na vituo vya watu binafsi kuliko nchi nyingi.

Katika Bara la Afrika; Zanzibar ni nchi ya kupigiwa mfano, mwananchi wa Zanzibar hatembei kilomita tano bila ya kupata huduma za afya nchi nyegine haiko hivyo wengine huenda mpaka kilomita 20 au 25 hakuna vitu hivyo sisi kwetu kilomita tano kituo cha afya unakutana nacho ni mafanikio makubwa. *(Makofi)*

MAJI SAFI NA SALAMA

Wakati nikilifungua Baraza hili, nilisema kuwa maji ni uhai na hasa maji safi na salama. Kwa hivyo, serikali yangu imeendeleza jitihada za Serikali za Awamu zilizopita na kuweka mikakati mipya katika kuwapatia wananchi huduma za maji safi na salama. Mipango ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba, ni pamoja na kukamilisha mradi wa usambazaji wa maji katika mikoa yote na hasa Mkoa wa Mjini Magharibi, kupunguza upotevu wa maji na kuvihifadhi vianzio vya maji.

Katika ahadi zangu nilizozitoa nilibainisha kuwa kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 – 2015, serikali inakusudia kusambaza huduma za maji safi na salama kufikia asilimia 95 katika miji kutoka asilimia 75 katika miji na asilimia 80 katika vijiji kutoka asilimia 60 katika mwaka 2015. Hali ya uzalishaji wa maji imefikia lita milioni 17.6 ambayo imewezesha kuongezeka kwa watu wanaopata maji na kufikia 175,873 katika kipindi hiki kifupi.

Mahitaji yetu halisi ya maji ni lita milioni 214.6 ambapo uzalishaji katika kipindi hiki umefikia lita milioni 163 sawa na asilimia 76 ya mahitaji. Kiwango chetu kimeongezeka. Kutokana na takwimu hizi upatikanaji wa maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi umefikia asilimia 87.7, Mkoa wa Kusini Unguja asilimia 76.45, Mkoa wa Kaskazini Unguja asilimia 71.68, Mkoa wa Kusini Pemba asilimia 74.08 na Mkoa wa Kaskazini Pemba asilimia 56.42 ya mahitaji halisi. Tuna kazi ya kufanya ili tufikie lengo la ilani yetu, hatuko mbali na hapo. *(Makofi)*

ARDHI NA MAKAAZI

Serikali iliahidi kushughulikia suala la matumizi bora ya ardhi kwa kuzingatia udogo wa ardhi tuliyonayo. Katika utekelezaji wa azma hii, serikali imetayarisha

sera mpya ya ardhi ili kusimamia na kutekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi. Sera hiyo pamoja na mambo mengine imezingatia mabadiliko ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi yaliyopo na yatakayokuja baadae. *(Makofi)*

Kazi ya usajili wa ardhi imeshafanywa vizuri na zaidi ya shehia 20 na zoezi la utambuzi linaendelea katika shehia 13. Jumla ya nyumba, viwanja na mashamba 22,398 vimeshatambuliwa sambamba na hatua hiyo, zoezi la utoaji wa Hati za matumizi ya Ardhi linaendelea kwa kutoa hati mpya na kuzibadilisha zile za zamani. Hadi sasa jumla ya mikataba ya matumizi ya ardhi 223 imeshasainiwa na kukabidhiwa wawekezaji. Vile vile, hati 1,310 za matumizi mbali mbali ya ardhi zimetolewa na viwanja 1,691 vimepimwa, Unguja na Pemba.

Katika kukabiliana na tatizo la matumizi mabaya ya ardhi, serikali imeshakamilisha mpango mkuu wa matumizi ya Ardhi ya Mji wa Zanzibar na Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Ardhi Zanzibar, sambamba na mipango ya matumizi ya ardhi ya Mikoa yote ya Zanzibar. Katika kuhakikisha uhifadhi wa Mji Mkongwe wa Zanzibar, serikali imeanzisha mfumo mpya kwa njia ya kuishirikisha Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*PPP*) kwa ajili ya kuhifadhi nyumba ziliopo Mji Mkongwe. Mfumo huo utafanywa kupitia Kampuni itakayoitwa Hifadhi ya Zanzibar na tayari imeshasajiliwa na kuanza kazi zake.

Aidha, serikali inaendelea na matayarisho ya kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Miji ili kusimamia ustawi wa maendeleo ya miji yetu.

Nina matumaini makubwa kuwa kupitia mipango hiyo, wananchi wataelimika na watazidi kuifahamu mipango ya matumizi bora ya ardhi na utaratibu huu utapunguza changamoto zilizopo hivi sasa. Nawasihi sana wananchi waendelee kushirikiana na serikali katika utekelezaji wa mipango hii ili tuweze kufikia azma yetu ya matumizi bora ya ardhi. *(Makofi)*

HABARI NA MAWASILIANO

Kwa upande wa habari; katika kipindi cha miaka mitano, serikali imeimarisha utoaji wa habari kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kurusha moja kwa moja matangazo yanayohusu vikao vya Baraza la Wawakilishi. Tumeliwezesha Shirika la Utangazaji la Zanzibar (*ZBC*) kufanya mageuzi ya kutoka mfumo wa "*Analogue*" kwenda "*Digital*" kwa mafanikio na kwa wakati tuliopangiwa na Jumuiya za Kimataifa. Tumeongeza muda wa kutangaza, ambapo hivi sasa *ZBC* Radio na TV zinakuwa hewani kwa saa 24. Vile vile, gazeti la Zanzibar Leo linalotolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ubora wake wa habari na uchapishaji umeongezeka na hivi sasa linapatikana kila siku katika maeneo mbali mbali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, Zanzibar imepiga hatua kubwa kwa kuongeza idadi ya vyombo vya habari zikiwemo radio jamii 4 pamoja na vituo vya habari binafsi. Hali hii imechangia sana kuongezeka kwa uhuru wa kupata habari na kusukuma maendeleo ya jamii yetu katika nyanja mbali mbali.

Vile vile, serikali imetekeleza azma yake ya kuwajengea wasanii wetu "*Studio*" za kisasa za kurekodia nyimbo na michezo ya kuigiza kama nilivyoahidi katika Baraza hili. Tumelikarabati jengo la zamani lililokuwa la Sauti ya Tanzania Zanzibar, baada ya kufanyiwa matengenezo makubwa, tumetengeneza studio mpya mbili nzuri jengo lile mkienda ndani mtashangaa lilivyo. Wasanii wetu watapata nafasi ya kurekodi michezo yao.

Kwa lengo la kutekeleza azma ya serikali ya kukifufua Kiwanda cha Upigaji Chapa na Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ili kurudisha hadhi yake na kuinua kiwango cha uzalishaji. Jumla ya Shilingi milioni 5,532.40 zimetumika kwa matengenezo ya majengo yaliyokuwa kiwanda cha sigara Maruhubi pamoja na ununuzi wa mashine mpya za kisasa za uchapishaji za kiwanda hicho.

Serikali ina lengo la kuimarisha zaidi kazi za kiwanda hicho ili kiweze kuchapisha magazeti, vitabu vikubwa na kadhalika. Fedha kwa ajili ya kazi hio tayari zimepatikana kutokana na msaada wa Serikali ya Oman. Wametuletea fedha *cash* kwa cheki hivi karibuni sikumbuki vizuri sijui ni Dola, dola milioni sita na zaidi. Kwa hiyo tuna uwezo sasa wa kununua mitambo mipya kuchapisha vitabu, magazeti na kila kitu, hatutopeleka tena nyaraka zetu kwenye taasisi za nje. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ni dhahiri kukamilika kwa kiwanda hiki kumeipunguzia mzigo serikali na kitaiwezesha kutoa huduma zenye ubora wa kiwango kikubwa zaidi, sekta bunafsi itakuja kwetu sasa kuchapidha.

Mhe. spika, kwa lengo la kuziimarisha huduma za mawasiliano serikalini, katika kipindi hiki cha kwanza cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba, serikali imeanzisha mradi wa *"e-government"* ambao uliuzinduliwa mwezi wa Januari mwaka 2013. Hadi hivi sasa, jumla ya majengo 86 ya serikali yameunganishwa katika mtandao wa serikali (e-*government*) na tayari yameanza kupata huduma ya "*internet*" bila ya malipo.

Awamu ya kwanza ya mradi huu inaendelea vizuri na maandalizi ya awamu ya pili yamekamilika, ambapo huduma za "*e-health*" na nyengine zitaanzishwa. Hivi sasa serikali imo katika maandalizi ya kuiunganisha Zanzibar na Tanzania Bara kupitia mkonga wa Taifa na ule wa kimataifa (*ESSY*).

UTAMADUNI NA MICHEZO

Mhe. Spika, kwa lengo la kudumisha na kutangaza utamaduni wetu, silka na desturi zetu, serikali imefanikiwa kuandaa matamasha mbali mbali ambayo yamesaidia sana katika kuendeleza na kuhifadhi utamaduni wa mambo ya asili.

Kadhalika, kwa kushirikiana na wana michezo, Serikali imefanikiwa na juhudi zake za kufufua na kuimarisha michezo nchini. Ni jambo la kufurahisha sana kuona kuwa baadhi ya Wawakilishi katika Baraza hili tukufu wamekuwa mstari wa mbele katika jambo hili kwa kuanzisha timu na vikundi vya michezo na mazoezi katika Majimbo yao na kuzipatia timu hizo vifaa mbali mbali. (*Makofi*)

Mimi nataka nimpongeze sana Mhe. Mohammedraza Hassanali; amenialika mara mbili kwenye Jimbo lake kwenda kutoa vifaa vya michezo kwa wanamichezo wa Jimbo zima na mara ya pili alivyonialika nikamuomba aniwakilishe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais katoa vifaa kwa skuli zote za Jimbo lake vya Michezo. Huu ni mfano mzuri wa uongozi bora na mfano mzuri wa viongozi kuwatumikia waliowachagua. Naamini na nyie Waheshimiwa Wawakilishi wengine pia mmefanya mambo hayo, lakini hamkupata bahati ya kunialika. Lakini mngenialika ningekuja, lakini naamini wengine mmefanya kazi hiyo maana na mimi nasikiliza taarifa za habari na vyombo vyengine vya habari, hongereni sana nyote. (*Makofi*)

Serikali imeanzisha mashindano ya riadha ya Wilaya, hatukua na mashindano haya kabla Wilaya zote kumi za Zanzibar na timu za michezo mbali mbali, zimepatiwa vifaa. Viwanja vyetu vimeimarishwa na hivi sasa Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, tumeanza matengenezo katika uwanja wa Mao- Tse Tung. (*Makofi*)

Tuliwaomba na wametukubalia ombi letu kazi itaanza mwezi wa pili mwakani. Sasa matayarisho mnayaona pale mkipita na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alikwenda pale kwenda kuangalia kazi zinavyofanywa.

Mhe. Spika, ni jambo la kujivunia sana kuona kuwa, katika kipindi hiki cha kwanza cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, awamu ya saba, yenye muundo wa umoja wa kitaifa tumeweza kuvijenga upya viwanja viwili vikubwa na vya kisasa vya kufurahishia watoto; Kiwanja cha Kariakoo kwa Unguja na Kiwanja cha Tibirinzi kwa upande wa Pemba.

Kiwanja cha Kariakoo nilikifungua rasmi tarehe 8 Januari, katika shamra shamra za Miaka 51 ya Mapinduzi. Vile vile, Kiwanja cha Tibirinzi nacho tunaweza kukifungua wakati wowote kuanzia sasa. Tunategemea mipango ikienda vizuri mwezi ujao huenda kikatumika kwenye sikukuu ya Idd El-fitri. Viwanja hivi

vitawapa watoto wetu sehemu nzuri ya kwenda kucheza na kufurahia na kuwafanya wakue wakiwa na afya bora.

Mhe. Spika, Ujenzi wa Mnara wa Kumbukumbu ya Miaka 50 ya Mapinduzi ulioko Michenzani nao umo katika hatua za mwisho za kumalizika. Niliweka jiwe la Msingi la Ujenzi wa Mnara huu tarehe 11 Januari, 2014. Ni dhahiri kuwa kumalizika kwa Mnara huu kutaongeza idadi ya maeneo ya kutembelea na kupumzikia kwa wananchi wetu wa Zanzibar na hasa wageni watakaotutembelea watapata fursa ya kujifunza historia ya Mapinduzi yetu. Katika sehemu ya chini ya Mnara huu, kutakuwa na chumba maalum kinachotoa maelezo na maonyesho ya mambo ya Mapinduzi. Lengo letu watu wajifunze Mapinduzi yetu. (*Makofi*)

MAKUNDI MAALUM

Mhe. Spika, Mashirikiano na mshikamano tuliouonesha katika kipindi hiki cha miaka mitano katika Serikali yetu tumeweza kuinua hali na ustawi wa kina mama, vijana na watoto, na vile vile na wazee wetu katika sehemu zote za Unguja na Pemba. Serikali imeweza kuwahudumia na kuwatunza wazee kwa kuyaimarisha makaazi yao na kuwapatia huduma muhimu za kila siku za maisha yao, kwa kiwango cha kuridhisha.

Sheria Namba 6 ya Mwaka 2011 mlioyoipitisha hapa Barazani, imetupa mwongozo imara katika kuweka mazingira bora ya kupatikana haki muhimu za watoto wanaoishi na kukua katika mazingira mbali mbali. Mahakama ya watoto tuliyoifungua rasmi mwezi Februari mwaka 2013 inaendelea kuimarisha utoaji wa haki na kuongeza kasi katika uendeshaji wa kesi zinazohusu masuala ya watoto.

Pamoja na hatua hiyo, Serikali imefungua vituo vya kushughulikia waathirika wa vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia katika Hospitali zetu za Mnazi Mmoja, Kivunge, Makunduchi na Chake chake vikiwa na wataalamu wote wanaohusika katika kuchukua hatua hizo.

Mhe. Spika, katika kuifanikisha Kampeni ya udhalilishaji wa wanawake na watoto tuliyoizindua rasmi tarehe 6 Disemba, mwaka jana; mwamko uliopo katika majimbo yetu umezidi kuwa ni chachu ya mafanikio makubwa tunayoyashuhudia katika kampeni hii.

Katika juhudi zinazoendelea kuchukuliwa za kuimarisha maslahi ya wazee. Serikali imeamua kuanzisha malipo ya pencheni kwa wazee wote bila ya kujali waliofanya kazi Serikalini au waliokuwa hawajafanya kazi Serikali hii inaitwa kwa kizungu *Universal Pension*. Kwa kuanzia malipo haya yatatolewa kwa wazee

wenye umri wa miaka sabiini (70). Tathmini ya awali imebainisha kuwa jumla ya wazee 27,366 watafaidika na mpango huu kwa kulipwa kila mwezi.

Serikali tayari ishatenga Shilingi bilioni 1 na milioni 650 kwa ajili ya malipo hayo kwa muda wa miezi mitatu ya mwanzo kuanzia mwezi wa nne mwakani. Katika mpango huu, wazee wote wa Zanzibar waliofikia umri huu watafaidika kwa kupewa TZS 20,000 kila mwezi kama nilivyosema bila ya kujali historia ya kazi yake aliyokuwa akifanya kabla ya umri huo.

Imani yangu ni kuwa utaratibu huu mpya tuliounzisha utasaidia wazee wengi sana, wale walikuwa katika ajira zisizo za kiserikali, hasa wakulima, wavuvi, wajasiriamali na wengine ambao walikuwa wakijikuta hawana msaada wowote wakati wanapoacha kazi zao (wanapostaafu). Wale waliostaafu serikalini watapata pencheni yao na hii ya shilingi 20,000 itakuwa inaongezwa. Katika miaka ijayo tunatarajia kupunguza umri tutashuka miaka 70, tutakuja chini Mwenyezi Mungu akipenda. (*Makofi*)

Vile vile, katika kipindi hiki cha miaka mitano, Serikali imefanya jitihada mbali mbali ili kuwasaidia watu wenye ulemavu. Mfuko Maalum wa Watu Wenye Ulemavu umeanzishwa na niliuzindua mwaka 2012. Mfuko huu hivi sasa una jumla ya TZS milioni 167.6 ambazo zitatumika kwa mahitaji mbali mbali ya watu wenye ulemavu.

Vile vile, Usajili wa watu wenye ulemavu uliofanywa kwenye Wilaya zote za Unguja na Pemba na sasa umekamilika, na umesaidia sana kuwatambua ili kurahisisha upangaji na utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo.

Kadhalika, Serikali itaendelea kutoa ruzuku kwa Jumuiya za Watu wenye Ulemavu Unguja na Pemba ili ziweze kutimiza malengo yao.

DEMOKRASIA NA UTAWALA BORA

Mhe. Spika, Katika hotuba yangu ya uzinduzi wa Baraza hili la Nane niliahidi kuwa Serikali nitakayoiongoza itazingatia Utawala Bora wenye kuheshimu sheria na haki za binaadamu. Vile vile, nilieleza kwamba nitaongoza nchi kwa misingi ya Katiba na Sheria za Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nimefarajika kuona namna ambayo tumeweza kutekeleza dhamira hizo. Katika kipindi hiki cha kwanza cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba, tumeweza kutekeleza mipango mbali mbali kwa ajili ya kuimarisha Utawala Bora zikiwemo kuendelea kuunda Wizara ya Nchi inayosimamia masuala ya Utawala Bora.

Juhudi kubwa zilielekezwa katika kuhakikisha kuwepo kwa taasisi zilizo huru zinazoendeshwa kwa kuzingatia Katiba na Sheria zinatekeleza majukumu yake kwa uadilifu na mashirikiano.

Serikali imeunda Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi baada ya Baraza hili Tukufu kutunga Sheria Namba 1 ya uhujumu wa uchumi ya mwaka 2012. Vile vile, imeimarisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuiwezesha kujenga na kuifungua Ofisi hii nzito huko Pemba kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake vizuri.

Juhudi kubwa zimefanywa kuimarisha Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ikiwa ni pamoja na kuiongezea idadi ya wanasheria ili itekeleze majukumu yake kwa ufanisi.

Tume ya kupitia Sheria imeendelea na itaendelea na kazi zake za kushauri kuondosha zile zilizopitwa na wakati na kuzifanyia marekebisho zenye kuhitajika.

Kukamilika kwa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kufuatia mswada wa Sheria uliopitishwa, tarehe 30 Januari mwaka huu na Baraza hili ni hatua muhimu katika kuimarisha Utawala Bora na demokrasia nchini. Nina imani kwamba viongozi wote watatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria hii katika utendaji haki na utoaji wa huduma zilizo bora kwa wananchi.

Mhe. Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mageuzi kwenye mfumo wa kiutawala kwa kuzipa uwezo zaidi Serikali za Mitaa ikiwa ni hatua muhimu ya kuimarisha Utawala Bora. Serikali imeandaa Sera ya Serikali za Mitaa pamoja na Mpango wa Utekelezaji. Natoa shukurani kwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu Mhe. Spika, kwa michango mbali mbali iliyowezesha kuifanyia marekebisho kwa Sheria Namba 3 na 4 ya mwaka 1995 na Sheria Namba 1 ya mwaka 1998 hadi ikatungwa Sheria mpya ya Tawala za Mikoa na Sheria mpya ya Serikali za Mitaa za mwaka 2014.

Aidha, natoa shukurani kwa wananchi kwa kutuunga mkono katika utekelezaji wa mageuzi haya.

Ni dhahiri kuwa mafunzo yaliyotolewa kupitia semina maalum kwa viongozi wa ngazi mbali mbali yalikuwa ni chachu ya kuwapa maarifa mapya na kuongeza uzoefu wenu na hatimae yaliwezesha kutekeleza majukumu yenu kwa ufanisi zaidi. Utaratibu tulioanzisha wa kuziita Ikulu Wizara zote za Serikali kuja kuwasilisha tararifa za utelezaji kwa Mipango Kazi maarufu kuwa Bango Kitita kila baada ya robo mwaka, umetuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa uwazi

na kuimarisha uwajibikaji, kuimarisha mashirikiano na mahusiano baina ya Idara mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Kadhalika, utaratibu huu umetusaidia kupunguza muingiliano wa majukumu baina ya Wizara moja na Wizara nyengine. Aidha, mpango huu umepanua upeo na maarifa katika kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo kwa mujibu wa vipaumbele na upatikanaji wa rasilimali fedha na watu. Haya yote ni mafanikio tuliyoyapata katika kuleta uwazi na uwajibikaji ambayo ni mambo ya msingi katika Mfumo wa Serikali ninayoiongoza.

Mhe. Spika, katika kipindi cha miaka mitano, Serikali imechukua hatua mbali mbali za kuimarisha manispaa ya Zanzibar pamoja na miji ya Chake Chake, Wete na Mkoani, Serikali ilianzisha Mradi wa Huduma za Jamii yaani *ZUSP* mwaka 2011. Ili kuimarisha upatikanaji wa huduma muhimu katika miji hiyo, kuimarisha haiba, mazingira pamoja na kuhifadhi eneo la urithi wa Mji Mkongwe.

SEKTA YA SHERIA

Mhe. Spika, Katika kipindi cha miaka mitano hii, Serikali imechukua hatua kadhaa za kuimarisha mazingira ya utendaji kazi katika Mahkama kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kazi zake, kupunguza mrundikano wa kesi na kuimarisha maslahi ya wafanyakazi. Serikali imeyafanyia matengenezo makubwa majengo ya mahkama likiwemo jengo la kihistoria la Mahkama Kuu Vuga na Mahkama nyengine nchini.

Kwa upande wa majaji, Serikali imefanikiwa kuongeza idadi yao kutoka wawili mwaka 2011 hadi sita kati ya Majaji hao sita wawili ni wanawake. Hili ni ongezeko la Majaji la asilimia 200 toka mwaka 2010 hadi mwaka huu.

Kwa upande wa Mahakimu wa ngazi mbali mbali, Serikali imefanikwa kuongeza idadi yao kutoka Mahakimu 43 mwaka 2010 hadi 85 mwaka 2015. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 97.7.

Kadhalika, Serikali imeiongeza Bajeti ya Mahakama kutoka TZS bilioni 1.3 mwaka 2010/2011 hadi TZS bilioni 5 mwaka 2013/2014. Hili ni ongezeko sawa na asilimia 284.6. (*Makofi*)

Mhe. Spika, wakati huo huo, katika kipindi hicho cha miaka mitano, Afisi ya Mufti wa Zanzibar imeendelea kuratibu na kusimamia majukumu yake ya kisheria. Katika kipindi cha miaka mitano, watendaji wa Afisi ya Mufti wametembelea Madrasa za Qur-ani 164 na Misikiti 166 na kutoa ushauri juu ya maendeleo ya taasisi hizo.

Aidha, Madrasa 500 za taasisi za kidini 73 zimepatiwa usajili pamoja na kurushwa hewani kwa vipindi 124 vya nasaha na mawaidha ya mafundisho ya kiislamu kupitia Radio ya *ZBC*.

Vile vile, Afisi ya Mufti imeshughulikia na kutatua migogoro mbali mbali pamoja na kuhamasisha amani na utulivu.

Kadhalika, Serikali imefanya jitihada mbali mbali katika kipindi hiki cha miaka mitano ya kuziimarisha Mahakama za Kadhi, ili kuendesha shughuli zake kwa ufanisi na haraka sana. Jitihada hizo ni pamoja na kuongeza idadi ya makadhi kutoka 12 hadi 15 na kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi kwa kuyafanyia matengenezo makubwa majengo ya Ofisi za Mahakama na kuzipatia vifaa na samani. Hatua hizo zimechangia sana katika kuongeza ufanisi na kupunguza malalamiko ya wananchi kuchelewa kufanyiwa kazi mashauri yao.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, imefanya jitihada kubwa ya kuiimarisha Mahkama ya Ardhi ili kuiongezea uwezo wa kutatua migogoro ya ardhi. Idadi ya Mahakimu katika Mahkama hiyo nayo imeongezwa kutoka Mahakimu wawili hadi wanane katika kipindi hiki cha awamu ya saba.

Hatua hiyo imeiwezesha Mahkama kupunguza mrundikano wa kesi za migogoro ya ardhi kutoka 800 hadi sasa 200. Mazingira ya kufanyia kazi yameimarishwa ambapo Mahkama hiyo inatumia jengo lilioko mjini na Koani Unguja na kwa upande wa Pemba ipo Mahkama ya Wete na Chake Chake. Hivi sasa mashauri ya migogoro ya ardhi yanafanyika kwa haraka zaidi ikilinganishwa na miaka iliyopita jambo ambalo limepunguza kwa kiasi kikubwa malalamiko ya wananchi.

Katika kipindi hiki cha miaka mitano, Serikali imefanya jitihada za makusudi za kuimarisha Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa lengo la kuongeza uwajibikaji na umahiri wa kisheria katika usimamizi wa mashtaka. Idadi ya Wanasheria wa Serikali imeongezwa kutoka 28 waliokuwepo mwaka 2010 hadi kufikia 50 mwaka huu. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 78.5.

Ongezeko hilo limeiwezesha Ofisi ya *DPP* kuendeleza mashtaka ya kiraia kwa kuwatumia Wanasheria badala ya Polisi katika Mahkama za Mikoa yote na Wilaya zote za Unguja na Pemba. Wilaya nne zilizobakia zinatarajiwa kuwa na utaratibu huu wakati zile sita zimeingia katika mfumo mpya katika utekelezaji wa mipango iliyobainishwa katika bajeti mliyoipitisha hivi karibuni ya 2015/2016. Tunatarajia utekelezaji uwe mzuri zaidi. Nina imani kuwa hatua hiyo iliyofikiwa itazidisha imani ya wananchi kwa Mahkama zetu na hukumu zinazotolewa.

BARAZA LA WAWAKILISHI

Mhe. Spika, Natoa shukurani kwa mara nyengine kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Nane kwa kuendelea kuweka misingi bora ya Utawala Bora na demokrasia. Kwa hakika mmeweza kutekeleza vyema wajibu wenu wa kikatiba wa kutunga sheria na kuisimamia serikali kama ilivyoanishwa katika kifungu cha 5A(1) na kufafanuliwa kifungu 5A(2) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984.

Katika kipindi cha miaka mitano, mmefanya majukumu yenu kwa kufanya mikutano yenu katika hali ya salama na utulivu. Licha ya kutofautiana kwa hoja na mitazamo kwa baadhi ya masuala muhimu, mmeweza kupitisha miswada ya sheria 63 na baadae iliwasilishwa kwa Rais kwa ajili ya kutia saini na sasa zimekuwa sheria kamili. (*Makofi*)

Takwimu zinaonesha kuwa katika kipindi hiki cha miaka mitano hiki maswali 1558 ya msingi na maswala ya nyongeza 3103 yameulizwa kwa Serikali na yalipatiwa majibu sahihi. Ninawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri kwa kutekeleza agizo langu nililowataka wajibu maswali vizuri, niliwaambia wajibu wasibabaishe na wajibu bila ya hofu. Kamati teule 5 mlizoziunda nazo zimetekeleza majukumu yake kwa uadilifu na umakini mkubwa. Nawapongeza wajumbe wote wa kamati teule hizo kwa kufuatilia na kuibua masuala juu mambo mbali na kuyaleta Barazani kwa kujadiliwa na baadae kuishauri Serikali juu ya mambo yanayoibuka.

Aidha, nalipongeza Baraza kwa kupokea na kujadili hoja binafsi zinazowasilishwa.(*Makofi*)

Mhe. Spika, Baraza hili la Nane limeingia katika historia ya nchi yetu, na litakumbukwa kwa kipindi kirefu sana kijacho katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushiriki katika Bunge Maalum la Katiba kwa lengo la kuunda na kutengeneza Katiba Inayopendekezwa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napenda nikushukuruni nyote Waheshimiwa Wajumbe kwa ushiriki wenu huo uliotuwezesha kupata Katiba Inayopendekezwa ambayo hivi sasa wananchi wanaisubiri kwa hamu kuipigia kura ya maoni.(*Makofi*)

Leo ni siku ya furaha kwa upande mmoja na siku ya huzuni kwa upande mwengine. Nasema hivi kwasababu leo baadae tutalivunja Baraza hili, tutalivunja kwa mbwembwe na madaha kutokana na mafanikio makubwa tuliyoyapata katika kuiendeleza nchi yetu. Lakini leo ni siku ya huzuni kwa sababu tunaagana na nitalivunja rasmi Baraza hili la Nane na huenda ikapita kipindi bila ya baadhi yetu kuonana ingawa tunategemeana kwa kiasi kikubwa tunaonana baadae.(*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa wale wenye dhamira ya kurejea majimboni kwa ajili ya kutafuta ridhaa ya wananchi kwa mara nyengine, nawatakia mafanikio ili warudi tena kwa miaka mitano ijayo. Kwa wale ambao wamefikia uamuzi ya kutogombea tena, nawasihi waendelee kutumia maarifa na uzoefu walioupata katika Baraza hili katika kuongoza, kuhamasisha na kushiriki kikamilifu katika harakati za maendeleo ya nchi yetu. Nyote mtabaki kuwa hazina kubwa katika kupanga na kutekeleza mipango ya nchi hii. (*Makofi*)

Hata hivyo, kwa wale mtakaojaaliwa kuchaguliwa tena na wananchi na kurudi Barazani, nataka nikunasihini na nikukumbusheni kuwa mnapokuwa kwenye Baraza hili muendelee kuzingatia, kutii na kutekeleza kwa vitendo Katiba ya Zanzibar, sheria ziliopo na kanuni za Baraza hili. Baraza la Wawakilishi ni muhimili uliowekwa ndani ya Katiba.

Hiki ni chombo kikubwa kinachoendeshwa kwa misingi ya Utawala Bora. Hakiendeshwi kwa kuendesha migomo au njia nyengine yoyote ya ubabe. Baraza ni chombo cha wananchi wa Zanzibar.

Kwa hivyo, suala lolote lenye maslahi ya wananchi wa Zanzibar, hapa ndipo pahala pa kisheria pakulizungumza jambo hilo, lisizungumzwe kupitia mgomo. Kutoka nje ya Baraza si ufumbuzi wa tatizo linalohusu hoja inayojadiliwa Barazani au hoja nyengine iliyokuwa haijadiliwi na Baraza hili.

Waheshimiwa Wajumbe nyinyi ndio mnaotunga sheria za nchi hii, kwa hivyo nakunasihini sana msichanganye mambo. Kila sheria iliyotungwa na Baraza hili matumizi yake yako wazi kwa kupitia taasisi iliyowekwa. Nyinyi ni Waheshimiwa na wananchi na jamii kwa jumla wanakuheshimuni na vile vile wanaliheshimu Baraza hili. Ni matarajio yangu kwamba nanyi Waheshimiwa mtairejesha heshima hiyo kwa wananchi kwa kuwatimizia matarajio yao ili tupate maendeleo zaidi.(*Makofi*)

Mhe. Spika, kila mmoja wetu anaelewa kwamba Baraza hili linaendeshwa kwa misingi ya Sheria na Kanuni. Hoja zinazotolewa na kujadiliwa na Baraza hili zinaendeshwa kwa misingi hiyo. Wakati Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa chama cha CUF waliposusia kikao cha tarehe 23 Juni, 2015 hivi juzi, hoja walizozitoa hazikuwa na mnasaba na hoja iliyokuwa imewasilishwa Barazani, Baraza halikujadili hoja yao. Siku hiyo Waziri wa Fedha alikuwa amewasilisha hoja ya kujadiliwa kwa Mswada wa Sheria ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ambao haukuwa na uhusiano wowote hata kidogo na masuala ya kujiandikisha katika daftari la kudumu la kupiga kura.

Hoja yao ilikuwa inahusiana na sheria nyengine, Sheria ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Nam. 9 ya mwaka 1992 inayosimamiwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar pamoja na Sheria ya Usajili wa Mzanzibari Mkaazi, Nam. 7 ya mwaka 2005. Waheshimiwa Wajumbe, musichanganye mambo.(*Makofi*)

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe uamuzi wao wa kutoka nje ya Baraza haukuzingatia uamuzi wetu wa kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Uamuzi wao wa kutoka nje haukuzingatia mapenzi tuliyoyajenga baina yetu. Uamuzi wao wa kutoka nje haukuzingatia sifa tulizozipata Zanzibar kutoka katika Jumuiya za Kimataifa kwa kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Uamuzi wao wa kutoka nje haukuzingatia maslahi ya Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe tuwaulizeni wenzetu wa CUF ambao tuliamua kwa pamoja kuianzisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa mujibu wa Katiba na Sheria za Zanzibar, tuwaulize kutoka hapa sasa tulipofika tunakwenda wapi. Hatimaye Serikali ya Umoja wa Kitaifa ikoje sasa. Wananchi wa Zanzibar wana hatma gani ya nchi yao sasa, waulizeni maendeleo tuliyoyapata miaka mitano hatma yake yakoje. Tuwaache wananchi waamue na wananchi wataamua tarehe 25 Oktoba, mwaka huu (2015), wataamua kuhusu hatma yao na maendeleo yao ya Zanzibar, watafanya uchaguzi sahihi, watachagua viongozi wanaoweza kuongoza. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wawakilishi, muliobakia humu wa Chama cha Mapinduzi ninataka nikupongezeni sana, mumewakilisha vizuri sana wananchi wa Zanzibar, mumefanya kazi kubwa sana ya kupitisha bajeti, mumedhihirisha ule usemi wetu "zege hailali". Mswada wa Sheria ya *Appropriation Bills* mumeupitisha kwa mapenzi makubwa na mbwembwe kubwa sana, tutawahudumia wananchi wa Zanzibar bila ya matatizo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kuhakikisha kila mwananchi mwenye sifa ya kupiga kura anapewa haki yake hiyo. Ninawanasihi sana na ninawataka sana Wanasiasa wasipotoshe wananchi juu ya haki hiyo. Nawanasihi viongozi wote wa siasa waiache Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ifanye kazi yake ikiwa huru na isiingiliwe kwa namna yoyote ile. Ni wajibu wetu sote kuheshimu sheria na kushirikiana na Tume hii, ili kuhakikisha kwamba tunatekeleza Uchaguzi Mkuu mwaka huu uwe huru na uwe na wa haki. Jambo hilo nitahakikisha linatokea na siyo vyenginevyo. (*Makofi*)

Kuanzia sasa ninataka nikwambieni kwamba macho ya ulimwengu yanatuangalia sisi. Tumefanya kazi na Mashirika mbali mbali duniani, nimetembea nchi mbali mbali duniani na kote tulikokwenda na wale wanaokuja Ikulu, wote wanaipa sifa

Zanzibar na uongozi wetu. Nasema sasa tusonge mbele kwa heshima na nia safi ya kuyaendeleza maendeleo yetu.

MASUALA MENGINEYO

AMANI NA USALAMA

Mhe. Spika, siri kubwa ya mafanikio yetu katika sekta zote za maendeleo nilizozielezea ni kuendelea kuimarika kwa hali ya amani na utulivu nchini. Kwa nyakati tofauti nimekuwa nikisisitiza sana umuhimu wa kusimamia amani na utulivu wa nchi yetu kwa vile ni rasilimali ya msingi ambayo kila mwananchi anapaswa kuilinda kuiendeleza na kuienzi kwa nguvu zake zote.(*Makofi*)

Katika hotuba yangu ya uzinduzi wa Baraza hili la Nane nilisema na ninajinukuu mwenyewe, nilisema hivi:

> *"*Suala la kudumisha amani si la Idara Maalum Na Vikosi vyetu vya Ulinzi Na Usalama peke yake, lakini linashirikisha wananchi wote kwa jumla."

Nimefarajika na mafanikio makubwa tuliyoyafikia katika kutekeleza wajibu wetu huo kwa vitendo. Katika kipindi chote cha miaka mitano, Idara Maalum za SMZ, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vimetekeleza vyema majukumu yao ya kusimamia ulinzi, amani na utulivu kwa kuhakikisha kwamba maisha ya watu wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla na mali zao yamekuwa salama. Napenda nitumie fursa hii kwa mara nyengine tena niwapongeza sana kwa utekelezaji mzuri wa dhamana zao hizo.(*Makofi*)

Mhe. Spika, hali ya amani na utulivu nchini imechangiwa sana na wananchi walio wengi kutambua kuwa vitendo vinavyosababisha kuvunjika kwa amani vina athari kubwa kwa maisha, uchumi na maendeleo ya ustawi wa maisha yao. Naamini kuwa wachache waliojaribu kuichezea amani kwa visingizio mbali mbali hawakuwa wakifurahiwa na wananchi wengine ila ni kwa sababu ya kukidhi malengo yao binafsi.(*Makofi*)

Napenda nisisitize kwamba kila mmoja wetu atilie maanani kwamba utii wa sheria ni hatua muhimu katika kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na amani, utulivu na kupata maendeleo zaidi. Kwa hivyo, ni jukumu la viongozi wote wa Serikali, wanasiasa, viongozi wa madhehebu mbali mbali wa Dini, viongozi wengine katika jamii na wananchi wote kwa jumla kutekeleza wajibu wetu wa kuhakikisha tunadumisha amani na utulivu na sheria tunazinafuata.

Kutii Katiba ya Zanzibar na sheria zake si jambo la hiari, si jambo ambalo mtu inabidi ajishauri bali ni wajibu wetu sote na msingi na hilo ni msingi muhimu wa kulinda amani na utulivu wetu. Nataka nikuhakikishieni, Waheshimiwa Wajumbe na niwahakikishie wananchi wote wa Zanzibar kwamba nitaendelea kuisimamia amani na utulivu kwa nguvu zangu zote. Nitaendelea kumchukulia hatua yeyote atakayejaribu kuivunja amani ya Zanzibar, sitokuwa na imani wala na amani na uvunjifu wa amani.(*Makofi*)

MUUNGANO

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba inatambua na inazingatia haja ya kuimarisha muungano wetu wa Tanzania kama nguzo ya pili muhimu baada ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964 kwa malengo yale yale ya waasisi wetu; Marehemu Mzee Abeid Amani Karume na Marehemu Baba wa Taifa; Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Ni dhahiri kuwa nguzo zetu hizi; Mapinduzi na Muungano yametuwezesha kupiga hatua kubwa za maendeleo yetu kisiasa, kiuchumi na kijamii na kuleta heshima ya Wazanzibari na Watanzania mbele ya mataifa mbali mbali katika kipindi cha miaka 51.(*Makofi*)

Katika kipindi hiki cha miaka mitano, Muungano wetu umezidi kuimarika kutokana na hatua zinazochukuliwa na viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hatua hizo ni pamoja na kuzifanyia kazi zile zinazotambuliwa kuwa ni kero za muungano. Masuala kadhaa yameshatatuliwa kupitia Kamati inayoongozwa na Mhe. Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inawajumuisha Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

Aidha, vikao vya kuimarisha mashirikiano ya kisekta kati ya Wizara za Serikali ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar, vimeendelea kufanywa na kuratibiwa kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, miongoni mwa mafanikio ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba, ni mchango wa Serikali katika mchakato wa kupata Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ulioasisiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa lengo la kuimarisha muungano wetu.

Kwa mara nyengine, napenda nimpongeze kwa dhati sana Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuanzisha mchakato wa Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kushirikiana mimi naye katika hatua zote na

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hatimaye kufikia kupatikana Katiba inayopendekezwa.(*Makofi*)

Sote tunatambua na tunathamini kazi nzuri iliyofanywa na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Katiba la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutupatia Katiba inayopendekezwa tuliyokabidhiwa mimi na Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 08 Oktoba, 2014 katika Uwanja wa Jamhuri pale Dodoma. Kazi iliyo mbele yetu wananchi wote ni kushiriki katika Kura ya Maoni wakati utakapofika, ili tuweze kunufaika na mambo mengi ya msingi yaliyozingatiwa katika kuandaa Katiba inayopendekezwa. *(Makofi)*

USHIRIKIANO NA NCHI NYENGINE NA WAZANZIBARI WANAOISHI NJE

Mhe. Spika, Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; imeendelea kushirikiana na nchi nyengine. Vile vile kitengo maalum kinachoratibu masuala ya Wazanzibari wanaoishi nchi za nje, kimeanzishwa kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maofisa wetu katika kipindi hiki wameshiriki katika mikutano mbali mbali ya kikanda.

Wazanzibari wanaoishi nchi za nje wamekua wakitoa michango mbali mbali ya fedha na kitaalamu hasa katika sekta ya elimu, afya, utalii, biashara na uwekezaji. Vile vile, Ofisi ya Rais Ikulu imeandaa utaratibu wa kukutana na Wana "Diaspora" kila mwaka kwa kualikwa Ikulu kubadilishana mawazo pamoja na Rais.

Uhusiano wetu umezidi kuimarika kwa kupata fursa ya kutembelewa na viongozi wa nchi kadhaa, taasisi za kimataifa, mabalozi na kufanya ziara katika nchi mbali mbali, mimi na viongozi wenzangu wakuu wa Serikali.

Kadhalika, kipindi hiki, cha miaka mitano nilipata fursa ya kufanya ziara za kuzitembelea nchi kadhaa kwa lengo la kuuimarisha uhusiano wetu.

Kwa nyakati tofauti nilikutana na Mabalozi, Wawakilishi wa taasisi mbali mbali za Kimataifa na viongozi wa nchi mbali mbali ambao walikuja kuonana nami na kufanya mazungumzo.

Katika mazungumzo yetu na viongozi hao tuliweza kuimarisha uhusiano wetu katika nyanja mbali mbali za maendeleo zikiwemo za kiuchumi na biashara, mazingira, elimu, na uimarishaji wa sekta ya afya na utamaduni na sekta ya utalii na nyengine mbali mbali. Faida ya makubaliano yetu hayo, zimeanza kupatikana katika utekelezaji wa mipango na miradi mbali mbali nchini.

MWISHO

Baada ya maelezo yangu ya kina ya utendaji na mafanikio ya Serikali ninayoiongoza tangu tarehe 3 Novemba, 2010 ambayo imetekeleza asilimia 90 ya Ilani ya Chama tawala, Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 – 2015, napenda kutoka shukurani zangu za dhati na zilizo nyingi sana kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kwa kunisikiliza kwa makini. Wakati leo nitalivunja Baraza hili rasmi, lakini safari yetu bado haijafika mwisho, na najua tumo katika matayarisho ya kuanza sehemu ya pili ya awamu hii. *(Makofi)*

Nachukua fursa hii kutoa shukurani kwenu nyote, kwa muda mlioutumikia kuzifanikisha shughuli za Baraza la Nane, kupitia vikao vya Baraza na Kamati zake mbali mbali. Sote tumetimiza wajibu wetu na tutaendelea kuwatumikia wananchi kila tutakapopata fursa ya kuwatumikia.

Mhe. Spika, natoa shukurani za dhati kwa wasaidizi wangu wakuu, Makamu wa Kwanza wa Rais; Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad na Makamu wa Pili wa Rais; Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa ushauri wao na kunisaidia katika kuzifanikisha kazi za Serikali katika utekelezaji wa kazi zetu za kila siku.

Kwa Balozi Seif Ali Iddi, namshukuru na nampongeza sana kwa kuziongoza na kuzisimamia kazi za serikali katika Baraza hili. *(Makofi)*

Kadhalika, shukurani zangu ziende kwa Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote, Katibu Mkuu Kiongozi wa Baraza la Mapinduzi, Makatibu Wakuu na Manaibu wao, Wakurugenzi, Watendaji na Watumishi wote wa Serikali, kwa ushirikiano walionipa na kwa kazi nzuri ya kuwatumikia wananchi.

Kadhalika, natoa shukurani maalum kwa Wajumbe na Watendaji wa Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Wilaya zote na Wananchi kwa jumla kwa ushirikiano walioipa Serikali katika utekelezaji wa mipango mbali mbali ya maendeleo. *(Makofi)*

Nathamini sana moyo wa uzalendo na kujituma waliouonesha wananchi pamoja na kuendeleza hali ya amani na mshikamano. Jambo hili limepelekea kuwepo kwa mashirikiano mazuri kwa Serikali na Wananchi katika kushughulikia masuala muhimu ya maendeleo.

Vile vile, kwa muda wote Serikali yetu imepata sifa kubwa katika kusimamia amani, utulivu na kuwaletea wananchi wake maendeleo. Sifa nyingi na shukurani hizo ambazo hufikishwa kwangu na Viongozi, Mabalozi na Washirika wetu wa Maendeleo ninaopata fursa ya kukutana nao ziwaendee wananchi wa Zanzibar.

Kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Wananchi wote napenda Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili mzipokee shukurani hizo kwa mchango wenu mkubwa na kwa kuunga mkono juhudi za Serikali za kutuletea maendeleo. Nasema ahsanteni Sana. *(Makofi)*

Nawatakia kheri wale Waheshimiwa ambao kwa sababu mbali mbali na kwa dharura maalum, na kwa ruhusa ya utawala bora, katika Baraza lijalo baada ya uchaguzi mkuu hatutokuwa nao. Wale wenye nia ya kurejea pamoja na wengine ambao sasa sio Wajumbe, nawasihi wazingatie utunzaji wa amani na utulivu katika harakati zao za uchaguzi. Huu ni wakati wetu sote, tudhihirishe ustaarabu wetu katika siasa zetu, umoja wetu na mshikamamo wetu. Tudhihirishe utiifu wetu wa sheria, utunzaji wa amani ni dhamana yetu sote. Kwa mara nyengine tena nasisitiza kwamba Serikali zetu mbili na vyombo vyake vya sheria, ulinzi na usalama havitomvumilia yeyote atakaehatarisha amani na kufanya fujo. Natoa wito maalum kwa vijana wasishawishike hata kidogo, kufanya fujo kwa sababu yoyote ile. Narudia tena, wasishawishike kufanya fujo yoyote kwa sababu yoyote ile. Watachukuliwa hatua zinazostaili na vyombo viliopo vya dola. Havitakuwa na mswalie Mtume na mtu yeyote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena natoa shukurani zangu za dhati kwako Mhe. Pandu Ameir Kificho, Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, kwa kuliongoza Baraza hili, wewe na msaidizi wako mkuu Naibu Spika, wewe na msaidizi wako mkuu Mwenyekiti wa Wenyeviti, wewe na wasaidizi wako wakuu Wenyeviti wote wa Baraza, Katibu wako na wasaidizi wote wa Baraza hili. Nyote mmefanyakazi kubwa ya kuendesha Baraza hili kwa uadilifu mkubwa.

Mhe. Spika, umetoa mchango mkubwa sana, katika kukuza demokrasia na utawala bora. Nakutakia kila la kheri katika maisha yako. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ili kutoa nafasi kwa matayarisho ya mwisho kwa ajili ya uchaguzi mkuu ifikapo tarehe 25 Oktoba 2015, kwa madaraka niliyo nayo kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 91 (2) (a) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, natamka kwamba kuanzia Alkhamis tarehe 13 Agosti 2015 Baraza la Nane la Wawakilishi limevunjwa rasmi. *(Makofi)*

Nakutakieni kila la kheri na Ramadhani njema.

MUNGU IBARIKI ZANZIBAR
MUNGU IBARIKI TANZANIA
MUNGU IBARIKI AFRIKA

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa hotuba yako nzuri sana, iliyochukua kiasi ya saa 2.50. Umeeleza mengi sana Mhe. Rais na makofi ambayo yalikwenda mfululizo wakati wote wa hotuba yako, inathibitisha Waheshimiwa Wajumbe hawa kuridhika na hotuba yako uliyotupa. Peke yake makofi hayo ni shukrani kwako kwa hotuba mwanana uliyoitoa katika kulivunja Baraza hili. *(Makofi)*

Sasa mimi niseme tu jambo moja na kwa kufuatana na muda kwamba Mhe. Rais nakushukuru sana. Nichukuwe nafasi pia kumshukuru sana Mhe. Jaji Mkuu kwa kuungana na sisi. Lakini Waheshimiwa Wajumbe pia niwashukuru wageni wetu, akiwemo Mhe. Mama Mwanamwema Shein, Mama Balozi Seif Ali Iddi, pamoja na wageni wetu wote ambao mlikuwa kimya kwa muda wote kusikiliza hotuba ya Rais. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, na nyinyi nakushukuruni sana, mmekuwa watulivu kwa muda wote mkisikiliza hotuba ya Rais. Hotuba hii imeelezea karibu mambo yote ya maendeleo yetu na hali ya nchi yetu. Narudia Mhe. Rais kukushukuru, muda hauko tena.

Kwa hivyo, nichukuwe nafasi hii kwanza Waheshimiwa Wajumbe, kuwakumbusheni, kwamba mara tukitoka humu ndani na kufanya shughuli hapo nje ndogo tu, tunaelekea Ikulu Mhe. Rais ametualika pale, tusije tukasahau, tukimaliza kazi hiyo hapo nje, ili tukamalize mafanikio ya hotuba na mambo yote aliyotayarishwa kwa ajili ya leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo sasa nichukuwe nafasi kurudia kuwashukuru wote na Baraza ndio limeshavunjwa. Kwa hivyo, kama Baraza limeshavunjwa hakuna hoja kwa jambo jengine, liliyobakia tutoke humu ndani baada ya kazi hiyo ya Mhe. Rais aliyoifanya.

Naomba sasa wimbo wa taifa upigwe.

(Saa 12:38 jioni Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, alitamka kwamba kuanzia siku ya Alkhamis ya tarehe 13 Agosti, 2015 Baraza la Nane la Wawakilishi amelivunja rasmi)

(Hapa Wimbo wa Taifa ulipigwa)